**30 OKTOBA, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

**Kikao cha Pili – Tarehe 30 Oktoba, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro.

Na. 20

**Serikali Kuongeza Pensheni ya Wastaafu Nchini**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza kiwango cha Pensheni kwa Wastaafu nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la kiwango cha Pensheni kwa Wastaafu hufanyika baada ya tathmini ya uhimilivu wa Mfuko kama ambavyo imeainishwa kwenye masharti ya Kifungu cha 57 cha Sheria ya *PSSSF* na Kifungu cha 71B cha Sheria ya *NSSF*. Tathmini hii hufanyika kila baada ya miaka mitatu au kipindi chochote inapohitajika kufanyika kwa tathmini hiyo. Kwa sasa Serikali inaendelea kufanya tathmini kama ilivyoelekezwa kwa mujibu wa Sheria za Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kupitia, Bunge lako Tukufu, Serikali inapenda kuwahakikishia Wastaafu kuwa itaendelea kufanya tathmini kwa lengo la kuboresha mafao kwa kuzingatia uhimilivu wa Mfuko na kwa mujibu wa Sheria husika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa gharama za maisha zimepanda na kuna wastaafu wanapokea pensheni chini ya shilingi 150,000 ambayo haiwatoshelezi kumudu gharama za maisha, ni kwa nini kima cha chini cha mshahara wa Serikali kilichowekwa hicho hicho kisiwe ndicho kima cha chini cha kutoa pensheni kwa watumishi ambao wanapokea pensheni kidogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa watumishi wanasubiri muda mrefu sana wa ku-*review* Sheria ya *PSSF* ambapo kwa jibu la msingi amesema ni miaka mitatu, haoni kwamba kuna haja ya kuwa inafanyika *review* kila baada ya mwaka mmoja badala ya watumishi kusubiria miaka mitatu hali ambayo inawafanya waendelee kuteseka? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika,

ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ndaisaba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kuhusu gharama za maisha kupanda ni sahihi, lakini utaratibu uliopo ni kwamba ni hesabu za kitaalam na kisayansi zinazoelekeza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Sheria zinazohusiana na masuala ya Hifadhi ya Jamii kufanyika kila baada ya miaka mitatu kwa sababu za kiuchumi, lakini pia kwa sababu ya kuwa na muda na kuweza kupata muda mzuri wa kuweza kupima uhalisia katika utoaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ni kwamba pia inategemeana na mshahara wa mtu wakati akifanya kazi katika kipindi chake cha utumishi na mishahara yake ya mwisho, ndiyo inaenda ku-*determine* kiwango cha pensheni anayopewa kila mwisho wa mwezi;

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwamba anataka kufananisha na jinsi ambavyo kima cha chini kinavyofanyika. Kima cha chini cha mshahara hufanyika kila mwaka; baada ya mwaka wa bajeti kukamilika inafanywa tathmini; na kuna Bodi maalum inayohusiana na Ushauri wa Masuala ya Uchumi na Jamii *(LESCO)* baada ya kufanya utafiti na uchunguzi kwenye maeneo ya mashamba, viwandani na maeneo yote kulingana na mfumuko huo wa bei au hali ya kiuchumi kama jinsi ambavyo alieleza ndiyo tuna-*determine* kuangalia kima cha chini cha mshahara, na *order* hiyo hutolewa kila mwaka. Hata hivyo, tayari Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni hili la kufanya *review* kila mwaka kwenye *Actual Evaluation*. *Actual Evaluation* ni tofauti na ufanyaji wa tathmini kwenye masuala ya kima cha chini cha mshahara, ni suala la kisayansi na mpaka sasa duniani kote sayansi inatuambia kwamba *Actual Evaluation* ifanyike kwa miaka mitatu *unless* kama itabadilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tuko tayari kufanya utaratibu huo, lakini hatukutaka kwenda tofauti na dunia inavyotaka, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, swali limechukua zaidi ya dakika sita. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, kwa niaba Mheshimiwa Zodo.

Na. 21

**Ujenzi wa Soko la Mgandini - Tanga**

**MHE. MWANTUMU M. ZODO K.n.y. MHE. UMMY A. MWALIMU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Mgandini katika Halmashauri ya Jiji la Tanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Majiji "*Green and Smart Cities*" imepanga kulijenga Soko la Mgandini katika Jiji la Tanga. Mpaka sasa kazi ya upembuzi yakinifu wa mradi ziko hatua za ukamilishaji, ambapo itafuatiwa na tathmini ya athari ya mazingira na usanifu wa michoro ya soko inayotarajiwa kukamilika mapema mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ratiba ya awali iliyotolewa na Jumuiya ya Ulaya mwezi Septemba, 2024, Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka 2027. Serikali imeanza majadiliano na Jumuiya ya Ulaya kwa lengo la kufanya marejeo ya ratiba za kazi zilizopangwa ili kuwezesha ujenzi wa soko hilo uanze mapema zaidi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zodo.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa soko hili linahudumia wananchi wengi na watu wa maeneo ya jirani kama vile Pemba na Comoro; kutokana na umuhimu wa soko hili, je, Serikali haioni haja ya kurudi tena mezani, kukaa na

mdau ili kuharakisha ujenzi wa soko hili angalau hata 2025? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa yako masoko mengine ya jirani ambayo miundombinu yake ni chakavu sana na wafanyabiashara wanaweka vyakula chini, soko kama vile la Makorora, Mlango wa Chuma na *Deep Sea*. Je, Serikali haioni haja ya kukarabati yale masoko mengine ya jirani? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba soko hili la Mgandini ni soko muhimu katika Jiji la Tanga na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Tanga Mjini, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu na Mheshimiwa Mwantumu Zodo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tanga wamekuwa wakifuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali pia inaona umuhimu wa kufanya majadiliano na Jumuiya ya Ulaya ili ujenzi wa soko hili uanze mapema iwezekanavyo. Hatua hiyo imeanza na tunaendelea na majadiliano ili ikiwezekana lijengwe mapema zaidi kabla ya 2027;

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele kwenye uboreshaji wa miundombinu mbalimbali yakiwemo masoko. Tumeshatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri kote nchini kuweka vipaumbele kwenye bajeti zao kwa masoko yale ambayo ni muhimu na yana hali mbaya. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi kumwelekeza na kumsisitiza Mkurugenzi wa Jiji la Tanga kuyaangalia masoko hayo ya Mlango wa Chuma, Makorora na mengine ili kuyaweka kwenye bajeti, lakini ikiwa bajeti haitoshi, pia kuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kutafuta fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imesema imewapa maelekezo Wakurugenzi kuhakikisha kwamba masoko yote yanajengewa miundombinu na yanakuwa na huduma muhimu; na kwa kuwa mpaka sasa yako masoko mengi kwenye Mkoa wa Tanga hayana huduma ya vyoo kabisa. Je, Serikali inapeleka maelekezo gani mahsusi kwa ajili ya miundombinu ya vyoo kwenye masoko hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, maelekezo ya Serikali ni kwamba masoko yote yanatakiwa kuwa na miundombinu yote muhimu vikiwemo vyoo. Suala la vyoo katika masoko yetu ni suala la muhimu na ni suala la dharura. Kwa hiyo, haikubaliki kuwa na masoko ambayo yanatumika na wananchi lakini hayana vyoo, kwani hii inahatarisha afya za wananchi na pia ni kinyume na taratibu na sheria ya afya ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumsisitiza Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, kuhakikisha wanafanya tathmini haraka iwezekanavyo na kutenga fedha katika hali ya udharura kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyoo hivyo ili masoko hayo yaweze kuhudumia wananchi ipasavyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

Na. 22

**Kupandisha Hadhi Zahanati ya Isagehe – Kahama**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza: -

Je, lini Zahanati ya Isagehe Kahama itapandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Zahanati ya Isagehe inahudumia wananchi wapatao 6,269 na ina eneo lenye ukubwa wa ekari nane ambalo ni dogo kwa ujenzi wa kituo cha afya ambapo zinahitajika angalau ekari 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa eneo la zahanati hii ni dogo kwa matumizi ya kituo cha afya; na kwa kuwa zahanati hii iko umbali wa kilometa tano kutoka katika Kituo cha Afya cha Kagongwa ambacho kinatoa huduma za upasuaji; Serikali itakiboresha Kituo cha Afya Kagongwa kwa kujenga miundombinu inayopungua zikiwemo wodi ili kiweze kuwahudumia wananchi wa kata jirani ikiwemo Kata ya Isagehe? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hii ya Isagehe inahudumia zaidi ya watu 15,000 lakini imezungukwa na Jimbo la Bukene na kata jirani za Mkoa wa Tabora na inahudumia zaidi ya watu 48,000. Je, endapo itapatikana ekari 15, Serikali iko tayari kujenga kituo cha afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kama ulivyosema katika jibu lako la msingi kwamba Kata ya Kagongwa ina kituo cha afya ambacho kinatoa huduma za upasuaji, lakini hakuna wodi za kutosha kuwahudumia. Je, Serikali iko tayari kujenga na kuboresha Kituo cha Afya cha Kagongwa kuwa na wodi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ujenzi wa vituo vya afya kwa mujibu wa Mwongozo wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Afya, tunajenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati na kigezo kimojawapo ni umbali kutoka kituo cha afya cha jirani unaozidi

kilomita 15, lakini pamoja na hayo kuna mazingira ambayo yanalazimisha kujenga kituo cha afya hata kama umbali ni chini ya kilomita tano, kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge, Dkt. Christina Mnzava kwamba tutalifanyia tathmini kuona idadi ya wananchi watakaonufaika kama kituo cha afya kitajengwa katika kata hiyo ya Isagehe na baada ya hapo tutaona utaratibu wa kuanza ujenzi wa kituo hicho ikiwa itakidhi vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni kweli Kituo cha Afya cha Kagongwa hakina miundombinu mbalimbali inayohitajika ikiwemo wodi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumekuwa tukijenga vituo vya afya hivi kwa awamu, tunakamilisha majengo ya kwanza ya msingi, lakini baadaye tunaendelea na majengo mengine zikiwemo wodi na tayari imewekwa kwenye mpango kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko, Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Zahanati nyingi katika Jimbo la Karatu zina uchakavu wa miundombinu, ukosefu wa madawa, upungufu wa watumishi, ukosefu wa umeme na kadhalika. Nini mkakati wa Serikali kuisaidia halmashauri ili iweze kuondoa upungufu huo uliopo katika zahanati husika? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, zahanati zote ambazo zina uchakavu tunaziwekea mpango mkakati kwa ajili ya ukarabati. Tumeanza ukarabati wa hospitali za halmashauri 59, tunakwenda ukarabati wa vituo vya afya 212, na tutaendelea na ukarabati wa zahanati zote. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba zahanati za Jimbo la Karatu ambazo ni chakavu nazo tutaziainisha, tutaziwekea mpango kwa ajili ya kuzikarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Serikali imeendelea kuajiri watumishi na kuwapeleka kwenye zahanati zetu zenye upungufu wa watumishi, ununuzi wa dawa na vifaa tiba unaendelea na Mheshimiwa Rais ametoa zaidi ya shilingi bilioni 230 ndani ya mwaka huu wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba, dawa na vitendanishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba tutaendelea kutoa kipaumbele kwenye zahanati hizo ili ziweze kupata vifaa tiba, vitendanishi, dawa, watumishi pamoja na mpango wa ukarabati, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kembaki.

Na. 23

**Kuongeza Miundombinu na Vifaa Tiba
Hospitali ya Wilaya Tarime**

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza miundombinu na Vifaa Tiba katika Hospitali ya Mji Tarime kutokana na kuelemewa na Wagonjwa kutoka maeneo ya jirani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya majengo na vifaa tiba katika Hospitali ya Mji Tarime, ambapo katika mwaka 2023/2024, Serikali ilipeleka shilingi milioni 900 katika Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa ajili ya ukarabati wa hospitali. Fedha hiyo imetumika kujenga wodi ya wazazi, jengo la kuhifadhia maiti na kichomeataka ambapo ujenzi uko 40%.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 Serikali imetoa shilingi bilioni 1.05 kwa ajilli

ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa dharura *(EMD)* na ununuzi wa dawa vitendanishi na vifaa tiba katika Hospitali ya Mji wa Tarime, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kembaki.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika hospitali yetu ya Wilaya ya Tarime kwa maana miundombinu mingi imeboreshwa. Tuna changamoto moja; kuna wingi wa wagonjwa wanaotoka katika Wilaya nyingine kama Rorya, Tarime Vijijini na wengine wanatoka katika nchi jirani ya Kenya, hali inayoleta upungufu wa madawa katika Hospitali yetu ya Wilaya. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba inaongeza fedha ya kununua dawa ili kutatua tatizo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sera na Miongozo ya Wizara ya Afya, huduma kwenye vituo vyetu vya huduma za afya hazina mipaka kwa maana ya ndani ya nchi. Kwa hiyo, wananchi wanaotoka halmashauri moja wana uhuru wa kutibiwa halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika katika kutoa dawa, vitendanishi na vifaatiba, bajeti inategemeana na taarifa za idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa katika hospitali husika. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kusisitiza Menejimenti ya Halmashauri ya Mji wa Tarime, Mkurugenzi, na Mganga Mkuu wa Halmashauri kutoa taarifa sahihi za idadi ya wananchi wanaotibiwa kwenye hospitali hiyo ambazo zitaweza kutu-*guide* kuwaletea bajeti inayotosheleza dawa, vitendanishi na vifaatiba kulingana na idadi kubwa ya wananchi wanaotibiwa hapo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kikoyo bado una swali?

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii, japokuwa swali kama limejibiwa na maswali ya watu wengine, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mbogo.

Na. 24

**Ukarabati Shule za Msingi katika Vijiji vya Kalundi, Lyapinda na Londokazi**

**MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati Shule za Msingi katika Vijiji vya Kalundi, Lyapinda na Londokazi Nkasi kusini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2022/2023 hadi 2023/2024, Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya ukarabati, ambapo shilingi bilioni 70.39 zimetolewa kwa ajili ya ukarabati wa shule 793 zikiwemo Shule za Msingi Chalantai, Nkundi na Sintali za Jimbo la Nkasi Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ukarabati wa shule chakavu zikiwemo shule za msingi katika Vijiji vya Kalundi, Lyapinda na Londokazi kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja. Shule ya Milundikwa, Nkomachindo, Chala B na Kasu zina maboma ambayo hayajaisha, na vyoo havipo kabisa. Lini Serikali itapeleka

fedha ili kujenga maboma, kuweza kuyapaua pamoja na fedha kwa ajili ya kujenga vyoo?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake lenye nia ya kuboresha Sekta ya Elimu katika jimbo lake. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imefanya tathmini ya maboma ambayo hayajakamilika kwa ajili ya miundombinu ya shule zetu, na pia imefanya tathmini nchi nzima na kubaini kiwango cha fedha kinachohitajika kwa ajili ya kukamilisha maboma haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pindi fedha zitakapokuwa zimepatikana, tayari kuna mpango wa kuhakikisha kwamba maboma haya yote yanajengwa ili wanafunzi wetu na watoto wetu waweze kupata miundombinu iliyo bora ya kupatia elimu. Nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kuwa na kwenye jimbo lako fedha hizo zitafika kwa ajili ya kukamilisha maboma haya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kutokana na shule nyingi za Wilaya ya Hai kujengwa kuanzia mwaka 1952 na kuendelea, shule takribani 77 ni chakavu sana na tuliandika andiko maalumu TAMISEMI kuomba Serikali itusaidie fedha za ukarabati wa Shule ya Chemka, Lerai, Kilanya, Kimbushi, Kisereni, Kware, Kyuu, Lambo - *Extended*, Masama, Bwera na Mroma.

Je, ni lini sasa Serikali italeta fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule hizi chakavu pamoja na shule nyingine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli

mara nyingi amekuwa akisemea changamoto za wapigakura wake na hasa kwenye sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mwaka huu wa fedha imetenga fedha mahususi kabisa kwa ajili ya kuzifikia shule hizi kongwe ambazo ni chakavu. Kwa hiyo, katika tathmini zinazofanyika zikikamilika tutahakikisha tunaweka kipaumbele katika shule alizozitaja ambazo zipo katika Jimbo lake ili ziweze kupata mgao wa fedha kwa ajili ya kuzirekebisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Kamamba.

Na. 25

**Hitaji la Ofisi ya TAKUKURU - Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Ofisi ya TAKUKURU Wilayani Kakonko?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuiimarisha TAKUKURU, imekuwa ikitenga fedha kwenye bajeti ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya ofisi kulingana na mpango wa ujenzi wa TAKUKURU na uwezo wa kibajeti. Ujenzi wa ofisi katika Mikoa na Wilaya huzingatia vigezo mbalimbali ikiwemo kigezo cha Wilaya zilizopo pembezoni mwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali ilitumia shilingi bilioni 4.5 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Mikoa na Wilaya na katika mwaka 2024/2025 kiasi cha shilingi bilioni sita kimetengwa kwa ajili hiyo. Kwa kuzingatia mpango wa ujenzi, vigezo na upatikanaji wa bajeti, ujenzi wa jengo la Ofisi ya TAKUKURU katika Wilaya ya Kakonko

unatarajiwa kuzingatiwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha wa 2025/2026. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamamba.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri. Wilaya ya Kakonko ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimeanzishwa hivi karibuni, sasa hivi ina changamoto kubwa ya miundombinu ya nyumba na usafiri kwa watumishi wa taasisi mbalimbali katika Wilaya.

Swali la kwanza, je, lini Serikali itajenga nyumba za watumishi wa TAKUKURU katika Wilaya ya Kakonko?

Swali la pili, lini Serikali itapeleka usafiri wa uhakika kwa watumishi wa TAKUKURU katika Wilaya ya Kakonko? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Aloyce Kamamba kwa namna anavyofuatilia masuala yanayohusiana na TAKUKURU. Naomba nimhakikishie, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi kwamba tuna mpango wa kujenga ofisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kwa hiyo, ujenzi wa ofisi hizo utaambatana na ujenzi wa nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, tutakapokuwa tunatakeleza bajeti hiyo na jambo hilo litazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili ameuliza juu ya usafiri. Ni kweli tulikuwa na changamoto kubwa ya usafiri nchi nzima kwenye Taasisi yetu ya TAKUKURU. Mheshimiwa Rais aliliona hilo na ameidhinisha fedha za ununuzi wa magari yapatayo 195. Juzi tarehe 26, Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa pale Moshi kwenye Mahafali ya TAKUKURU alikabidhi awamu ya kwanza magari 88.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Aloyce, tunajua changamoto ya Kakonko katika mgao wa magari haya, tutazingatia naye kupata mgao kwa kadri tutakavyokuwa tunapata hayo magari, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Uyui ndiyo Wilaya pekee TAKUKURU wanakaa Wilaya nyingine na wanafanya kazi Wilaya nyingine. Je, ni lini Halmashauri ya Wilaya ya Uyui itajengwa ofisi kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Venant kwa kufuatilia mambo yanayohusu TAKUKURU na kwa bahati nzuri hivi karibuni nilikuwa ziarani Mkoani Tabora, nilitembelea katika Wilaya yake. Nimhakikishie kati ya Wilaya ambayo nilipokea changamoto, nao tumewaingiza kwenye mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Tutakapokuwa tumeanza, nao tutawapelekea fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na nyumba za watumishi wa TAKUKURU.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tanganyika ni miongoni mwa Wilaya ambazo hazina Ofisi ya TAKUKURU na nimekuwa nikiuliza swali hili mara kwa mara. Je, ni lini mtaenda kujenga Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nikienda moja kwa moja, kama nilivyojibu kwenye maswali mengine juu ya ujenzi wa ofisi za TAKUKURU, Serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha Wilaya zake zote zinapata majengo ya ofisi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso, hata huko

Tanganyika tutafika na tutaizingatia kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge wote mliouliza maswali ya TAKUKURU, kiti kinawapa maua yenu, hongereni sana. Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Gwajima. *(Makofi)*

Na. 26

**Mpango wa Kuhakikisha kila Awamu inatekeleza Maono ya Dira 2050**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kila awamu inatekeleza maono ya Dira ya Taifa 2050?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa Dira inayopendekezwa na Serikali inatekelezwa katika kipindi chote cha uhai wake, Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia kanuni zake, shughuli za Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge pamoja na shughuli zake pale linapokaa kama Kamati ya Mipango litahusika katika kuisimamia Serikali kutekeleza Dira ya Taifa 2050 na kuhakikisha kila awamu inatekeleza maono ya Dira 2050. Hivyo, ni matarajio ya Serikali kuwa awamu zote za uongozi zitatekeleza maono ya Dira 2050 kwa kuwa ni takwa la kikatiba na kisheria, na pia Bunge litakuwa linahusika katika kusimamia utekelezaji wake, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali ipo katika mchakato wa kuandaa Dira ya Taifa au maono ya Taifa ya muda mrefu 2050, je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba kila Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Siasa inalenga maono ya Taifa ya muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge swali hilo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba tunapoandaa Dira ya Mwaka 2050, tunaiandaa kwa maana ya kwamba ni dira ya muda mrefu wa miaka 25, na utekelezaji wake unatekelezwa kwa awamu. Tunaivunja katika miaka mitano mitano na katika kila awamu katika miaka mitano kunakuwa na Mpango wa mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali kuhusu vyama vya siasa, nadhani ni utashi wa chama cha siasa kuisoma Dira ya Mwaka 2050 na mambo yake na kuja na ilani inayoelekeza ni namna gani ilani hiyo ya chama hicho itakwenda kutekeleza na kufanikisha yale ambayo yamo ndani ya Dira ya Mwaka 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni utashi wa chama cha siasa na kitakwenda kujiuza na kujinadi kwa wananchi, wananchi wakielewa kama wanavyokielewa Chama cha Mapinduzi watapigia kura chama hicho na chama hicho kitatekeleza hiyo Ilani au Dira ya Mwaka 2050.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Dira ya Taifa ya 2050 inahusisha vipi wanawake na vijana katika maendeleo ya uchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda au tuko katika mchakato wa kukusanya maoni ya Dira ya Mwaka 2050. Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba tumeshaanza kukusanya maoni kutoka kwa wananchi, tumeshaanza kukushanya maoni kutoka kwa viongozi wastaafu na viongozi walioko madarakani na keshokutwa siku ya tarehe 02 Bunge lako Tukufu litapewa hali halisi *(status)* ya maoni yalivyo na Bunge lako litakwenda kutoa maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nieleze kwamba haya yote aliyozungumza Mheshimiwa Mbunge, wakiwemo wakina mama, tumeyapa kipaumbele kikubwa kwa maana ya kumwendeleza Mtanzania awe mwanaume au mwanamke. Vilevile, kuhusu nchi tunataka iweje mwaka 2050; na jamii ya Kitanzania tunataka iweje mwaka 2050; pia mtu mmoja mmoja tunataka aweje mwaka 2050; haya yote tumeyazingatia na yamo katika dira ya mwaka 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu ni kwamba wananchi wote waendelee kutoa maoni yao ili tuboreshe dira ya mwaka 2050 na iende kutekelezwa kwa maslahi na maendeleo ya Taifa letu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Francis Koka.

Na. 27

**Fidia kwa Wananchi waliopisha Mkondo wa Umeme k*VA* 400 - Kibaha**

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi na Kampuni 18 za viwandani na Zegereni Mji wa Kibaha waliopitiwa na umeme wa *kVA* 400?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza Mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Mkuranga kupitia Kinyerezi. Katika awamu ya kwanza ya ulipaji fidia katika mradi huo, kiasi cha shilingi bilioni 29.4 kati ya shilingi bilioni 33 kimelipwa kwa wananchi walioathiriwa na mradi huu kwa sehemu ya Chalinze - Kinyerezi. Aidha, katika eneo la viwanda la Zegereni kuna wananchi na kampuni 18 ambao wanadai fidia yenye thamani ya shillingi bilioni 1.1 na fidia hii italipwa fedha zitakapopatikana, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Koka.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu hayo mazuri ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa walisimamishiwa maendeleo yao kuanzia mwaka 2015 na wakalipwa mwaka 2022 na hawa wakabaki. Swali la kwanza, je, leo mwaka 2024 ni miaka 10, Serikali haioni kwamba utaratibu huu ni kinyume cha sheria na taratibu za ulipaji fidia kwa wananchi hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wananchi hao waliobaki ni wachache, na fidia ni takribani shilingi bilioni 1.1, kwa nini sasa Serikali isilipe fidia hii ndani ya miezi sita kuepuka tena uthamini mwingine au wananchi hawa kuendeleza maeneo yao na kusababisha gharama kubwa kwa Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Fidia ambazo zinalipwa kwa wananchi zina taratibu zake na kama ni fidia ambazo zimekaa muda mrefu, *review* huwa zinafanyika, kisha fedha inayolipwa inalipwa kulingana na taratibu ambazo zipo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, fedha ile ya awali ambayo imelipwa ambayo ni takribani shilingi bilioni 29.4 ililipwa kwa mujibu wa sheria na

taratibu, na kwa kweli tunawashukuru wananchi kwa kuendelea kutuvumilia kwa kipindi hicho na kuruhusu miradi hii iweze kupita kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu fedha kulipwa ndani ya miezi sita, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa dhamira ya Serikali ni kuhakikisha tunalipa fidia hizi. Tutaendelea kuongea na wenzetu wa Wizara ya Fedha juu ya kuona kipaumbele cha kulipa fidia hii ambayo imebakia ya takribani shilingi bilioni 1.1 na wananchi hawa watalipwa fedha hizo. Wananchi waendelee kutuvumilia na waendelee kupisha miradi iweze kufanyika na sisi Serikali tutahakikisha fidia yao inalipwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Swalle, jiandae Mheshimiwa Sanga.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kata ya Kichiwa eneo la Igumila na sehemu ya Luhuki kule Idamba wanaidai fidia Serikali ambapo pia wanajenga bwawa la umeme. Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wananchi ambao wanaidai Serikali? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Fidia hii tunaendeleo kuifanyia kazi na tutahakikisha tunaendelea kuifanyia tathmini na fidia hii inalipwa kwa wakati kwa wananchi hawa ambao wamepisha maeneo yao kwa ajili ya mradi huu wa umeme, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa mara ya tatu leo nauliza. Wananchi wa Jimbo la Makete walipisha ujenzi wa bwawa kubwa la umeme, Rumakali, na tayari *demacation* na tathmini ishafanyika. Wananchi hawa hawaendelei na shughuli za kiuchumi kwa sababu wamewasimamishwa. Je, ni lini Serikali itawalipa fedha wananchi hawa ili waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi kwenye

maeneo mengine kwa sababu hadi sasa hivi wako *stranded,* hawajui nini cha kufanya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali. Fidia hii ambayo Mheshimiwa Mbunge anaulizia ni kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Rumakali ambapo fidia yake ni takribani shilingi bilioni 27. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, taratibu za kulipa fidia hii zinaendelea, nasi tunaliwekea jambo hili umuhimu sana kwa sababu Rumakali pamoja na Ruhuji ni mabwawa ambayo yataenda kuzalisha takribani megawati karibia 500. Kwa hiyo, yana umuhimu sana kwenye sekta yetu ndogo ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Makete kuwa tunalifanyia kazi na watalipwa fidia yao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

Na. 28

**Matumizi ya Gesi kwa Magari na Mitambo Nchini**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha upatikanaji wa huduma ya gesi kwa matumizi ya magari na mitambo nchini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishaanza programu mbalimbali za matumizi ya gesi iliyogandamizwa (*CNG)* kwenye magari. Mpaka sasa Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imefanikiwa kufungua vituo vitano na inatarajia kufungua vituo vingine vitatu ifikapo mwezi Desemba, 2024. Aidha, jumla ya vituo 13, vituo mama viwili, vituo vya kuhamishika sita na vituo vidogo vitano vinatarajiwa kufunguliwa mwaka 2025, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Soud.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa huduma hii inaonekana zaidi kulenga maeneo ya majiji na zaidi Dar es Salaam, je, Serikali ina mpango gani wa kupanua wigo wa huduma hii katika maeneo mbalimbali ikiwemo Mikoa na Wilaya nchini?

Swali namba mbili, kama unavyojua kwamba Zanzibar na Tanzania Bara tuna ufanisi mzuri sana katika biashara ya umeme. Sasa nataka kujua je, Wizara ina mpango gani wa kuweza kuiga mfano mzuri wa *TANESCO* kuweza kupeleka huduma hii Zanzibar ili kupanua wigo wa kibiashara katika suala zima la *CNG? A*hsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwenye swali la kwanza la kupanua wigo tayari tumeshaanza kulifanyia kazi. Kwanza, vituo hizi ambavyo vinahamishika kuna baadhi vitakuja Dodoma. Vilevile, tumeanza kufanya mawasiliano na *GPSA* na tumeshaanza kufanya tathmini kuweza kuona tunaweza kuweka vituo kati ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma. Kwa hiyo, tumeanza kufanyia kazi kuweka vituo hivi nje ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ni hatua, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mikakati tunayo na azma ya kuhakikisha tunaendeleza matumizi ya nishati (hii gesi) kwenye magari nje ya Mkoa wa Dar es Salaam na tayari tunaifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la ushirikiano na kupeleka kituo hiki Zanzibar, mikakati ipo, ni kwa sababu tu maendeleo ni hatua, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa azma yetu ni kuhakikisha ajenda hii ambayo Mheshimiwa

Rais ameibeba kwa dhati ya moyo wake, tayari tumeshaanza kutekeleza mkakati wa miaka kumi mpaka 2034 inatekelezeka kwa ufanisi na ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaendelea na mikakati kuhakikisha pande zote mbili za Muungano zinanufaika na rasilimali hii ambayo tunayo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Shangazi.

Na. 29

**Utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji – Mlalo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, lini Miradi ya Umwagiliaji itaanza kutekelezwa katika Jimbo la Mlalo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu za umwagiliaji zilizopo katika Bonde la Umba lililopo katika Jimbo la Mlalo. Skimu hizo zinajumuisha Kwemgiriti (hekta 1000), Kituanimwenzae (hekta 1,000) na Kitivo (hekta 800). Aidha, ujenzi wa Skimu hizi utaanza baada ya taratibu za manunuzi ya mkandarasi kukamilika katika mwaka wa fedha 2024/2025. Kukamilika kwa ujenzi wa skimu hizo kutawanufaisha wakulima 1,107, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, Skimu hii ya Kituani imeharibika kutokana na mvua za mafuriko zilizopita mwaka huu 2024. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kupeleka fedha za dharura angalau

kwa kurekebisha skimu hii ili wananchi waendelea na shughuli zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Tuna mifereji ya asili ya Hambalawei katika Kata ya Lukozi na Shundai katika Kata ya Mwangoi ambayo mwanzoni nayo pia ilifanyiwa kipaumbele. Ni lini ujenzi katika mifereji hii ya asili utaanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupeleka fedha katika Skimu ya Kituani ambayo ilikuwa imeharibika, tumeshawatuma tume kwa ajili ya kwenda kufanya tathmini ili sisi kama Wizara tutafute fedha na tuweze kufanyia marekebisho kabla ya msimu wa mvua kwisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ambayo yanahusu mifereji ya asili ambayo Mheshimiwa Mbunge anahitaji yajengewe, nayo ni lazima tuyafanyie upembuzi yakinifu na baada ya hapo tuyaingize katika mipango yetu ili tuweze kuwasaidia wananchi. Kwa hiyo, awamu ya kwanza ni hiki ambacho tumekijibu katika jibu la msingi ambayo tutayaingiza katika mpango wetu wa awamu ya pili, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi karibuni tulipata ahadi ya kuendeleza miradi nane ya umwagiliaji katika Wilaya ya Nyasa, ni lini tunategemea kuanza miradi hiyo, hasa ule wa Lundo ambao tayari wananchi walishathibitishiwa kuwa watapata shilingi bilioni 25.4?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Nyasa, ipo miradi ambayo ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu, mingine ipo katika hatua ya kumtafuta mkandarasi na mingine mkandarasi alishapatikana, tunachosubiri ni hatua ya mwisho ya *vetting* ili tuwakabidhi wakandarasi *site* na waanze

kazi. Kwa hiyo, ninamthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi zote na ahadi ambazo Serikali ilizitoa tutazitekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ya kwamba lazima upembuzi yakinifu ufanyike katika maeneo ambayo yameharibika katika skimu za umwagiliaji, lakini skimu ya umwagiliaji ya Bahi haijafanyiwa ukarabati siku nyingi na kuna maeneo ambayo yanatakiwa yafanyiwe ukarabati. Je, Serikali na mwaka huu imeshindwa kufanya ukarabati kama ilivyodhamiria? Haiwezi ikaja ikafanya ukarabati katika maeneo korofi ili angalau kuleta ahueni kwa wananchi kupata mavuno katika msimu ujao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Bahati nzuri kutokana na umuhimu na ukubwa wa skimu ya Bahi sisi Wizara tumeifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa lengo la kuijenga upya ili isiwe inaharibika mara kwa mara. Skimu hii imeshatangaziwa mkandarasi na Mheshimiwa Mbunge anafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakachokifanya sisi ni kuharakisha *process* ili mradi huu uweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati, jiandae Mheshimiwa Mabula.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tangu tarehe 5 Aprili, 2023 mpaka leo Skimu ya Umwagiliaji ya Ruaha Mbuyuni iliacha njia ikachepuka kutoka kwenye mkondo wake, mpaka sasa hivi wananchi wanaishi kwenye maisha magumu, je, ni lini sasa marekebisho yatafanyika ili wananchi wale waweze kuishi maisha yenye amani na furaha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Ruaha Mbuyuni ni kama ambavyo nimejibu kwenye Skimu ya Bonde la Bahi kwamba ni moja ya skimu kubwa ambazo marekebisho peke yake hayatoshi kuifanya iendelee kudumu. Kwa hiyo, sisi kama Wizara, skimu ya Ruaha Mbuyuni tumeitangaza katika tenda ili tuweze kuijenga upya kabisa na iwe ya kudumu kwa siku zote. Kwa hiyo, skimu hii ipo katika mpango huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Mabula jiandae Mheshimiwa Jesca.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, Wilaya ya Ilemela imezungukwa na Ziwa Victoria na kando kando kuna mabonde mazuri ambayo yangeweza kuwa na kilimo cha umwagiliaji na mavuno angalau mara tatu kwa mwaka. Je, ni lini Serikali itawezesha miundombinu ya umwagiliaji, kutoa maji katika Ziwa Victoria kwenda kwenye yale mabonde ya kilimo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri kuhusu matumizi ya maji ya Ziwa Victoria, tuna mradi mkubwa sana ambao Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Mifugo tunafanya kazi pamoja. Sasa hivi wako katika hatua ya kutengeneza usanifu wa kina juu ya mchoro ambao utafanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawathibitishia watu wote wa Kanda ya Ziwa kwamba mradi huu utakapokuwa umekamilika, sisi Wizara ya Kilimo tutatumia, Wizara ya Maji watatumia na Wizara ya Mifugo na Uvuvi vile vile. Kwa hiyo, jambo hili lipo katika mpango wa Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya tatu, namwomba tena Mheshimiwa Waziri, kama

wanaweza kutusaidia kama Serikali kuifanyia ukarabati Skimu ya Mkoga iliyopo ndani ya Mji wa Iringa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge alituomba jambo hili. Sisi tumeshatuma wataalam, wanaendelea kufanya tathmini, kwa sababu kikubwa ni lazima tufanye tathmini ili tujue ukubwa wa changamoto ya bwawa na gharama halisi ambazo zinahitajika katika ujenzi. Kwa hiyo, ninamthibitishia kwamba Serikali tumelichukua hilo kwa umuhimu mkubwa na tutalifanyia kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kuwa 90% ya maisha yetu wananchi wa Wilaya ya Nkasi ni kilimo. Eneo lililopimwa ambalo linafaa kwa umwagiliaji ni hekta 6,145, maeneo ambayo mpaka sasa wamepeleka fedha ni hekta 3,300. Je, ni lini watamalizia hekta 2,845 ili nasi Wanankasi tuendelee na kilimo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunafanya kazi kwa awamu na bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge anafahamu na mradi wake unaendelea. Tutakachokifanya sisi baada ya kumaliza awamu ya kwanza, upo mpango wa kuongeza ukubwa kufikia ile hekta 6,400 ambayo Mheshimiwa Mbunge ameieleza. Kwa hiyo, ni sehemu ya mipango ya Serikali kuhakikisha kwamba wakulima wa Nkasi wanakuwa na maji ya uhakika na mradi wao unakamilika kwa wakati ili waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hili lipo katika mipango yetu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Mheshimiwa Shekilindi.

Na. 30

**Ujenzi wa Minara ya TBC – Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano ya TBC – Lushoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, matangazo ya redio za *TBC* yanapatikana Lushoto kupitia mitambo ya *TBC* iliyofungwa katika mnara wa kituo cha redio cha Utume *FM* kilichopo katika kata ya Kwemashai. Hivyo *TBC Taifa* inapatikana kwa masafa ya *87.9MHz* na *Bongo FM* kwa masafa ya *89.9MHz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na jiografia ya Wilaya ya Lushoto, kuna maeneo hayapati matangazo ya redio na maeneo mengine usikivu ni hafifu. Hivyo, kupitia Mradi wa Mawasiliano Vijijini Awamu ya Kwanza *(Rural Connectivity Phase I),* Lushoto ni miongoni mwa Wilaya zitakazonufaika na mradi huo kwenye maeneo ambayo kwa sasa hayapati usikivu, ambapo kituo cha kurushia matangazo ya redio kinatarajiwa kujengwa katika Kata ya Ngwelo, ambapo usikivu wake utafika maeneo yote ambayo hayapati matangazo ya redio na yale yenye usikivu hafifu. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, hasa katika Jimbo la Lushoto kujengewa mnara kwenye

Kata ya Ngwelo, naishukuru sana Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto ya mawasiliano ya simu katika Kata za Ngwelo, Makanya, Kilole pamoja na Malibwi. Je, ni lini Serikali itajenga mawasiliano ya simu katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naishukuru Serikali imejenga mnara wa mawasiliano ya simu katika Kata ya Ubili, lakini mnara ule mpaka sasa una zaidi ya miaka mitatu haufanyi kazi. Nilikwenda kwa Mheshimiwa nikamwambia kuwa wataalam wameenda kule lakini bado mpaka sasa hivi mnara haufanyi kazi. Je, ni lini mnara ule utafanya kazi ili wananchi wangu wa Kata ya Ubili waweze kupata mawasiliano? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mradi wa *Digital Tanzania* ambao unajenga minara 758 ambayo tayari Wizara imeandaa taarifa na itapatikana kwa Waheshimiwa Wabunge kwenye Bunge hili. Namwomba Mheshimiwa Mbunge apitie taarifa hiyo na aone kama maeneo yake yanafikiwa na mradi huo. Kama hayafikiwi nitawaelekeza wataalam wa *UCSAF* wafike jimboni kwake ili waone maeneo ambayo ameyataja kama yataweza kuingizwa kwenye mradi wa *Rural Connectivity Phase I*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mnara uliojengwa ambao haufanyi kazi namwomba Mheshimiwa Mbunge mara baada ya maswali na majibu tukutane ili tuweze kulifanyia kazi kwa pamoja. Nimhakikishie kwamba mnara huo utawashwa na kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na changamoto ya usikivu wa redio hasa *TBC Taifa* katika Jimbo la Newala Vijijini, na ni changamoto ya muda mrefu. Je, ni lini Serikali itafanya maboresho katika Jimbo la Newala Vijijini ili vipindi vya redio vya *TBC* viweze kusikika kwa uhakika? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtanda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa kujenga mitambo ya kuongeza usikivu wa Redio ya Taifa kwa miradi 29. Vilevile, kuna mradi wa *Rural Connectivity Phase I* utakaokuwa na miradi 15 ya kujenga mitambo ya kuongeza usikivu. Pia kupitia *UCSAF* tuna miradi mitano. Namwomba Mheshimiwa Mtanda awe na subira. Tutawasiliana naye tuone kama eneo lake; na ikiwa jimbo lake la Newala halitakuwa kwenye miradi hii 29 inayotekelezwa kwa sasa tutahakikisha kuwa kwenye ile miradi 15 ya *Rural Connectivity Phase I* eneo la Newala nalo linaguswa kwa sababu ni maelekezo ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha usikivu wa *TBC* unapatikana kwenye maeneo yote nchini kufikia mwaka 2025. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, jiandae Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Mkoa wa Lindi ni miongoni mwa mikoa michache ambayo haijafikiwa na *TBC Radio*, hususan Wilaya ya Liwale. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutupelekea matangazo ya redio kwenye maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumthibitishia

Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale kwamba Wilaya ya Liwale ipo kwenye miradi 29 inayotekelezwa sasa, na tayari mitambo imeshaagizwa na kufika. Namthibitishia kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu Wilaya ya Liwale mtambo wake utawashwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na shida ya mawasiliano ya simu Mbinga, na ni muda mrefu, lakini hali hiyo imekuja hadi hapa Dodoma. Watu wanataka kutoa fedha hazitoki, wanataka kutuma fedha haziendi, lakini hata kupiga simu ni shida, takribani mitandao yote nchi nzima. Shida ni nini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na shida tangu siku ya Jumapili na tulipata malalamiko makubwa kutoka mtandao wa *Vodacom* ambao walikuwa wanaboresha mfumo wao wa *billing system*. Tayari nimewaelekeza *TCRA* kufanya tathmini ya suala lenyewe kama kweli ni suala la kiufundi au kama kuna aina yoyote ya uzembe kutokana na leseni waliyopewa wenzetu wa *Vodacom* na nimeagiza *TCRA* wachukue hatua. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mohamed Monni.

Na. 31

**Mradi wa Maji Kijiji cha Igunga – Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatoa shilingi za Kitanzania 300,000,000 kwa ajili ya mradi wa maji Kijiji cha Igunga kutoka chanzo cha Ntomoko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mpango na bajeti kwa mwaka 2024/2025, Serikali itatekeleza mradi wa kutoa maji kutoka chanzo cha Mto Ntomoko na kuyafikisha katika Kijiji cha Igunga. Mradi huo kwa sasa upo katika hatua ya manunuzi ya kupata mkandarasi na ujenzi wake unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2025. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Wilaya ya Chemba ina miradi kama 17 ya maji lakini 80% imesimama kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili miradi ile iendelee kukamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mwaka 2022 Bunge lako Tukufu lilipitisha bajeti, Wilaya ya Nchemba visima 11 lakini mpaka leo vimechimbwa vitatu tu. Je, ni lini Serikali itakwenda kukamilisha miradi hiyo ya visima vinane vilivyobaki? Aahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Monni kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya kule Chemba. Ni kweli kabisa kuna miradi ambayo inaendelea pale Kubunko, Kelema Balai, Machiga na Mkalabati. Hayo yote ni maeneo ambayo wakandarasi wanahitaji fedha. Kama ambavyo nilisema hapa jana, Serikali kupitia Wizara ya Fedha tayari wameshatupatia *exchequer* ya shilingi bilioni 140. Pia, kwa miradi yetu ya *P4R* tuna shilingi bilioni 150 ambapo Katibu Mkuu alishaanza kukusanya hati za madai ili ziweze kuwasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo ya wakandarasi ili waendelee na kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu visima, pamoja na visima hivyo, kuna miradi zaidi ya mitatu ambayo iko katika hatua ya manunuzi lakini katika visima vile 900 mpaka sasa tuna visima 561 kati ya visima 900 ambavyo vinaendelea kuchimbwa nchini ambavyo ni sawa na 62%. Kwa upande wa Chemba kulikuwa na vile visima vitano, tayari vitatu vimeshachimbwa. Vilevile, kuna visima vya 2021 kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, tukishakamilisha hivi 900 baadaye tunaenda kukamilisha na vile ambavyo tulikuwa tumemwahidi Mheshimiwa Mbunge. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Awack.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, ni lini Serikali itatoa shilingi milioni 145 katika mradi wa Bwawani – Magafi? Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi kwa changamoto inayopatikana katika Mji wa Karatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, na kwa bahati nzuri nilifika katika jimbo la Mheshimiwa na Serikali ilitoa ahadi. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, kwamba tayari Serikali imeshatoa fedha nasi tunaweka utaratibu mzuri ili kuhakikisha kuwa fedha zinapotakiwa kwenda kwa ajili ya kukamilisha miradi, basi zifikishwe ili miradi hiyo iweze kukamilika na kutoa huduma za maji safi na salama ambapo ni pamoja na jimbo la Mheshimiwa ambalo ameuliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Monduli ina changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji hususan kwenye Vijiji vya Nanja, Mti mrefu na Lepurko. Vijiji hivi hawajawahi kupata maji kabisa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea wananchi hawa huduma hii muhimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa na kwa upande wa Monduli changamoto kubwa iliyopo pale ni ile *water table*. *Solution* ambayo tunakuja nayo ni ya kuchimba mabwawa. Tulikuwa na wakandarasi ambao tuliwapatia kazi ya kuchimba mabwawa, lakini wakasuasua na hivyo tukawaondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna mabwawa ambayo tunaendelea kuyakarabati na kuyafanyia kazi kwa kutumia *Force Account*. Kwa hiyo, tunaamini hata vijiji hivyo tutavifanyia tathmini na kuangalia ni namna gani tutavifikishia huduma ya maji safi na salama. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chomete, Mheshimiwa Kasaka na Mheshimiwa Kilave mjiandae.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya swali. Je, ni lini Serikali itawalipa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji katika Mkoa wa Mara na hasa Mradi wa Miji 28 unaotekelezwa katika Mkoa wa Mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miradi ya miji 28 ambayo inaendelea nchini hatujawahi kupata changamoto ya kifedha. Mkandarasi anapokamilisha na kuleta hati za madai wamekuwa wakilipwa bila kuwa na changamoto. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama kuna changamoto katika Miradi ya Miji 28, basi tuonane ili tuweze kuchukua hatua ili kuhakikisha kwamba wakandarasi hao hawakwamishwi kwa sababu hatuna changamoto ya kifedha katika Miji 28, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kasaka, Mheshimiwa Kilave na Mheshimiwa Bonnah mjiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Chunya Mjini tuna shida kubwa sana ya maji, tayari

fedha zipo na mkandarasi alishasaini mkataba, lakini mradi huu mpaka sasa hivi haujaanza na upo katika Mradi wa Miji 28. Je, ni lini mradi huu utaanza na utekelezaji wake utafanyika mara moja? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utaanza baada ya taratibu za kimanunuzi kuwa zimekamilika. Namtoa hofu Mheshimiwa Mbunge, ninaelewa kabisa kwamba mradi huu ni wa kimkakati na ameupambania sana. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ikiahidi itatenda, na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Miji 28 haitakuwa na jambo lolote ambalo litakwamisha miradi hiyo kuweza kuanza mara moja. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave, wajiandae Mheshimiwa Bonnah na Mheshimiwa Kunti.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni nini chanzo cha kukosa maji katika Jimbo letu la Temeke, wakati maji yalikuwa yanatoka lakini sasa hivi kata 13 hazipati tena maji ya bombani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Temeke tulikuwa na changamoto ya kimiundombinu na miundombinu hiyo sasa tumeshaanza kuifanyia kazi na kuirekebisha ili kuhakikisha kwamba maji yanatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ni vyema tukajulishana kuwa idadi ya wakazi wa Temeke na uwezo wa uzalishaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam kwa ujumla wake, bado tuko kwenye asilimia kidogo ukilinganisha na idadi ya watu walioko kwenye mtandao wa maji. Kwa hiyo, tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba, ile miradi ya kutoka Bwawa la Kidunda ndiyo tunaendelea kuharakisha ili kuongeza uzalishaji ambapo itakuja kuongeza kwenye *reservoir* zetu za Dar es Salaam ili iweze

kusaidia hata Wilaya ya Temeke kupata maji ya uhakika katika muda wote, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bonnah, jiandae Mheshimiwa Kunti.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Segerea kumekuwa kuna matatizo ya maji hasa kwenye Kata ya Bonyokwa, Kinyerezi pamoja na Kisukulu na *DAWASA* hawana jibu la moja kwa moja, ni nini kinaendelea? Je, Serikali ina mpango gani na dharura hiyo ambayo inaendelea katika Jimbo la Segerea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji unapokuwa ni kidogo, maana yake inapelekea kwenye mgao. Mgao huo unapokuja, maji yanapoachiwa mara nyingine yanaachiwa kwa kasi ambapo mara nyingine yamekuwa yakiharibu miundombinu yetu. Tumebaini changamoto ambayo inatokea Kinyerezi, Tabata, Kisukulu na maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Mbunge ameongelea. Mimi nimekuwa nikifuatilia pia na ziara zake ambapo amekutana na changamoto kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie kwamba Wizara ya Maji tumejipanga kwenda kutatua changamoto hii katika Jimbo la Segerea na Dar es Salaam kwa ujumla wake. Kulingana na upungufu uliopo bado Serikali inaendelea kuongeza kasi kwenye ujenzi wa Mradi wa Bwawa la Kidunda ili tuweze kuongeza uzalishaji kuleta katika *reservoir* yetu ya Dar es Salaam ili waweze kupata maji yanayotosheleza, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Jimbo la Dodoma Mjini kumekuwa na changamoto kubwa sana ya maji. Pili, changamoto kubwa hii ya maji kwa Dodoma Mjini, Bahi pamoja na Chemba, tegemeo kubwa ni mradi wa Bwawa la Farkwa. Ni lini Mradi wa Bwawa la Farkwa unaenda kuanza ili kuondokana na changamoto kubwa hii

inayoikumba Jiji la Dodoma, Wilaya ya Bahi pamoja na Wilaya ya Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya Jiji la Dodoma ni lita milioni 149 na uzalishaji wetu ni lita milioni 79 ambao ni sawasawa na 52%. Wananchi wa Jiji la Dodoma waliopo katika mtandao ni 92% ya Wanadodoma wote. Kwa hiyo, unaweza ukakuta kwamba, kuna changamoto kubwa. Ni kweli kabisa hatua ambazo Serikali inazichukua kwanza ni Serikali kuongeza visima Nzuguni ambayo inaongeza 11.7%. Pia tuna *phase II* Nzuguni ambapo itaongeza katika uzalishaji wetu 15%. Pia, tuna Zuzu-Nala na yenyewe itaongeza katika uzalishaji wetu. Huo ni mpango wa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa tumechimba kisima pale Kisasa ambapo kitaweza kutoa lita 120,000 kwa saa, maana yake kwa maeneo ya Kisasa, Ilazo angalau tutapunguza ule ukali wa mgao wa maji. Vilevile, katika upande wa *solution* ya kati tuna hili Bwawa la Farkwa ambalo Mheshimiwa Mbunge ameongelea. Sasa hivi Serikali iko kwenye utaratibu wa kumpata mkandarasi ambaye atakuja kutekeleza mradi huu. Mradi wa kudumu ambao ni kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria ambapo tayari tuko kwenye *feasibility study* itakapokamilika maana yake ni kwamba tutaingia kwenye *detail design,* mradi utatafutiwa fedha na maji yatavutwa kutoka Ziwa Victoria, baadaye tutakuwa tumetatua changamoto ya maji katika Jiji la Dodoma, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tumeshakuelewa. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

Na. 32

**Muda Unaotumika Kupata Kitambulisho cha *NIDA***

**MHE. MOHAMED SAID ISSA** aliuliza: -

Je, Mwananchi aliyekamilisha maombi ya kitambulisho cha *NIDA* anaweza kupatiwa ndani ya muda gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwombaji akishakamilisha taratibu za awali, hatua zinazofuata ni hatua muhimu za kiofisi zinazohusisha uchakataji na uhakiki wa mwisho wa taarifa za mwombaji wa kitambulisho. Aidha, kutokana na Serikali kuboresha mfumo wa uzalishaji vitambulisho, kwa sasa mwombaji baada ya kukamilisha taratibu zote anapatiwa Namba ya Utambulisho wa Taifa ndani ya siku tatu mpaka saba na kupatiwa kitambulisho cha Taifa baada ya siku 14, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza. Je, ni sababu gani zilizofanya Watanzania wengi kuwa na namba za vitambulisho vya *NIDA* lakini hawana vitambulisho vyenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Mheshimiwa Rais anayo nia thabiti ya kuhakikisha watoto wetu wote ambao wana sifa za kwenda elimu ya juu wanapata nafasi hiyo kwa kuongeza bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kwa nini Ofisi ya *NIDA* haiweki masharti nafuu ambayo itamfanya mwanafunzi aweze kupata kitambulisho cha *NIDA*, yule ambaye amefikisha umri, lakini wazazi wake hawana viambatanisho kama vyeti vya kuzaliwa ama kitambulisho cha *NIDA*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mohamed kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni kweli kwa kipindi kirefu huko nyuma tulikuwa na changamoto ya upatikanaji wa vitambulisho, na hivyo wananchi wamekuwa na zile namba. Kuanzia mwezi Oktoba, 2023 tumeanza uzalishaji mkubwa na usambazaji mkubwa wa vitambulisho vya Taifa. Kwa hiyo, changamoto hiyo kwa sasa hivi haipo baada ya Serikali kutoa takribani shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, *NIDA* husajili kwanza raia, wageni wakaazi pamoja na wakimbizi. Hivyo mwanafunzi yeyote atasajiliwa baada ya uhakiki wa wazazi wake, kujua yupo kati ya kundi lipi? Hii ni ili kulinda raia au wageni wakaazi au ni wakimbizi, kwa sababu suala la kitambulisho ni suala la usalama wa nchi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Nyamoga.

Na. 33

**Mitambo ya Kuchakata Sukari Inayotengenezwa na *TEMDO* – Kilolo**

**MHE. JUSTINE L. NYAMOGA** aliuliza: -

Je, lini Mitambo ya Kuchakata Sukari inayotengenezwa na *TEMDO* itafungwa katika Kata ya Mahenge – Kilolo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mtambo wa kuchakata sukari unatarajiwa kukamilika utengenezaji na kufanyiwa majaribio ya

awali ifikapo mwezi Aprili, 2025. Hivyo, mtambo huo utakuwa tayari kuzalishwa kibiashara katika msimu ujao (2025/2026) na tunatarajia kuanza kutengeneza au kukamilisha mpango huo mwezi Mei, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hatujapokea maombi rasmi kutoka Wilaya ya Kilolo. Pale watakapoleta maombi hayo, Serikali kupitia Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania *(TEMDO)* itafunga mtambo huo katika Kata ya Mahenge, Wilayani Kilolo, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali ya nyongeza mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika swali la kwanza, je, Serikali iko tayari kufanya majaribio hayo katika eneo hilo ambalo ni Kata ya Mahenge ili tuweze kuanza kupanda miwa kwa ajili ya majaribio hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Wakulima wa Miwa cha Kata ya Mahenge na Nyanzwa wako tayari kutoa ushirikiano kuanza maandalizi ya michoro ili tuweze kuendelea na maandalizi tukiamini kwamba mitambo hiyo itawekwa katika eneo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wa jambo hili kwa sababu alianza wakati tunawasilisha bajeti yetu ya mwaka kuhusiana na kuomba mtambo huu wa kuchakata miwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalichukulia kwa uzito kabisa na iko tayari pale mtakapowasilisha maombi rasmi tuje kufanya majaribio katika Wilaya ya Mahenge ili wananchi ambao kama wako tayari na wamelima miwa, basi tufanye majaribio hapo, na ninaamini

mtambo huo ukifanyiwa majaribio hapo maana yake utafungwa hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, maandalizi tunayofanya tutatuma wataalamu wetu kama ambavyo tumeainisha kwenye maeneo mbalimbali. Pale wanapohitaji watakuja kufanya utafiti na kuona sehemu gani pazuri pa kuweka mtambo huu kwa maana ya kiwanda kwa kushirikiana na wakulima. Kwa hiyo, tuko tayari kuja kwa niaba ya Serikali, wataalamu wetu watakuja kufanya ushirikiano huo, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Sichalwe.

Na. 34

**Mkakati wa Kuifanya DRC Iwe na Bandari Zaidi ya Kaleme (Kalemie)**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza: -

Je, nini mkakati wa Serikali kufanya *DRC* kuwa na Bandari nyingine zaidi ya iliyopo ya Kalemie?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya watu wa Congo *(DRC)* zimeingia makubaliano maalum *(MoU)* ya kuboresha Bandari ya Kalemie, Moba, Ujenzi wa Bandari kavu ya Kasambondo na uboreshaji wa miundombinu ya reli iliyopo nchini *DRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia makubaliano hayo yaliyofanyika, Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)* imesaini mkataba tarehe 31/5/2024 na Mshauri elekezi kufanya upembuzi yakinifu wa Bandari ya Kalemie na Moba na tayari ameshakabidhiwa eneo la kazi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali kwa hatua hiyo nzuri ambayo wamefikia. Pamoja na pongezi zangu, nashauri tu kwamba Bandari ya Momba upande wa *DRC*, ile siyo bandari ni mwalo. Kwa hiyo, siyo kuboresha bandari, labda kama kutakuwa na kujenga bandari mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa Bandari ya Kalema kwa upande wa Tanzania imejengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 49, kutoka kukamilika kwake, ni ipi tija ambayo tumeipata Serikali mpaka sasa kwa kujengwa bandari hiyo kubwa na uwekezaji mkubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa *Memorandum of Understanding* hii ambayo Serikali imesaini tarehe 31 Mei, ilikuwa ni kwa ajili ya maboresho ya *railway* kutoka Moba kwenda Lubumbashi na wafanyabiashara wengi ambao wanafanya biashara kwenda *DRC* Lubumbashi wanatumia magari kupitia nchi ya Zambia, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha wanaboresha barabara kushirikiana na Serikali ya *DRC* kuboresha barabara kutoka upande wa Kalemie - Moba mpaka Lubumbashi ili kutokuharibu biashara ya wafanyabiashara wa magari kipindi hicho bandari imekamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Condester Sichalwe Mbunge wa Momba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Kalema baada ya kukamilika haijaanza kazi 100% kwa sababu ya hiyo miundombinu ya upande wa pili, lakini tayari kuna mizigo ya meli ndogo imeendelea kufanya kazi pale. Pia, imekuwa na msaada mkubwa pale ambapo Bandari ya Kasanga kutokana na mabadiliko ya tabianchi imekuwa na maji kujaa. Kwa hiyo, hii bandari imekuwa

ni msaada mkubwa sana kutumika na tunavyoongea sasa hivi tayari wako wenzetu ambao wameomba waikodishe ile bandari, kwa ajili ya kuitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, 100% ya tija ya bandari hii itapatikana wakati meli zetu ambazo tunazifuata na zile ambazo tunajenga zitakapokuwa zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upande wa barabara ya upande wa nchi ya pili, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndiyo maana tumeweka mshauri elekezi ambaye ataeleza Moba ijengweje, Kalemie ikarabatiweje ili iweze kwenda sambamba na bandari zetu za Tanzania. Hii ni pamoja na kuangalia kama kuna umuhimu wa kujenga barabara upande ule, Serikali haitasita kufanya hivyo, ikiwepo reli na bandari kavu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini meli za *MV-Mwongozo* na Liemba zitaanza kutoa huduma ya usafirishaji katika bandari zilizoko katika Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Bandari ya *MV - Mwongozo*, Liemba pamoja na Sangara ambayo inatumika sana kubeba mafuta, tayari ziko kwenye ukarabati. Kwa hiyo, tunategemea zikishakarabatiwa zitaanza kufanya kazi. Nataka nimhakikishie kwamba, tayari wakandarasi walishaanza kazi ya kufanya ukarabati, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

Na. 35

**Ujenzi wa Barabara ya Turiani – Mziha – Handeni**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, lini kipande cha Barabara ya Turiani – Mziha hadi Handeni kitajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Turiani – Mziha hadi Handeni ni sehemu ya barabara ya Magole - Turiani – Mziha – Handeni yenye urefu wa kilometa 148.6. Ujenzi wa barabara hii unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikani wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa jumla ya kilometa 52.27 zimekamilika kuanzia Magole – Turiani. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Handeni – Kang'ata ambayo itakuwa na urefu wa kilometa 30, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daktari Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Je, ni lini Barabara ya Bigwa - Kisaki ambayo tumekuwa na matumaini ya muda mrefu ya kujengwa kwa kiwango cha lami itaanza kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Hili swali nimeliuliza mara nyingi humu Bungeni. Je, ni lini kipande cha Mikumi – Kilosa kitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, kusudi barabara yote iweze kuwa na lami? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Bigwa - Kisaki tulishasaini mkataba na kwa kweli sasa hivi tumeshapeleka maombi kwa ajili ya kupata malipo ya awali ili mkandarasi aweze kuanza kazi. Mara atakapokuwa amelipwa *advance payment* mkandarasi huyu ataanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara ya Mikumi - Kilosa, kwanza nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Waziri ameshasema kwamba hii barabara kwanza inapandishwa hadhi kutoka barabara ya mkoa kwenda kuwa barabara kuu na tayari tumeshaanza kuijenga kwa awamu. Kwa hiyo, tutaendelea kuijenga kwa awamu wakati Serikali inatafuta fedha ya kukamilisha kipande chote kwa lami kati ya Kilosa na Mikumi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda sana.

Tunaendelae na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, swali namba 36 limetolewa kutokana na maombi ya Mheshimiwa Mbunge mwenyewe. Tunaenda Wizara ya Afya, Mheshimiwa Profesa Aloyce Ndakidemi.

Na. 37

**Kuimarisha Tiba za Kitalii Nchini**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, Serikali imechukua hatua gani za kuimarisha Tiba za Kitalii kutokana na kuimarika kwa huduma za Afya katika Hospitali za Rufaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Afya kwa kununua vifaatiba vya kisasa, kuimarisha miundombinu ya matibabu, kusomesha wataalamu ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeteua hospitali saba kwa ajili ya utekelezaji wa huduma za Utalii wa Tiba, tano zikiwa za Serikali na mbili za binafsi ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Moi, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Hospitali ya Benjamin Mkapa, Hospitali ya SAIFEE na Hospitali ya Aga Khan.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri, kwani huu mradi utaliingizia Taifa letu fedha nyingi za kigeni. Pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro ni lango kuu la kuingiza watalii hapa nchini na katika Kanda ya Kaskazini. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutumia fursa hii kujenga Hospitali ya Tiba za Kitalii karibu na uwanja huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hospitali ulizozitaja sita kati ya saba ziko Dar es Salaam na moja iko Dodoma. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuiongeza Hospitali ya *KCMC* katika mradi huu, kwani wako vizuri sana kwenye kutibu tezi dume na viungo bandia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anafanya masuala mazuri kwenye jimbo lake, lakini anazungumzia mambo mazuri kwa ajili ya Mkoa wa Kilimanjaro. Mheshimiwa amesema swali lake la kwanza, kuhusu kujenga Hospitali ya Utalii kwa maana ya Kilimanjaro *International Airport* ni lango la watalii kuingilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa, kwanza uhitaji utakapokuwepo, itakuja, lakini hospitali yetu ya *KCMC* sasa hivi inaimarishwa na Serikali, na siyo tu Hospitali ya *KCMC,* na hospitali nyingine za kanda ili kuongeza idadi ya hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana utaona Serikali inapeleka shilingi bilioni 1.2 kila wakati kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni saba sasa hivi kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha huduma za kansa katika hospitali hiyo ya *KCMC* na huduma nyingine ili ifike mahali hakuna sababu ya kutoka Kilimanjaro na Kanda ya Kaskazini kuja Dar es Salaam. Sasa wenzetu wa nchi zilizopakana na Mkoa wa Kilimanjaro, Arusha na kwingine wanaweza wakaja huku kwenye hospitali yetu ya *KCMC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amesema hospitali zote zipo Dar es Salaam, ni kweli kwa maana ya kwamba tuna zile hospitali zetu za Taifa na ya kanda ni moja ambayo ni Benjamini Mkapa tunayotaka iwe sasa na yenyewe Hospitali ya Kitaifa. Pia Mtwara kwa sababu iko kule mpakani na wenzetu tunataka waboreshewe na ifike mahali sasa kuwe na uwezo wa kutoa tiba ya kitalii kwa maana ya Hospitali ya Kanda ya Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kigoma itajengwa Hospitali ya Kanda kubwa sana Kigoma na lengo siyo tu kutibu Wanakigoma na Wanakanda wa kanda hiyo, lakini pia kuleta Watalii kwa maana tiba na utalii kwa nchi ambazo zimezunguka kwenye eneo lile la Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, hayo yanaendelea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliokaa Jukwaa la Spika, tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambao ni Viongozi wa Shirikisho la Vyama vya Madereva Pikipiki, Bodaboda na Bajaji kutoka Mkoa wa Dar es Salaam wakiambatana na wenzao kutoka mikoa mbalimbali nchini wakiongozwa na Mwenyekiti, Ndugu Said Chenja, karibuni sana Bungeni watoto wa mama, kazi nzuri mnafanya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao ni wanafunzi 20 na walimu 18 wa Shule ya Msingi Majengo kutoka Mkoa wa Tabora, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni marafiki zake kutoka Jimbo la Arkansans nchini Marekani, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Ravia Faina ambao ni viongozi wa Matawi ya CCM Jimbo la Makunduchi Kusini Zanzibar. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mariam Kisangi ambaye ni Mwenyekiti wa Kikundi cha Futa Machozi kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga ambaye ni mdogo wake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, karibu. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Assa Makanika, yeye ni Mwenyekiti wa Kata ya Mwandiga, Jimbo la Kigoma Kaskazini. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanachuo na walimu 55 wa Chuo cha Biblia kutoka Mkoani Morogoro, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 70 wa darasa la sita na walimu wanne kutoka Shule ya Msingi Ilolo iliyoko Wilaya ya Chamwino Mkoa wa Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 99 na Walimu 11 wa Chama cha Skauti Tanzania kutoka Shule ya Msingi *Peace and Love* iliyoko Wilaya ya Ubungo Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Ofisi ya Bunge, Katibu wa Bunge anawatangazia kuwa Madaktari kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Taasisi ya Magonjwa ya Moyo *JKCI* wapo katika Kituo chetu cha Afya hapa Bungeni tangu

tarehe 29 Oktoba mpaka tarehe 8 Novemba, 2024 kwa ajili ya kutoa huduma za afya. Madaktari hao ni wafuatao; Daktari Jimmy Ernest, Daktari Bingwa wa Tiba ya Pua, Koo na Sikio, Daktari Lona Kasanyanyu, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ngozi, Daktari Emil Richard, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mifupa na Daktari Kawanyika Mwinyipembe, Daktari Bingwa wa Moyo. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023; na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano. Tunaanza sasa na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, jiandae Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa na Mheshimiwa Joseph Tadayo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yako ya Kamati hizi tatu; *LAAC, PAC* na *PIC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana nijikite zaidi kwenye taarifa iliyoletwa hapa Bungeni ya *PIC*. Sekta ya Umma kwa maana ya Serikali na Dola kujiingiza kwenye biashara ilishamiri sana miaka ya 1961 mpaka 1967. Ni vizuri tukaiweka hii kwenye *context* ya historia kwa sababu historia inatufundisha, moja ya mambo ambayo tunajifunza katika historia ni kutojirudia makosa, kwa hiyo, ni vizuri siku zote tukakumbuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika mengi kuanzia miaka ya 1967 mpaka 1987 yalidhihirika wazi kwamba yana ufanisi ulio duni hasa wa kifedha na kiutendaji. Ni wazi kwamba Serikali ilikuwa ikiingia hasara kubwa. Sababu zipo nyingi na hatuna haja ya kurejea, lakini zipo chache za msingi ambazo zinaweza zikatusaidia kuona namna gani yale ambayo yamebainika sasa hivi kwenye ripoti yanatakiwa yashughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa kwamba mtaji ambao ulikuwa ni mdogo uliowekezwa, usimamizi na uendeshaji duni naongelea miaka ya nyuma, Bodi dhaifu ambazo zilipewa kazi ya usimamizi. Pia tumeambiwa kulikuwa na mgongano mkubwa wa maslahi, mpaka kusababisha sasa Serikali kufanya maamuzi makubwa ya kubadilisha na ku-*reform* Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kazi ya Bunge katika mchakato huo ilikuwa ni kubwa pamoja na kutunga sheria mbalimbali ikiwemo sheria iliyounda Tume ya Rais ya kubinafsisha Mashirika ya Umma na kuyabadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nasema wazi, mimi nilikuwa ni mmoja katika watu waliobahatika kufanya kazi katika Tume ya Rais ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma kwa kipindi cha miaka nane. Sipo hapa kuitetea Tume hiyo, lakini nipo hapa kueleza *facts* chache ambazo zinaweza zikatusaidia kuelewa tulikotoka na tunakotakiwa kwenda na kwa nini tupo hapa tulipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Makampuni ya Mwaka 1992 ndiyo hasa iliyoanzisha mchakato huo na Tume ya Rais, iliyopewa *mandate* ya kufanya kazi miaka saba na ikaongezewa miaka mitatu na ikamaliza kazi yake mwaka 2007. Wakati

inamaliza kazi hiyo, Mashirika yaliyokuwa yamebakia katika miliki ya Serikali kwa maana ya kumilikiwa moja kwa moja au nasema *partial* yalikuwa hayazidi 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ripoti hii kwanza inakuonyesha sasa hivi tunaongelea zaidi ya mashirika 248. Nami najiuliza hivi, lini tumeunda mashirika yote hayo? Lakini hoja ya msingi siyo lini tumeunda na kwa nini tumeunda mengi? Kuna sababu za kitalaamu, kwa nini pengine tunayo? Hoja ya msingi ni kwamba tulifanya yaliyofanyika kwa sababu yalikuwa yanaingiza hasara, yalikuwa yanachukua ruzuku ya Serikali kwa mamilioni na matrilioni ya shilingi. Kwa hiyo, hatukuwa na *option* zaidi ya kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukisoma ripoti ya Kamati, unapata kuwa mwelekeo bado haujabadilika sana, bado tuna mashirika mengi sana ambayo yanatia hasara, hayajatambua kwamba Serikali imewekeza mtaji na inatakiwa ipate faida kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana, baadhi ya mashirika hayo, msingi mzima wa kuyarekebisha ilikuwa ni kuhakikisha angalau tuna mashirika ya aina mbili. Yapo yale yanayotoa huduma na ni muhimu kwa maslahi ya nchi kwamba hata pengine yasipopata faida kwa wakati bado huduma za jamii zinatakiwa ziwepo. Kwa hiyo, hayo utayaacha pengine yataendelea na utayavumilia, yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo Mashirika ya kibiashara ambayo yanatakiwa yashindane, yaende kwenye ushindani; yahakikishe yanarudisha mtaji, yalete faida na yatoe gawio. Katika mashirika 35 ya kibiashara bado mashirika 17 yanapokea ruzuku ya Serikali. Haya ndiyo mambo yaliyofanya kwa nini tufanye *reforms?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tubinafsishe baadhi ya mashirika hasa ya kibiashara ili yasichukue ruzuku ya Serikali kwa ajili ya kuendesha mambo ya biashara? Ni lazima tutambue kwamba kufanya biashara kuna miiko yake na kuna taratibu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, moja ya taratibu kubwa ni kurudisha mtaji na kuhakikisha yanafanya kazi kwa tija. Naiomba sana Serikali, nafahamu Ofisi ya Msimamizi Mkuu kwa mujibu wa Sheria za Tanzania kwenye upande wa mashirika ni Ofisi ya Msajili wa Hazina. Nafahamu kuna jitihada kubwa zinazoendelea, lakini ni lazima tutambue kwamba jambo hili tusilivumilie kwa muda mrefu. Tulifika tulipofika kwa sababu tulilivumilia kwa muda mrefu na labda tulikuwa na sababu za kihistoria na za kisiasa ya kulivumilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani mpaka leo hii Mashirika ya Umma, eti mishahara bado inatoka Hazina. Mashirika ya kibiashara! Tufike mahali tunasema kwamba hili haliwezekani na halikubaliki. Siyo matumizi mazuri ya fedha za umma, na ni vema tukatambua kwamba itatusaidia kama nchi ili miradi mingine mingi ambayo pengine badala ya kulipa mishahara kwenye mashirika ya kibiashara ya umma, fedha hizi zitakwenda kusaidia miradi mingine ya sekta za kijamii katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyobainika kwenye ripoti hii ni mengi, lakini mengine ukisoma kwa haraka unapata mshituko kidogo. Tunasema faida ndiyo kila kitu katika kuendesha mashirika ya kibiashara, haijalishi kama Serikali ni mmiliki au mtu binafsi ni mmiliki, faida na ufanisi ndiyo kila kitu. Sasa Serikali imeweka vigezo vingine kwamba hata pengine usipoweza kufikia mahali ukatoa faida, basi utoe asilimia 15 ya mapato ghafi angalau kama mchango.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado hata hiyo baadhi ya mashirika maana yake faida ni mpaka ukokotoe kila kitu useme nilifanya matumizi yalikuwa ni haya, mtaji wangu ulikuwa ni huu, nimeuza kiasi hiki, nimetoa huduma kiasi hiki, faida iliyopatikana ni hii. Sasa siku zote wahasibu wanajua ina *complications* zake, lakini kutoa gawio la mapato ghafi katika matumizi yako kwa mwaka, ni jambo ambalo shirika lolote la kibiashara linatakiwa lifanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta bado kuna mashirika hata hiyo wanashindwa, na uhalisia unaonyesha kwamba hata kwa wale waliotoa, mwenendo unaonyesha kwamba kumekuwa

na *decline* au kuteremka kwa hilo gawio au la mapato ya 15% ya mapato ghafi. Kwa mfano, mwaka 2021/2022 kulikuwa na punguzo la karibu asilimia 6.4, ungetegemea siku zote angalau haya mashirika yaendelee kutoa gawio la kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza zaidi, utegemezi wa mashirika haya ya umma bado unaendelea kukithiri. Kwa mfano, ripoti yetu inaonyesha wazi kwamba mwaka 2022 mpaka 2023 utegemezi uliongezeka kutoka shilingi bilioni 13.2 mpaka shilingi bilioni 17.4. Huo ni utegemezi kwamba shirika ni la kibiashara, lakini bado linaitegemea Serikali kwa mambo mengi, kwa mtaji kwa mishahara wa ruzuku, na kwa kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mashirika tuungane na Mheshimiwa Rais ambaye amesema wazi na ameonyesha wazi kwamba tusiyavumilie mashirika ambayo hayatoi mchango katika mfuko mkubwa wa Serikali. Nami nasema hili kwa uchungu, kwa sababu kama nilivyosema, nilikuwa ni mmoja wa watu ambao walishughulika sana na *reforms* za nchi hii katika kuhakikisha *Parastatal Sector Reform* ina-*perform.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limejitokeza, kuna makampuni yanatoa hasara, yaani kila mwaka, miaka mitatu mfululizo. Katika hali ya kawaida Kampuni ya kibiashara ikifanya hasara miaka mitatu mfululizo, labda kama kuna maelezo ya kitalamu ya kihasibu, kampuni hiyo ni mufilisi. Kwa hiyo, tuziangalie kampuni hizo kama mufilisi na zishughulikiwe kama Kampuni ambazo zinafilisika, zisiendelee ku-*drain resources* za nchi kwa kuendelea kufanya biashara ambazo hawawezi kuzifanya kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nafahamu na ninaelewa jitihada kubwa inayofanyika mpaka muda huu na Serikali kupitia Ofisi ya *TR* kwa kuweka mikataba ya aina mbalimbali tunasema mikataba ya usimamizi wa taasisi hizo ili ziweze ku-*perform*.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo ambayo yameelezewa vilevile katika uchambuzi wa Kamati, nashukuru Kamati kwa uchambuzi mzuri ni kwamba kuna Makampuni yana majengo, yana *non-productive assets* ambazo katika hali ya

kawaida Kampuni ya biashara ambayo ina *non-core assets* inatakiwa isiwe nazo. Sasa nami nitoe angalizo, ni rahisi sana kufikiria kwamba labda tuuze *non-core assets*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe angalizo na nitoe wazo kwa Serikali kwamba kuuza *non-core assets* za Kampuni siyo *solution* ya kuifanya kampuni iwe na mtaji, lakini ni kinyume chake kwamba *assets* hizo zinaweza zikatumika kufanya kitu kinaitwa *securitization* ili kuzisaidia kupata mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa kuona kwenye tathmini inaonyesha kwamba zina *assets* lakini hazina mtaji. Kampuni hizo zina mtaji kwa kutumia hizo *non-core assets*. Tuzitumie *non-core assets* kutengeneza mtaji ili kuweza kufanya biashara, na kama haziwezi, basi Serikali iangalie utaratibu mwingine wa kuzifunga au kuzifilisi au kuzitafutia wabia Kampuni hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi, bado kwenye faida ndiyo kila kitu kwenye biashara. Unaweza ukafanya *comparison* ya haraka kwa mashirika ambayo Serikali ina hisa chache na yale ambayo Serikali ina hisa zote. Kwa tathmini iliyo katika kitabu hiki na katika ripoti hii ya Kamati, ni wazi kwamba kuna ufanisi mkubwa kwenye Taasisi na mashirika ambayo Serikali ina hisa chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kujiuliza, ni kwa sababu gani? Sababu zinaeleweka. *Is what we call operational efficiency? Operational efficiency* inaanzia kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana katika nchi yetu ya kutambua kazi, umuhimu wa Bodi za Wakurugenzi na sisi Wabunge ni moja ya sehemu ya watu ambao tunatakiwa tulielewe. Maana yake mara nyingi tunadhani na tunaambiwa, na tunaombwa kwamba mzee fulani ame-*retire,* ebu, mtafutie nafasi ya Bodi. Bodi siyo sehemu ya kupeleka watu walio-*retire*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee, sisemi kwamba watu wote walio-*retire* hawafai. Ninachosema, Bodi ya Wakurugenzi ndiyo sehemu sahihi ya kuongoza kampuni na siyo lazima kila mtu aliye-*retire* lazima akawe Mkurugenzi wa Bodi. Kwenye nchi nyingine wengi walio-*retire* wanakuwa *disqualified* kuwa Wakurugenzi wa Bodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuliangalie jambo hili kwa makini. Ninafahamu utaratibu ambao Ofisi ya *TR* inajaribu kuuweka wa kutangaza hizi nafasi, lakini kutangaza na mchakato mzima wa kuchagua nani anafanya, mwisho wa siku nani anaamua? Kwa sababu unaweza ukatangaza, lakini ukaishia kuwa na watu ambao wame-*retire* na hawana uwezo wa kuwa Wakurugenzi wakawa Wakurugenzi wa kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliangalie hili jambo kwa umakini sana kwa sababu nchi inaongozwa na Rais. Rais akitetereka, nchi inatetereka. Kampuni inaongozwa na Bodi na Mwenyekiti wa Bodi. Bodi ikitetereka, kampuni inatetereka. Kwa hiyo, kwenye uchaguzi wetu tuwe makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi, ni muhimu sana ofisi inayosimamia, katika hali ya kawaida wanahisa ndio wanaotakiwa waifukuze bodi. Sasa madaraka haya yote ni madaraka ambayo Watanzania tumempa Rais wetu. Rais wetu hawezi kufanya kila kitu, na tumemsikia akisisitiza umuhimu wa kuhakikisha bodi zinafanya kazi zake na Wenyeviti wanafanya kazi zao. Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa sheria ame-*delegate* hiyo kazi aidha kwa Mawaziri, na ndio wanaomshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo. Mheshimiwa Idrissa.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ajiande Mheshimiwa Tadayo na Mheshimiwa Songe.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika hizi hoja tatu za Kamati zilizoletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuipongeza Serikali kwa kujitahidi kuendelea kupunguza dosari zinazotokea katika kila mwaka. Dosari ambazo tumeziona wakati tunajadili jambo kama hili katika mwaka uliopita kwa kiasi zimepungua, zimezaliwa dosari mpya. Pia baadhi ya mambo ambayo hayakuwepo katika taarifa zilizopita, safari hii hayapo tena. Naomba niipongeze Serikali katika masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* miongoni mwa Kamati ambazo zimewasilisha taarifa yake hapa. Yapo mambo tumeyaona katika halmashauri zetu wakati tukizikagua tukipitia Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kweli ni mambo ya kupongezwa. Pia yapo mambo ambayo ni ya uzembe na yanakwenda kinyume na yale maelekezo ama matakwa, ama hamu ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kuona Halmashauri za Serikali za Mitaa nazo zinaweka mchango mkubwa katika kuhakikisha Taifa letu na wananchi wanapata huduma zilizo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua katika hii Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ambayo tunaijadili ya mwaka 2022/2023, Serikali Kuu ilipeleka katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ruzuku ya shilingi trilioni 7.6. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia na Serikali Kuu walitimiza wajibu wao Barabara, wa kupeleka fedha katika Serikali za Mitaa, japokuwa na zile zilizotengwa katika Serikali za Mitaa zilizopangwa kukusanywa, zilikusanywa kwa zaidi ya 100%, shilingi bilioni 912. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na dhamira njema ya Rais na Serikali katika kufanikisha mambo, bado Serikali za Mitaa

zimeshindwa kuendelea kukusanya fedha ambazo zipo wazi kabisa kwamba zinaweza kukusanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali za Mitaa katika mwaka 2022/2023 mawakala wanaokusanya fedha za baadhi ya halmashauri, shilingi bilioni 5.6 zilikusanywa na mawakala, lakini hazikuwasilishwa katika halmashauri; Mkaguzi wa Hesabu za Serikali amebainisha kwamba mwaka uliopita lilionekana na mwaka huu linaonekana tena. Serikali za Mitaa kupitia mashine za *POS* jumla ya shilingi bilioni 6.1 ilikusanywa, fedha haijapelekwa katika halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa *LGRCS* shilingi bilioni 45 zimeshindwa kusuluhishwa. Kwa hiyo, Serikali inaelekea kupoteza shilingi bilioni 45. Nini ninachotaka nizungumze hapo? Bado kuna wajibu wa kuongezwa nguvu katika kusimamia fedha za Serikali katika halmashauri. Fedha hizi ambazo nimezisema hapa hazijaweza kukusanywa na kufikishwa katika Serikali japokuwa zilishakusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamekusanya shilingi bilioni 5.6, hawajapeleka Serikalini, wanajulikana, lakini hakuna kilichofanyika. Hii siyo sahihi. Watu wamekusanya shilingi bilioni 6.1 kupitia mashine za *POS,* fedha hazijapelekwa benki. Aliyepewa mashine anajulikana, fedha inajulikana iko wapi, lakini hakuna kilichofanyika. Hii siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 45 ambazo zilikuwa katika Mfumo wa *LGRCS,* Kamati tulielezwa na Serikali kwamba mfumo huu kufa kwake na kwenda katika Mfumo wa Tausi, madeni haya hayatakwenda. Hii siyo dhamira ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuona fedha zilizokusanywa zikatatue matatizo ya wananchi zipotee hivi hivi. Nini ushauri wangu maalumu katika hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha, wakati wanakwenda kuufuta kabisa Mfumo wa *LGRCS,* ni lazima wahakikishe fedha shilingi bilioni 45 siyo zinasuluhishwa tu, zipatikane, zirudi katika mfuko wa Serikali na

dhamira ya Mama Samia kuendelea kutoa huduma kwa wananchi ili iendelee kuwa nyepesi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado pia halmashauri hazikusanyi vizuri. Kuna shilingi bilioni 61 iliyotakiwa kukusanywa kutoka katika vyanzo muhimu na vya kawaida, mfano leseni, ukusanyaji wa ushuru katika masuala ya vileo, halmashauri hazijakusanya. Sasa, Wizara ya TAMISEMI ni lazima ihakikishe fedha hizi zinakusanywa. Pamoja na kwamba walifika zaidi ya 100% ya makusanyo yaliyopitishwa na Bunge hili katika bajeti iliyopita, lakini zaidi ya shilingi bilioni 60 hawakukusanya. Kwa hiyo, ni lazima fedha hizi zikusanywe ili dhamira yetu ya kuhakikisha Taifa hili linakwenda mbele itimie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kipengele cha mapato ya ndani kutokupelekwa katika shughuli za maendeleo. Halmashauri 80 tu, zile zilizofika mbele ya Kamati yako kati ya halmashauri 184 zilizokuwepo katika Taifa letu, shilingi bilioni 17.6 haijapeleka katika shughuli za maenedeleo. Halmashauri fedha wamekusanya, wamepanga mipango yao, wakachukua fedha zilizostahiki kwenda kujenga madarasa, hospitali, kuboresha huduma za wananchi ambao wametoa fedha hizo, lakini hawajapaleka shilingi bilioni 17.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, hapa baadhi ya hawa watu katika halmashauri hawamtendei haki Mheshimiwa Rais, hawaitendei haki CCM ambayo imeelekeza wananchi wakapewe huduma na fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulalamika peke yake hakutatosha. Naishauri Serikali ihakikishe kila Afisa Masuuli aliyeshindwa kusimamia fedha za shughuli za maendeleo, ambazo walishakusanya katika halmashauri zao, zikashindwa kwenda katika miradi ya maendeleo kwa ajili ya wananchi, Serikali itafute hatua muhimu za kuwashughulikia. Nimesema hii shilingi bilioni 17.6 ni halmashauri 80 tu, chini ya 50% ya halmashauri zote katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za 10%, katika huu mwaka wa fedha tunaoujadili ambao Ripoti ya CAG ililetwa kwetu, fedha

ambazo zilistahiki kukusanywa, watu walishakopeshwa, na halmashauri ilitakiwa izikusanye kutoka kwa vijana, akina mama na watu wenye ulemavu shilingi bilioni 79. Zimepungua kutoka zile ambazo hazikukusanywa katika mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha inatolewa anapewa mtu, na mtu anayepewa anapewa ndani ya halmashauri. Hivi ni kweli halmashauri walikuwa hawajui wanampatia nani? Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi aliyoyafanya ya kuzuia fedha zile zisiendelee kutolewa, lakini napongeza zaidi kwa maamuzi yaliyokwishaamuliwa ya fedha zile zianze kutolewa na mchakato unaendelea tangu mwezi wa Saba mwaka huu 2024. Kwa hiyo, shilingi bilioni 79 katika mwaka mmoja tu wa 2022/2023 nazo zipatikane ili zikaongeze msingi wa fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutaweza kukubali na haitakuwa sahihi kwa Rais wetu na kwa chama chetu ambacho kimetuweka madarakani sisi sote humu ndani, kuona fedha hizi ambazo zilishakusanywa, wakakopeshwa watu ili wakajiendeleze, zinapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ihakikishe inatengeneza mazingira fedha hizi zikusanywe ili zikatanue ule mfuko wa takribani shilingi bilioni 200 ambazo Mheshimiwa Mchengerwa ametutangazia kwamba Rais ameridhia zitaanza kutolewa kuanzia mwezi wa Saba na mchakato unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizi zenye kuendelea, shilingi bilioni 227.9 ambazo zinategemea kutolewa; kutoa mikopo tangu mwanzo tulikuwa tunatoa, lakini tija ya mikopo tuliyoitoa ambayo inatokana na fedha za 10% haikuwa nzuri sana. Fedha zimetolewa mabilionea hatujawaona, fedha zimetolewa, hazijarejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini ushauri wangu katika fedha hizi? Pamoja na hayo yote ambayo yameshaanza kufanyika katika Serikali za Mitaa; kufanyika mikutano ya mitaa, kuita watu ili wajulikane wale ambao watakopeshwa fedha. Siyo kila atakayepewa fedha ataweza kufanya biashara na kuziendeleza

fedha. Sasa watenge fungu maalumu la kuwafundisha watu kufanya biashara wale wenye uhitaji wa kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukazaa watoto mapacha, ukawapeleka skuli pamoja, wakafundishwa na mwalimu mmoja, wakamaliza elimu pamoja. Huyu ukampatia shilingi bilioni moja na huyu mwingine ukampa shilingi bilioni moja, yupo atakayeweza kuziendeleza, yupo atakayeweza kuzitafuna zikaisha. Sasa halmashauri zetu ziangalie, siyo tu kutoa fedha kwa sababu watu wameomba. Je, tunaowapatia fedha watakwenda kutengeneza matokeo tutakayoyategemea kwa maslahi ya Taifa? Je, tunapokwenda kuwapatia fedha tunatengeneza mabilionea wapya? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tadayo, jiandae Mheshimiwa Songe na Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Kamati hizi tatu muhimu, Kamati ambazo zipo katikati kabisa katika jukumu letu la Bunge la kuisimamia Serikali. Nawapongeza Kamati zote tatu kwa taarifa zao nzuri. Kimsingi mimi naziunga mkono taarifa zote tatu, lakini nitachangia kwenye taarifa moja tu ya *PIC* kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda hapo, namshukuru sana *CAG* kwa kazi yake nzuri ambayo amekuwa akiifanya kila wakati inayoziwezesha Kamati hizi kutupatia taarifa ambazo zinatufungua na kutuwezesha kuisaidia zaidi Serikali kwa namna hii ya kuisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi kampuni zetu za umma, zipo ambazo zimefanya vizuri, lakini zipo ambazo zimeendelea kupata hasara kila mwaka, yaani taarifa zake ni hasara. Kila mwaka lazima tunasikia hasara *TTCL, NARCO, NDC, ATCL* pamoja na nyingine. Sasa kampuni inapopata hasara, wenye kampuni ambao kwa sasa hivi ni sisi wananchi, kwa sababu haya mashirika ni ya umma, tunakuwa na mambo matatu. La kwanza, labda tukakope ili tuongeze mtaji; la pili, labda Serikali ikusanye kodi kwetu sisi, yaani kwa wananchi halafu iende iwapatie wao wafanye biashara; na la tatu, ni kuingia kwenye utaratibu kama wa *PPP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kurekebisha Mashirika ya Umma Serikali ya Awamu ya Tatu, yale ambayo yaliingia katika Mfumo wa *PPP* yalionesha mafanikio makubwa sana. Hatuna kelele zozote *Tanzania Breweries, Tanzania Cigarette Company, NMB* na mashirika mengine ambayo yaliingia katika utaratibu huu, yameendelea kufanya vizuri. Yale ambayo yaliuzwa moja kwa moja, mengine yalikufa, mengine yalibadili mwelekezo yakafanya kitu kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inaonekana kwamba utaratibu huu wa *PPP* kama umeandaliwa na ukasimamiwa vizuri ni utaratibu mzuri ambao unaendeleza mashirika vizuri na Serikali inandelea kupata kodi. Laiti *TTCL* ingeingia katika Mfumo wa *PPP,* pengine ingeweza ikashindana katika hii sekta ya mawasiliano ambayo ina ushindani mkubwa sana, lakini kwa sababu ilibaki yenyewe, imeendelea kuzama na kila mwaka tunahesabu hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mashirika yetu yanaitwa Mashirika ya Umma, lakini kwa hali ya uchumi wa sasa hivi ni lazima ya-*operate* kibiashara kama mashirika binafsi. Hata kama siyo *private,* basi angalau yakue, yaani yawe kama nusu *private*. Sasa, ili shirika liweze kwenda mbele, lazima liwe na vitu viwili vikubwa. Cha kwanza, pawe na bodi nzuri, na cha pili pawe na menejimenti nzuri. Haya Mashirika ya Umma ambayo sisi ni mali yetu, sisi ambao tunamtazama ambaye tumemkabidhi dhamana ni bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana bodi zetu nyingi ambazo zimekabidhiwa mashirika haya ya umma, sijasema zote, lakini nyingi ni zile ambazo kwenye *corporate world* wanasema ni bodi uyoga *(mushroom board)*. Zipo pale tu, lakini hazina umahiri na sekta ile wanayoisimamia. Matokeo yake wanaendeshwa zaidi na menejimenti hasa *CEO* au pengine na Wenyeviti. Kwa hiyo, wanakuwa hawawezi kutupatia matokeo yale ambayo tunayataka, kwa sababu hawana umahiri kwenye aina ya biashara ambayo hili shirika linafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko ya hapa na pale kwamba, wanaingiliwa labda na Serikali au nini, lakini mimi nadhani kuingiliwa ni sehemu tu ya kukosa umahiri. Kama bodi ni *competent,* itakataa kuingiliwa, itakuwa na misimamo na ikishindikana wanajiuzulu, kwani shida iko wapi? Wewe unakabidhiwa kazi unaharibu, halafu baadaye unatuambia sisi kwamba kuna mtu alikuingilia. Mbona wakati anakuingilia ulikuwa husemi na huchukui hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani kikubwa kabisa ni kupata viongozi kwenye haya mashirika kwa maana ya bodi ambao wamebobea kwenye zile sekta, na wapo tayari kufanya kazi. Siyo wako tayari kubembeleza ili waweze ku-*survive,* hapana. Hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, sheria ifuatwe, wapewe uhuru wa kufanya kazi zao kama vile ku-*recruit* wafanyakazi. Tuziruhusu bodi hata kama wanaamua kutafuta *CEO* kutoka nje, waacheni watafute. Sisi tunachotaka mwisho wa siku tuione faida imekaa mezani. Tuwape nafasi hiyo, lakini tusiwaingize kwenye mambo ambayo yanawakwamisha kwenye kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, msisitizo wangu kwa kweli ni kwamba, pale ambapo bodi inaona imeingiliwa kiasi cha kushindwa kufanya majukumu yao, ni bora wajiuzulu tu, kuliko kukaa hapo halafu tunapohesabu hasara watupatie habari za namna hii kwamba, kuna fulani alituingilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bodi zetu ni lazima zitambue kwamba, kazi yao wao ni ku-*govern,* siyo ku-*manage*. Ni

kutawala, siyo kuongoza. Bodi lazima itawale shirika ili mwisho wa siku ituletee faida na ituambie kwamba walifanya nini? Bodi isimamie mashirika yetu yaingie katika miradi ambayo kweli italeta faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, wataalamu wa *real estate* wanasema kwamba, mradi wa *real estate* unatakiwa ujilipe baada ya miaka 18. Kama ni zaidi ya hapo, ni kuachana na hiyo biashara kwa sababu kama miaka 18 haijalipa zaidi ya hapo ni kwamba utaanza kukarabati lile jengo lako ulilojenga na faida hutaiona. Kwa hiyo, lazima tuingie kwenye biashara ambazo kweli tunaona kabisa kwamba zitalipa na tusiwe watu wa visingizio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya miradi ukiangalia kule kujenga kwenyewe, miaka 18 inakaribia. Sina hakika kama jengo kama *Mzizima Tower* pale Dar es Salaam toka limenza kujengwa ni miaka mingapi? Ukija kujumlisha na muda kama tayari litaleta kweli *return,* mimi napata mashaka sana. Kwa hiyo, bodi lazima ziwe katika mazingira ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ili kweli tuweze ku-*realize* kupata faida kutoka kwenye mashirika yetu, tunahitaji hali kidogo kama ya mapinduzi katika sekta hii. Kama tutaendelea na *business as usual*, mimi sidhani kama tutaweza kupata faida katika mashirika yetu haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu kwa upande huo ni machache, kwenye Kamati hiyo moja tu ya *PIC*. Mengine wengine watachangia, lakini ninaunga mkono hoja ya Kamati zote tatu kwa sababu ripoti zao nimezisikiliza vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe, jiandae Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Haji Amour Haji atafuatia.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia taarifa hizi ambazo zipo mbele yetu. Nawapongeza sana Wajumbe wa

Kamati wakiongozwa na Wenyeviti wetu wa hizi Kamati zetu zote tatu kwa taarifa yao nzuri ambayo inatupatia taswira na nini kinachofanyika kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo nitajikita kwenye maeneo machache sana. Nataka nichangie katika maeneo matatu. Jambo la kwanza nitachangia eneo la ukaguzi wa ufanisi katika taasisi yetu ya Bodi ya Mikopo. Pia nitachangia habari ya *NHIF* ikihusishwa na hospitali ambazo zinatoa huduma ya kutibu wananchi. Pia, nitasema kidogo habari ya Kiwanda cha Dawa Keko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Ripoti ya *CAG* katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, utaona kuna mambo ambayo ameyaibua pale, yanahitajji kurekebishwa na mengine ni ya haraka ili kuweza kunusuru taasisi yetu kwa maana ya hii Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukaguzi wa miaka saba (2015/2016 – 2021/2022), ilibainika kuwa kuna fedha ambazo zilikatwa kwa wale wanafunzi waliokuwa wamekopeshwa na Bodi ya Mikopo, kwamba walikatwa zaidi ya kile kiwango ambacho walitakiwa kukatwa. Kitu hiki hakikubaliki na hakiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha kuona Bodi yetu haina mfumo wa kutambua kwamba mwanafunzi alishakatwa kiasi chake mpaka ameshamaliza, lakini anaendelea kukatwa. Makato haya yaliyokuwa na thamani ya shilingi bilioni 36, wanafunzi zaidi ya 59,000 walikatwa fedha hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wengine walikatwa fedha hizi wakati hata mikopo hawakupewa. Katika hao watu 59,000, kuna wengine walikatwa zaidi ya kile kiwango walichokuwa wamepewa. Tulipowahoji Bodi ya Mikopo walikiri kwamba, fedha hizi zipo, lakini bado hawajafanya *reconciliation* na wanufaika ili waweze kuwarejeshea fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashangaa kuona Bodi ya Mikopo kama haina mfumo madhubuti wa kuonesha kwamba, mwanafunzi huyu alikuwa anadaiwa kiasi fulani na ameshakatwa

na ameshamaliza. Inasababisha kuendelea kukatwa mpaka mkopo wake unaisha na anaendelea kukatwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu kazini huko wanaendelea kukatwa mikopo wakati hawajawahi kuchukua mikopo katika Bodi ya Elimu ya Juu, lakini kuna wengine ambao wameendelea kukatwa na wameshamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naishauri taasisi hii, hasa Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba, wanafunzi au wanufaika waliokatwa mikopo yao na wakati hawakukopa au wale wanafunzi waliokatwa zaidi ya kile walichokuwa wamekopa, kwa sababu hizi fedha zipo shilingi bilioni 36.8, waweze kurejeshewa fedha zao ili wanufaika hao sasa wasiendelee kuidai Serikali kwa sababu fedha hizi zipo. Warejeshewe fedha hizi kulingana na kile ambacho amekatwa zaidi ili wafanye kazi zao na kunufaisha kazi zao na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lililojitokeza katika Bodi hii ya Elimu ya Juu ni mikopo iliyotolewa zaidi ya shilingi trilioni 2.2 ambayo haijakusanywa mpaka sasa na mingi ya mikopo hii imeshaiva. Sehemu kubwa ya wanufaika hawajulikani waliko. Takribani wanufaika 256,000 wamekopeshwa mikopo na hawajarejesha na hata hawajulikani wako kwenye taasisi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wako kwenye taasisi za *private,* wanaendelea kupata mishahara, lakini kwa sababu, hakuna mfumo unaosomana na taasisi hizi, inasababisha kuzikosa fedha hizi na kutokuwa zimekusanywa mpaka sasa hivi. Zingeweza kukusanywa hizi shilingi trilioni 2.2 zingeweza kuwanufaisha wengine ambao wapo. Hasa kwa mfano ukiangalia bajeti yetu hii ya mwaka 2023/2024 ni takribani shilingi bilioni 570 ambazo tumepanga, kwa ajili ya mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana fedha hizi zingeweza kukusanywa zingeweza kuwasaidia wanufaika zaidi ya miaka miwili, ambao wanahitaji mikopo hii na hata ambao wanaendelea kukosa wangepata mikopo, kwa sababu tunapozungumza shilingi 2,200,000,000,000 ni fedha nyingi. Zikikusanywa zinaweza kusaidia wanufaika wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa waliokopeshwa hawajulikani wako kwenye taasisi gani, basi ni vizuri mifumo iweze kusomana ikiwemo na mifumo ya *NIDA*. Mtu anapopata ajira taarifa zake zijulikane, lakini pia kule Wizara ya Elimu taarifa za mnufaika huyu zijulikane, ili aweze kujulikana ni wapi amepata ajira na ni wapi anasomeka ili aweze kurejesha mikopo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kati ya hawa 256,000 ni wanufaika 88,449 ndiyo wamerejesha sehemu ya mkopo. Hawa 88,000 walikuwa wanadaiwa shilingi 1,033,000,000,000, lakini wamerejesha kiasi cha shilingi bilioni 405, ikisababisha shilingi bilioni 627 kutokuwa zimerejeshwa kwa hawa wanufaika 88,449. Hawa wanufaika 168,000 hawajarejesha kabisa kiasi cha shilingi 1,600,000,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima sasa Wizara yetu ya Elimu ione ni namna gani bora ya kuwafikia wanufaika ambao walishachukua mikopo, lakini bado hawajanza kurejesha na wengine wako kwenye kazi. Tayari wamepata ajira, lakini hawajaweza kuwafikia wala hawawatambui ili kuweza kuwatafuta na kuweza kupata mikopo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba kuwepo na mwongozo wa hali ya juu sana, ikibidi na sheria zitungwe ili kusudi mwajiri anapomwajiri mtumishi ahakikishe kwamba, taarifa zake ziko sahihi, lakini pia, anafanya *consultation* na Bodi ya Mikopo ili kujua kama mtumishi huyu anadaiwa na Bodi ya Mikopo. Aweze kujulikana na kuanza kukatwa kuweza kurejesha mikopo ya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua na ninatambua wapo vijana ambao bado hawajapata ajira, lakini ikijulikana pia siyo dhambi. Wajulikane wako wapi na wanafanya nini, ili watakapopata kazi basi takwimu ziwepo za kuwafanya wajulikane waliko na kuanza kurejesha mikopo yetu baada ya kuwa wameshapata ajira. Nilitaka niseme hilo kwenye eneo la Bodi ya Mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nataka nichangie eneo moja. Tulifanya mahojiano na Hospitali ya Benjamin Mkapa. *CAG*

ameeleza ya kuwa walipata hasara ya shilingi 3,266,000,000 baada ya kupeleka madai *NHIF* ya huduma waliyoitoa na *NHIF* kuyakataa madai hayo kuwa siyo halali na hayako sawa ikilinganishwa na huduma iliyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara hii ni ya mwaka mmoja wa 2022/2023, shilingi 3,266,000,000, hiki kitu hakikubaliki. Ni lazima sasa tuwe na mpango kuanzia taasisi hizi za hospitali. Kwa mfano, hii ni taasisi moja ya Benjamin Mkapa, hatujazungumzia Bugando, hatujazungumzia Muhimbili, hatujazungumzia maeneo mengine ya taasisi zetu. Hatujazungumzia hata *Shirati Hospital*, hatujazungumzia *Busega Hospital*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima sasa *NHIF* pamoja na watoa huduma hawa wakae pamoja ili waelewane, kwa sababu, makato haya, kwa mfano ya Benjamin Mkapa, shilingi 3,266,000,000 haimaanishi kwamba huyu mgonjwa hajapata matibabu. *Client* yeye ameshapata matibabu, ameshaondoka, yuko nyumbani anapumzika. Vyovyote vile ilivyo, lakini huku sasa kwa upande wa pili, madai yamepelekwa huko *NHIF* yamekuwa yana makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta mengine hayana *signature*, utakuta mengine alitakiwa atibiwe na Daktari Bingwa ametibiwa na *Clinical Officer.* Utakuta mengine labda dawa hii haikutakiwa kuandikwa hivi, ilitakiwa *code* ionekane hivi, lakini mwisho wa siku haya makato yanakatwa kwenye hospitali zetu na kuzisababishia kupata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi 3,266,000,000 kwa Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa mwaka mmoja ingeweza kusaidia kununua vifaatiba vingi, ingeweza kusaidia hata kunufaisha madai mbalimbali ya watumishi. Kwa hiyo, naomba sana *NHIF* kwenye eneo hili, pamoja na makosa haya, wakae na hawa watoa huduma kwa maana ya hospitali, ili waongee lugha moja na wawasaidie ili mwisho wa siku makosa haya yaweze kupungua na hospitali zetu ziweze kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, kuna makosa ambayo yanaweza kurekebishwa. Kwa mfano, fomu imepelekwa

*NHIF* na ikaonekana ina kosa ambalo linaweza kurekebishwa, basi hospitali zetu zipelekewe ili ziweze kurekebisha makosa haya na fedha hizi ziweze kulipwa kwa taasisi zetu. Kwa sababu, taasisi zetu sasa zinakosa fedha na zinashindwa kujiendesha kwa sababu *NHIF* imewakata makato haya na kushindwa kuyapeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya yote waendelee kutoa elimu kwa Watumishi wa Idara ya Afya ambao wanajaza fomu hizi, ambao wanatumia mfumo wa *NHIF*. Waweze kujua ni kwa namna gani mabadiliko yanakuwepo kwenye mifumo ili waweze kufanya kwa ufanisi zaidi kuweza kuzisaidia taasisi zetu na kupunguza makosa haya ili fedha ambazo zimekuwa *billed* kwenye *NHIF* ziweze kulipwa kama ilivyokusudiwa na kutokuwa na hasara zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ni Kiwanda cha Dawa Keko. Kiwanda cha Dawa Keko kina ubia wa Serikali pamoja na mtu binafsi. Kwa kipindi kile, huyu mtu binafsi alikuwa anamiliki 30% na Serikali 70%, lakini umefika muda sasa wamekubaliana kwamba, umiliki wote uwe wa Serikali, lakini kwa sababu, bado hawajifikia muafaka, na bado hawajasainishana mikataba na *documents* mbalimbali, kiwanda hiki kimeendelea kupata hasara kwa miaka miwili mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mwaka wa fedha 2021/2022, kiwanda hiki kilipata hasara ya shilingi 2,200,000,000, lakini mwaka wa fedha 2022/2023 kilipata hasara ya shilingi bilioni 12,100,000,000. Hasara imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Ni imani yangu, pia inawezekana 2023/2024 itazidi hii shilingi 12,100,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini? Kwa sababu kiwanda hiki bado hakitoi ufanisi uliokusudiwa kupatikana ukilinganishwa na mahitaji ambayo tumeendelea kuwanayo. Amezungumza hapa Mheshimiwa Mwanyika kuwa tuna taasisi ambazo zinaendelea kupata hasara. Mfano ni huu wa taasisi yetu ya *Keko Pharmaceutical*, ambayo inamilikiwa na Serikali, iliyopata hasara ya shilingi bilioni 5.2 kwa mwaka wa fedha 2022 na shilingi bilioni 12.1 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi, huyu mwenza alivyoona huko nyuma kwamba kuna hasara inaendeleaendelea, akaamua kuomba nafasi Hazina ili awe mshauri wa kiwanda hiki na sasa kazi yake anayoifanya ni ya ushauri. Yeye sasa analipwa mshahara wa shilingi milioni 15 kila mwezi, kitu ambacho tulivyouliza sisi kama Kamati kwamba, ni nini tija ya ushauri wake alioutoa kwenye maendeleo? Ikaonekana kwamba, hamna tija yoyote kwa sababu, kiwanda hiki kinaendelea kupata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalie kwa macho mawili kiwanda hiki. Naiomba sana Serikali itupie macho hapa. Kama kiwanda hiki sasa kimeshindwa kujiendesha na kupata faida, basi kiwe Kampuni Tanzu ya *MSD*, ili *MSD* iweze kukiendesha kwa namna ya kuwa kampuni tanzu ili sasa kuwe na *connection* kati ya *MSD* pamoja na kiwanda hiki ili kiweze kuleta tija kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kwa miaka miwili kiwanda hiki kuendelea kupata hasara ya shilingi bilioni 5.2, mwaka ule tena hasara ya shilingi 12.1, inawezekana pia, mwaka huu wa fedha ambao umeisha 2024 wakapata hasara. Hii haikubaliki, na pale kuna Mkurugenzi, kuna watumishi wanafanya kazi, wanaendelea kututia hasara. Hii haikubaliki. Ni bora kiwanda hiki sasa kiwe Kampuni Tanzu ya *MSD* ili kiwe na tija kwa Watanzania na tija kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja mapendekezo yote ya Kamati zetu tatu, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, jiandae Mheshimiwa Haji Amour na Mheshimiwa Juma Makoa, jiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nachukua fursa hii pia, nijiunge na wenzangu kumpongeza Spika wetu, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa umahiri wake aliouonyesha wakati akiendesha Mkutano wa *IPU*.

Naona ameiweka nchi yetu mahali pazuri, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwa kuwapongeza Wanakamati, Wajumbe wa Kamati zetu tatu ambao wamepitia taarifa ya *CAG* na kuichambua vizuri. Ninaamini kwamba, tumefaidi sana sisi ambao hatukuwa ni wa kuchambua moja kwa moja taarifa hizi; tumezisoma, lakini hatukuwa na muda wa sisi kupitia. Tuko kwenye Kamati nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunamshukuru *CAG* kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya. Ninaona anaendelea kutuletea ripoti ambazo zina mashiko, zinatuwezesha kuisimamia Serikali na kuishauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba, ni kwa mara ya kwanza tumepokea Ripoti za *CAG* na alisema kwamba, ametoa hati, lakini hakukuwa na hati mbaya. Kulikuwa na hati ambazo zina mashaka kidogo ambazo nazo zimepungua sana; sijui ni nne! Ni kama nne hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi hiyo kwa sababu, usimamizi wa Serikali umesababisha Serikali kuwa adilifu na kutekeleza kazi yake kwa kuzingatia kanuni na hivyo, hati zikawa ziko safi na uongozi unaanza juu.kwa hiyo, Mheshimiwa Rais ndiye ameweza kuwaonesha wenzetu kwenye Wizara mbalimbali na wakaweza kutenda kazi zao sawa sawa. Ninaamini kwamba, mwakani hata hizo ambazo zina mashaka zitakuwa zimeondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea Ripoti ya Kamati ya *LAAC,* ni nzuri sana, lakini utakuta kwamba, *sample* waliyoweza kuchambua ni halmashauri 55 tu kati ya halmashauri 181. Ni 29.9% ya Halmashauri, ni ndogo sana. Kwa hiyo, unaweza ukaona hili jambo siyo *alarming,* lakini pengine ni kwa sababu, zimeachwa nyingine nyingi na angalau wangefikia 50% hivi, ingekuwa inafurahisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inasababisha kuona umuhimu wa kumwomba Spika, kama itampendeza, wakati tunapokuja

mwakani aweze kuwapa Kamati hii muda zaidi. Hata kama ni wiki nne, inaweza kupendeza wakaongeza hiyo idadi ya halmashauri zitakazochambuliwa angalau kufikia 50%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naishauri Kamati kwamba, endapo wanaona muda wanaopewa ni mfupi, basi wawe wanatumia muda wao kabla ya *session* hii, waanze kuchambua hizo ripoti kwa sababu, tunazipata mapema kuanzia mwezi Juni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ripoti tumeona Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wamelalamika sana kwamba, wanashindwa kesi zile ambazo ni za *arbitration*. Kesi za *arbitration* kwenye mikataba mingi ile mizuri ina-*provide* kwa kusuluhisha matatizo yanayojitokeza kwenye kutekeleza mradi au mkataba kwa njia ya *arbitration*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi siyo mwanasheria, lakini ninajuajua kidogo na nimeendesha shirika ambalo tumeingia kwenye *arbitration* nyingi. *Arbitration* ni fani tofauti sana na kuwa tu mwanasheria. Unaweza ukawa mwanasheria mzuri sana, lakini ukienda kwenye *arbitration* kuna mbinu zinatumika, kuna kanuni ambazo ni tofauti kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mtu yeyote ambaye ni *arbitrator* anasoma masomo na kuna *certification* ambazo zinatolewa na vyuo mbalimbali. *UK* wana ya kwao, ni kama hizi tu za *CPA* na nini, lakini wanatoa; India wanatoa, *China* wanatoa, hata *UK* na *USA* wanatoa. Kwa hiyo, wana-*certify* kwamba, huyu mtu ni *certified arbitrator*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninajua hilo kwa sababu, ni *conflict* kidogo ya *interest*. Mtoto wangu ana *certification* hizo na pia ni *arbitrator* kwenye mataifa mbalimbali. Kwa hiyo, siyo kitu tu cha kusema tunapeleka mtu ilimradi ni Wakili wa Serikali, anaenda ku-*arbitrate*, hasa hizi za kimataifa, na ni gharama sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mwanasheria Mkuu na Wakili huyu wakae pamoja, wajaribu kuunda kitengo mahususi kwa masuala ya *arbitration*. Unakuta tunapigwa dola nyingi bila

sababu. Mtu amekosea tu kidogo, amekosea *tactics* tu, wanatumia *tactics* za *arbitration,* unakuta tumeshindwa. Kwa hiyo, naomba waunde kitengo mahususi, waweze kukiwezesha, kukipa uwezo kwa kuwapa mafunzo, kuwapa *certification* hizo wafanye, wawe *certified* kwamba, ni *arbitrators*, halafu sasa wajue wanaenda kutuwakilisha kwenye masuluhisho hayo ambayo yanahusiana na mikataba ya Serikali. Naomba sana hilo lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mfupi huu ambapo inachukua muda kidogo kupata hizo *certification* na kuwa *certified* uwe mzuri, lazima watu wawe wazuri sana kwenye sheria pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kwamba, kwa kipindi cha mpito basi Serikali iangalie uwezekano wa kutumia mashirika binafsi au kampuni binafsi za sheria na hata hizi za *accounting* na wenyewe wana vitengo vya kisheria ambao wanaweza wakatuwakilisha, ili tuweze kuendelea. Japokuwa natambua kwamba, zile kesi nyingi, mashauri mengi ya usuluhishi yanapungua na presha imepungua pia, kwa hiyo, ninaamini kwamba, hatuendelei, lakini tujenge uwezo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la mikopo, niseme tu sentensi moja kwenye suala zima la mikopo hii ya 10%. Vikundi ni vizuri sana kwa sababu wanasaidiana; lakini nataka niwahakikishie kwamba, kurejesha mkopo kutoka kwa kikundi ni vigumu sana kwa sababu, kwenye vikundi kuna watu ambao ni tofauti tofauti. Wana *characters* tofauti, japokuwa utatarajia kwamba, kikundi kiundwe na watu ambao wana-*share the same vision* na *passion*, lakini *unfortunately* vikundi hivi vinakuwa vigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tuangalie gharama ya kuunda kikundi. Kuna majimbo ambayo watu wanakaa mbalimbali, mtu anatoka kilometa 10 kwenda kwenye mkutano wa kikundi, anatoka kilometa 20 kwenda kwenye mkutano wa kikundi. Mpaka uunde kikundi kile, gharama ya kuendesha inakuwa iko juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema, tuangalie na ninamwomba sana Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa, aone kama haitaleta tija kufikiria namna gani ya ku-*graduate* watu hata akiwa mmoja mmoja. Nia ni kuwawezesha wanawake wa Tanzania, vijana wa Tanzania na walemavu wa Tanzania, lakini isiwe kwamba, ni lazima tung'ang'anie vikundi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambako utaona kwamba, ukimpa mtu mmoja mmoja, amekuja na wazo lake zuri, unamwuliza maswali machache; mawili, matatu, hasa wale wanaotumia benki, akienda pale, akiulizwa maswali machache, huku wana-*certify* kwamba, huyu mtu kweli ana uwezo, anaweka akiba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikundi ni ngumu kidogo, halafu huwezi kufunga kikundi. Kikundi kikishindwa kulipa mkopo utakiweka ndani! Mtu mmoja mmoja unaweza ukamwogopesha ukamwambia tutakuweka ndani wewe, lakini kikundi watu 10 ndiyo unaenda kuwakamata kuwasweka ndani, inakuwa hamna uwezo, hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye masuala ya mashirika ya umma. *Return on asset* kwenye hizi shilingi trilioni 75 kwenye mashirika ya umma ni *1.3 percent,* hiyo ni ya chini sana. *Of course* hapo nitakuwa sijawa sawa kabisa kwa sababu kuna mashirika mengine ni ya kutoa huduma za jamii, mengine pengine ni ya *infrastructure,* lakini mimi nasema kwamba *return on asset* ipo *very low*. Kwa sababu ipo *low,* inakuwa kwamba sasa *overtime* tunajikuta tunabeba mzigo mkubwa zaidi hasa tunapoona kwamba tunaendelea kuwekeza kwenye mashirika haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba kweli kuna mashirika ambayo tunatarajia pengine yafanye kwa faida kama *ATCL* bado *will take a long time* kwa sababu bado tunawekeza; pengine *TRC* na yenyewe bado *SGR* itachukua miaka pengine 20, 30 kabla haijalipa lakini tunatarajia kwamba angalau iweze kujiendesha yenyewe bila kutegemea ruzuku *after sometime*. Kwa kipindi cha hapa karibuni, lazima watategemea, lakini shirika

kama *TTCL* kuna mambo mengi ambayo yanaweza yakafanyika kuliepusha na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba *TTCL* pia kuna malengo fulani ambayo tunaangalia kwamba na yenyewe inasaidia kwenye mambo ya usalama na nini, lakini kuna eneo lile ambalo ni *technical* tu la kuendesha mtandao. Hasa kwenye kuendesha mtandao, kwa nini tusihakikishe kwamba sisi wenyewe tunai-*support*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tungesema kwamba wafanyakazi wa Serikali hata sisi Wabunge tujaribu kuwa na laini ya *TTCL* angalau tuwaongezee kidogo *volumes* na nini, lakini kusema kweli, kwa namna ile *the way it is*, ilikuja imechelewa kwenye mitandao ya simu. Kwa hiyo, imechelewa na yenyewe kupata wateja, kwa hiyo, *is the problem*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba muda mrefu umeelekezwa, unatumika kufanya marekebisho mashirika haya, tuliambiwa na hasa baada ya kumpata Msajili mpya wa Hazina tulifikiri kwamba tutapata marekebisho makubwa ya haraka, na mwenzangu pale Mheshimiwa Mwanyika amesema, tunavyozidi kuchelewa ndiyo tunazidi kuongeza matatizo, yaani kuipa Serikali shinikizo la kutoa ruzuku nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa tuone mpango kamili. Pengine kama mtunza Hazina, huyu Msajili wa Hazina hajaweza kutengeneza hiyo *business plans,* basi awa-*task* ile bodi na menejimenti ya kila shirika itengeneze mpango wa kujinasua na uwasilishwe kwake ndani ya muda mfupi, aziangalie kama zipo sahihi, basi aweze kuwapa *go ahead.* Pale anapoona kwamba hawajaweza kutengeneza mpango wa kuweza kujinasua, basi awafukuze. Afukuze menejimenti, afukuze na bodi hiyo atafute wengine watengeneze kitu kitakachoweza kujinasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikia kama *TIB* wanakimbizana na kujinasua, kila saa wanalalamikalalamika tu kwamba mtaji mdogo, mtaji mdogo. Unataka mtaji wa kiasia gani ambapo wameshapata mtaji wa kutosheleza mahitaji ya Benki Kuu?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Dkt. Kimei, ahsante.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kwa nini muda wangu huwa unaisha haraka sana? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja zote na mapendekezo yote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haji Amour, jiandae Mheshimiwa Makoa, jiandae Mheshimiwa Venant Protas.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu kuweza kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo alitoa hotuba yake kubwa iliyotuvisha nguo Watanzania pamoja na Waafrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nawapongeza Wenyeviti watatu wote waliotoa taarifa zao kwa umakini kabisa hususan ninampongeza Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Augustine Vuma, kwa taarifa aliyoitoa ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ambaye nimesimama hapa ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Mitaji ya Umma *(PIC)*. Kwanza, katika hali yote hiyo katika taarifa yetu ile imegusa mambo ambayo ni muhimu sana, lakini katika mambo ambayo imeyagusa katika taarifa yetu ni suala la mafanikio ambayo yapo kwa upande wa gawio, yapo kwa upande wa ile 15% na yapo katika masuala ya kiutendaji katika hali ya kawaida. Vilevile kuna yale mafanikio ya ongezeko la mtaji wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, nije katika taarifa yangu ambayo nitagusia katika mambo matatu, hasa nizigusie changamoto ambazo zimo katika ile taarifa yetu. Katika taarifa yetu ile utakuta kwamba kila mmoja ambaye kasimama hapa, hasa kwa upande wa uwekezaji wa mitaji ya umma amegusia mambo matatu ambayo ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazifafanua changamoto hizo hasa kwa upande wa mambo matatu. Nitagusia suala la kisheria, nitagusia suala la ukosefu wa mitaji na vilevile nitagusia suala la rasilimali watu hususan wale watu ambao wanaoziongoza zile taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwa upande wa sheria. Katika taarifa yetu ile, utakuta kwamba mambo mengi ambayo yamezungumzwa katika ile taarifa, vitu vingi ambavyo vimezungumzwa, ule upungufu ambao umo katika ule utendaji hususan katika suala la gawio kwa 15%, kwamba utakuta kuna taasisi ambazo zinashindwa kutoa lile gawio hasa kwa 15%. Hilo ukiliangalia, hasa ukitazama sheria yetu, maana yake ni kama vile hakuna mwanya wa kuweza kuwakamata wale watu ambao hawawezi kutoa lile gawio.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake kwa upande wa sheria, Kamati tumekuja sana na mapendekezo ya kuitaka ile Sheria ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma iweze kuja ili kuweza kuyaangalia mashirika yetu na makampuni yetu yaweze kujenga ufanisi pamoja na tija ya mashirika yetu.

Mheshimiwa Naibu Sika, nikiacha hilo, nije katika suala la ukosefu wa mtaji. Utakuta vilevile katika taarifa yetu kuna baadhi ya mashirika hayafanyi vizuri kama vile *TTCL*, Posta na mashirika mengine. Vilevile kuna baadhi ya mashirika kama benki ya *TIB* pia ina ukosefu wa mtaji, *TTCL* pamoja na kutokufanya vizuri, lakini pia tumegundua kwamba kuna ukosefu wa mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali katika mashirika yetu haya; Posta au *TTCL,* kutokana na hali ya ukwasi wao uliokuwa nao na ile kwamba kutokujenga ile faida au kutokuleta tija, maana yake ukiangalia kubwa zaidi pale, kwanza kuna tatizo la mtaji. La pili, kuna tatizo la kimenejimenti iliyopo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwamba kwa suala la mtaji maana yake tujaribu kulitazama kwa mfano kama *TTCL* wana vianzio vingi ambavyo vinaweza vikaleta tija kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kama *TTCL* wana ile *data centre* peke yao. Maana yake ukisema uifanyie kazi vizuri, maana yake wanaweza wakaleta tija kubwa sana, lakini inawezekana pengine pale kuna tatizo la ukosefu wa uendeshaji wa ile taasisi yenyewe. Pia kuna suala la mawasiliano ambalo pale *TTCL* pana namna ya kuweza kuingia katika suala la kuleta faida kwa mashirika yetu ya umma, pamoja na kwamba kuna *competition* kubwa ya kampuni za mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la rasilimali watu. Huku utakuta kwamba kwa kila Mbunge ambaye kanyanyuka hapa aliyezungumzia suala la mashirika ya umma, kagusa masuala yanayohusiana na bodi, kagusa masuala yanayohusiana na menejimenti. Nije kwa upande wa mchangiaji wa mwanzo Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, alizungumza wazi suala la watendaji wetu kwamba hawana weledi wa kutosha. Tunatakiwa tuwe na watendaji ambao watakuwa na weledi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la rasilimali watu katika taasisi zetu hizi za mashirika ya umma, utakuta kuna changamoto kubwa sana. Kuna mashirika ambayo utakuta wakati wa ule uteuzi wao, maana yake hapo kuna mambo mawili; kwanza, mimi nashauri Serikali kwamba katika uteuzi wa hawa watendaji kuwe na mchakato maalum wa kuweza kuwachagua viongozi. Viongozi watakaochguliwa katika mashirika haya katika taasisi zetu hizi, wawe na weledi wa kutosha na vilevile wawe ni watu ambao ni *competent* kuhusiana na zile shughuli walizochaguliwa. Hata hawa Wajumbe wa Bodi, nao pia vilevile nadhani kuna namna ya kuweza kuwapendekeza Wajumbe wenye uwezo, na weledi wa kuweza kuzisimamia zile taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu ambavyo ni viwili katika hii rasilimali watu; kuna suala la menejimenti, na kuna suala la bodi. Bodi lazima iwe na watendaji, kama ni wenyeviti, wawe ni wenye utendaji wa kutosha na pia kwenye menejimenti wale ambao ni ma-*CEO* maana yake nao wawe ni watu ambao watakuwa na weledi ambao wa kutosha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo yamezungumzwa katika suala la taarifa yetu ya uwekezaji wa mitaji ya umma ambayo amezungumza Mwenyekiti wetu. Kazungumza mengi; kazungumza mafanikio lakini utakuta kwamba shida ipo katika mambo hayo matatu. Ipo kwa upande wa sheria kwamba ni lazima Serikali kutokana na hali ilivyo na kwa namna ambavyo tunavyokwenda kwenye sayansi na teknolojia, mashirika yetu, makampuni yetu ni lazima tubadilishe sheria ambayo iliyokuwepo, maana yake tuje na mfumo mpya wa kisheria utakaoweza kuyajenga mashirika yetu na makampuni yetu kupata tija na kuweza kuleta ufanisi katika mashirika yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yetu, kwa namna yoyote ile, kutokana na ukosefu wa mtaji, maana yake tuje na taasisi itakayoweza kuwa kama ni mwarubaini wa kuweza kukusanya mtaji wa kuweza kuyasaidia mashirika ya umma. Suala la tatu ni suala la rasilimaliwatu. Maana yake ni lazima suala hili liwe na mfumo mzuri katika kuwatafuta au kuwachakata watendaji wetu wa mashirika ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya uwekezaji wa mitaji ya umma kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Makoa, jiandae Mheshimiwa Protas, ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Rwamlaza.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo Mezani. Mimi natoka Kamati ya *LAAC,* na bahati nzuri tumezipitia vizuri taarifa za *CAG* na tumeona yale ambayo yamo humo ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa, tunaipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kupeleka fedha kikamilifu kwenye halmashauri zetu. Ripoti ya mwaka huu tuliyoipitia imekuwa na utofauti mkubwa sana, hoja ya Serikali kutokupeleka fedha za maendeleo au *OC* kwenye halmashauri

pengine hatukuziona kabisa, kwa maana hiyo, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan iliweza kupeleka fedha kwa kiwango kinachohitajika na Halmashauri nyingine zilipata mpaka zaidi ya kile walichokuwa wanatakiwa kukipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hoja nyingi safari hii utaziona zilikuja kutokana na matumizi ya fedha hizo ambazo zimepelekwa na Serikali ya CCM. Nilikuwa nadhani fedha nyingi zinazotajwa na nimesomasoma, nimepitia vichwa vya habari vya magazeti ya jana kuzungumzia Kamati hii namna ilivyowasilisha hoja, ifike mahali wale Maafisa Masuuli waone aibu juu ya haya maandishi ya ovyo ambayo yanaandikwa kwa sababu ya kutokufuata miongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa makubwa yanayofanywa na Wakurugenzi ni kutokusimamia vizuri sheria na miongozo ya matumizi ya fedha ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri zao, na utaona hoja nyingi ni kuhusu *compliance*. Fedha zinatakiwa ziende *A,* wao wanapeleka *B.* Matumizi mabaya ya fedha yanafanywa kwenye ngazi zetu hizi za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine hata bajeti ambayo tunawapitisha, huwa hawaifuati na ndiyo maana utakuta fedha ambayo ilitakiwa iende kwenye miradi ya maendeleo wao wanapeleka kwenye *OC*; fedha ambayo ilitakiwa iende kwenye vikundi, wao wanapeleka kwenye matumizi yao ya kawaida; fedha ambazo zilikuwa kwenye akaunti ya amana kwa matumizi maalumu, wao wanazichomoa wanapeleka kwenye matumizi yao ya kawaida; fedha ambazo zilitakiwa zikatwe makato ya watumishi kupeleka kwenye mashirika, wao wanachukua na wanatumia fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi tuliyoyapitia kwenye taarifa ya *CAG*, yanatokana na kutokuifuata miongozo ambayo wao wenyewe wamejiwekea, na pengine Bunge limewawekea, lakini wao wanakuwa wakiivunja. Utaona kuna malipo bila stakabadhi, kwa nini inatokea hii wakati tuna wasomi na wana miongozo na wanajua malipo yanatakiwa yafanyikeje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malipo ya fedha taslimu, miongozo ya malipo ikoje? Wanafahamu vizuri kabisa, lakini hawataki kuifuata. Kuna manunuzi ambayo yamepita bila kuhidhinishwa na bodi ya zabuni; kwa nini linatokea hili na wakati tuna wasomi na wataalamu ambao wameajiriwa kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo manunuzi nje ya mpango wao wa manunuzi wa Halmashauri. Kwa nini inatokea hivyo wakati tuna wataalamu ambao tumeawaamini na ni wasomi wazuri? Tunao mwongozo ule wa 4:4:2, kwa nini uchukue fedha za walemavu ukawape wanawake au uchukue fedha za wanawake uwapelekee vijana? Miongozo wanayo, lakini hawataki kuifuata. Sasa kwa kutokufuata hii miongozo, tunatarajia *CAG* atatuletea hizi hoja mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kifanyike? Lazima sasa TAMISEMI wakae vizuri na hawa Maafisa Masuuli na kuwaeleza namna bora ya kuendelea kufuata hii miongozo ili *CAG* asituletee tena hizi hoja wakati mwingine na pengine inabidi Wakurugenzi hawa wasihamishwe mara kwa mara. Maana yake wakati mwingine tunakutana na Halmashauri, Mkurugenzi ndiyo ana siku ya pili, au siku ya tatu, au ana wiki; mwingine kahamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetamani wasingekuwa wanahamishwa ili waweze kufuta hizi hoja ili Serikali yetu iweze kunufaika na fedha ambazo inazitafuta na kuzipeleka kule kwa wananchi, ili wananchi waweze kupata matunda ya fedha ambazo zinapelekwa na Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni miongozo ya kuhamisha fedha kwenda sehemu moja na kwenda sehemu nyingine. Unakuta mradi una gharama ndogo, lakini gharama ya usimamizi ni kubwa. Mathalan, Serikali inapeleka *OC* kwa 100% ikatumike Halmashauri. Halmashauri itachukua tena fedha kutoka kwenye ile 80%, wengine 60%, wataipeleka kwenye *OC,* na fedha ile itatumika yote na itaisha. Bado watakuja kwenye 40% ya miradi ya maendeleo, napo watachukua fedha badala ya kupeleka kwenye maendeleo watapeleka kwenye matumizi yao ya kawaida. Hata kwenye mikopo ile ya vikundi kwenye ile 10%, tena

watachukua kiasi wakipeleke kwenye maeneo yao ya kawaida. Vile vile wanachukua fedha za amana wanapeleka pia kwenye matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha kabisa, unakuta wanachukua, lakini wanashindwa kuwalipa hata wale ambao wanawapa huduma. Maana yake pia kutokuwalipa wale wenye kuwapa huduma ambao ni wazabuni, zile fedha ambazo wanatakiwa walipwe pia ni sehemu ya matumizi yao ya kawaida ambayo yapo katika halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kutokufanya hivyo, bado jicho la Bunge *CAG* ataendelea kuzileta hizi hoja kila mara na haina tija, na mambo haya kiukweli yanaweza kuzuilika kama watakuwa na dhamira ya dhati ya kufuata sheria nzuri na bora zinazotungwa na Bunge; na sheria nzuri na miongozo wanayoipata kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninalotaka kuchangia ni suala la mikopo ya vikundi baada ya kufungiwa kwa muda wa mwaka. Muda uliopita palipofungiwa, sasa mikopo hii inakwenda kutolewa, tunatarajia mwongozo ambao utatoka kwa ajili ya kupeleka hizi fedha kule kwenye vikundi kwanza upunguze urasimu. Kusiwe na urasimu, kuwe na uwazi na ushirikishwaji uliokamilika, na hasa Madiwani washiriki kwa kiwango kikubwa, Waheshimiwa Wabunge, pengine na Wenyeviti wetu wa Serikali za Mitaa ili vile vikundi vikiwa vinatoka kwenye mitaa ile, viwe vinatambulika kwa viongozi wote na siyo jukumu lote lipelekwe kwa Watendaji wa Serikali, jambo ambalo lilisababisha kufeli katika fedha hizi na ndiyo utakuta kuna fedha zaidi ya shilingi bilioni 79 hazijarejeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima waangalie changamoto zilizosababisha kusimamishwa ili changamoto hizo ziweze kuondolewa na mikopo hiyo itoke na watu wanufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninapenda kuchangia; nimeona ukurasa wa 43 kwenye hotuba aliyoisoma Mwenyekiti wa *PIC* ambayo inahusiana na bei na ninayaunga mkono maazimio kuhusu bei ya umeme vijijini na vile vijiji miji. Ninaunga

mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, kwamba Serikali imewekeza fedha nyingi sana katika maeneo haya, imewekeza fedha nyingi kwenye miundombinu ya umeme; lakini tija yake na *return* yake itakuwa ni ndogo sana. Hii ni kwa sababu unakuta mtaa mzima au kijiji kimefikishiwa umeme, lakini wanakijiji hawaunganishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakupa mfano ulio hai ili uweze kuona namna gani Serikali yetu imewekeza fedha kwenye miradi hiyo lakini wananchi wanashindwa kuunganisha kwa sababu bei ni kubwa. Kwa mfano, katika jimbo tumepeleka umeme eneo la Damai. Tangu tumepeleka huu ni mwaka wa pili lakini waliojiunganisha hawazidi watano. Sasa miundombinu ile itaharibika halafu wananchi hawataunganisha umeme na hivyo Serikali itapata hasara. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ilegeze haya masharti ya kuwafungia umeme kwa ile bei ambayo wanakijiji wale hawana uwezo wa kulipa ili waweze kulipa na ili watumie fedha iliyowekezwa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo kama ya Itiso, Bolisa, Poisi pamoja na Serya tumepeleka umeme lakini wananchi hawaunganishwi kwa sababu bei ni kubwa. Wananchi hao wana matumaini na Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali kwamba siku moja itaweza kurudisha bei ile ya shilingi 27,000 ambayo wanaiweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali yangu sikivu; imeshawekeza sana; kwa kuwekeza kule basi wananchi wakanufaike na ule uwekezaji na ili Serikali iweze kurudisha zile fedha kutokana na wananchi kuunganisha na kutumia umeme huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, ninaunga mkono hoja zote tatu ambazo zimeletwa na Kamati zetu hapa. Mwenyezi Mungu akubariki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Protas, jiandae Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwe miongoni mwa Wabunge ambao watachangia hoja ya Kamati tatu za *PAC, LAAC* na *PIC* kuhusu hesabu ambazo zilikaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizoishia Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nipende kumpongeza *CAG;* kama jicho la Bunge amekuwa mtu muhimu sana wa kuonesha aidha wizi ulipotokea au dalili za wizi ambapo unaweza kutokea ili Serikali ichukue hatua kabla ya mambo hayajaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za nchi ripoti inapowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais, baadaye Kamati zako kwa niaba ya Bunge inazijadili na kuwapa nafasi Maafisa Masuuli kujitetea kuhusiana na maeneo ambayo hawakuelewana na *CAG* ili mhimili wako uweze kueleweshwa na baadaye tutoe maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona hoja imekuja mpaka humu hatujamalizana huko ujue hiyo hoja imeshindikana, kwamba walipewa muda wa kujitetea na bado hawajamalizana kujitetea kwa *CAG*. Baadaye wakaja kwenye Kamati, lakini hatujamalizana nao; na baadaye tumekuja kuwashtaki humu ili wananchi wajue fedha zao zimetumika vipi huko. Kwa hiyo, ni kitendo kizuri sana cha *CAG* kutusaidia kwa sababu sisi Wabunge pamoja na uwakilishi wa wananchi, pia tunaisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi ambayo *CAG* amerudiarudia kuyasema. Jambo la kwanza ambalo nataka nichangie kati ya maeneo machache sana ni kwamba; *CAG* kila mwaka amesema kuna mashauri ya kikodi ambayo yana takribani trilioni 10, hayajapata maamuzi mpaka leo. Hoja hii kila siku inaletwa na *CAG* lakini hatujawahi kuona upande wa Serikali umechukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mashauri yapo kwenye madawati ya usuluhishi, bado hatujaenda kushtakiana; lakini yawezekana fedha hizi kuna watu wamezikalia tu makusudi kwa sababu wanajua Serikali ipo na kwa hivyo hawawezi kuwafanya

chochote; basi anaamua tu, kila siku, kwenda kuleta *document* mpya. Leo ameleta hii kesho ameleta hii ili aendelee kuwacheleweshа na wao wanaocheleweshwa wanaendelea kuchelewa na wakiendelea kuchelewa wananchi wanaendelea kuchelewa kupata maendeleo. Sasa ifike mwisho tutafute namna ya kuisaidia Serikali. Yawezekana hizi trilioni 10 wamebishana kwa muda mrefu, basi waingie mezani ili tupate trilioni tano, mbili au hata moja, za kwetu zikafanye kazi kuliko kuwa zimekaa kwa matajiri au kwa watu kule ambapo kila siku tunasema mashauri mashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tufike mahali kama Bunge tutoe maazimio ya moja kwa moja kuhusu haya mashauri ya kikodi ya zaidi ya trilioni 10. Tunazihitaji kwenda kujenga zahanati na vituo vya afya kule majimboni, hususani katika Jimbo langu la Igalula na maeneo mengine. Tunazihitaji hizi fedha ziende zikafanye kazi. Kwa sababu haya madeni yapo na wao wanakiri kwamba madeni yapo, wanabishana tu kwenye *terms*. Sasa wakubaliane ili waweze kuyamaliza madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* ametuambia kwamba *TRA* ilishindwa kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa zaidi ya trilioni moja mwaka ulioishia Juni, 2023. *CAG* akasema kuwa sababu mojawapo ambayo imesababisha kutokufikiwa kwa malengo ni pamoja na kutokukusanya kodi, hasa kwenye kampuni kubwa. Ameeleza kuwa kuna mianya au changamoto kwenye ving'amuzi ambavyo vinasaidia kusafirisha mizigo inayokwenda nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo *CAG* ametuonesha kuwa kuna tatizo na mahali tatizo hilo lilipo. *CAG* siyo Mtendaji wa kila siku kwenye maeneo yao ya ofisi, *CAG* amekwenda kwa muda wa wiki moja au wiki mbili amebaini kuwa mfumo wa ving'amuzi una changamoto ilihali kuna wataalam ambao wamepewa kazi na wanalipwa mshahara na Serikali ya kusimamia ving'amuzi pindi gari au mzigo unapotoka bandarini mpaka unapofika *border* za Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wale watumishi wapo wapi mpaka sasa hivi *CAG* anafika na kusema kuwa mizigo hiyo

ilitakiwa ifike Rwanda, lakini haikufika Rwanda? Imepotea, haijulikani ilihali kuna utaratibu upo; kwamba kama mzigo haujafika kwenye nchi husika ile kampuni iliyohusika kupeleka ule mzigo na wanakiri kuwa ule mzigo haujafika basi inachukuliwa hatua. Hadi *CAG* anakwenda pale hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Mpaka leo tunabaki tunakusanya mapato kwa wale walala hoi wa chini. Tunakwenda kung'ang'ana na 600,000, 200,000 ilihali kuna mizigo ina kwenda haifiki nchi ya jirani, hasa mizigo ya mafuta. Mafuta mengi yanakuwa *dumped* hapa kwenye Nchi yetu ya Tanzania ilihali mafuta yale ni ya *transit*. Vyombo vipo, lakini wahusika hawachukui hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima kama nchi ione namna gani ya kusaidia kwa sababu *CAG* ameyasema. Haya maneno si yangu, ni ya *CAG,* kwa hiyo msinikaririshe maneno huko; haya ni maneno ya *CAG;* amesema kwamba mafuta yalibaki hapa zaidi ya lita 1,000,000; yakabaki hapa nchini na hayakulipiwa kodi wahusika wakayatafute yapo wapi mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, *CAG* amesema; hapa mwaka jana nilisema; kwamba, nchi yetu inatakiwa sasa tutengeneze mfumo kwa sababu imekwishakua kiuchumi. Mheshimiwa Rais amepambana nchi yetu ameikuza kiuchumi, kwa hivyo ni lazima sasa twende kwenye kuudhibiti uchumi wetu usibadilike kuwa tabu na karaha kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini, nimesema hivyo? Leo nchi yetu inaingia katika mikataba mingi ya kimataifa. Ipo mikataba ya kibiashara na vilevile ipo ya kimahusiano, ambayo itasaidia sasa kutanua wigo wa kibiashara ili wananchi wapate fursa mbalimbali za Kimataifa na wananchi wapate uchumi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la kimikataba bado kuna changamoto. Hapa nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchukua hatua haraka kwa kuwafuta kazi Mwanasheria Mkuu pamoja na Wakili Mkuu; na aliliona mapema zaidi kwa sababu na sisi Kamati tulikuwa tumekwishaliona. Hapa kuna tatizo la kutokusomana katika mfumo wa kuendesha na kusimamia mikataba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano mdogo sana; leo hii kazi ya kusimamia mikataba amepewa Mwanasheria Mkuu. Mwanasheria Mkuu anakwenda kusimamia mkataba lakini mambo yakiharibika anasema hili siyo la kwangu analipeleka kwa Wakili Mkuu wa Serikali. Sasa, yeye amekwenda kule kuingia mkataba, yeye mwenyewe amekwenda kuji-*commit terms* ambazo haziwezi kutekelezeka na anajua kabisa; halafu limemshinda anampelekea mtu ambaye hakuwepo hata kwenye makubaliano hayo. Sasa hapo ndipo mimi ninaposhindwa kuelewa; hivi Serikali kuna mifumo kweli ya kusomana hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali, katika hili, pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais ameanza kufanya mabadiliko, ni lazima Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali wafanye kazi kwa pamoja, leo tumeingia hasara ya mabilioni ya fedha. Nikutolee mfano; *CAG* amesema, siyo mimi, *CAG… (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ya pili hiyo.

**MHE. VENANT D. PROTAS**: …Hee! Haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rwamlaza, wajiandae Mheshimiwa Kuchauka pamoja na Mheshimiwa Ngassa. *(Makofi)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika taarifa ya Kamati yetu ya *LAAC*. Nipende kuchukua nafasi hii kuwashukuru hata Wenyeviti wa Kamati nyingine kwa taarifa zao walizozitoa. Nimshukuru Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Halima Mdee, ambaye amewasilisha taarifa yetu kwa namna tulivyomwelekeza. Hakuweka maneno yake, maneno yote haya yaliyosemwa ni mawazo yetu sisi Wanakamati wa *LAAC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzisema halmashauri. Tunaposema Serikali za Mitaa tunafikiria zaidi halmashauri ambayo ni Serikali iliyopo chini Serikali Kuu. Serikali

Kuu inazitumia halmashauri kuweza kutekeleza sera zake. Kwa hiyo, kwa lugha nyingine halmashauri zinarahisisha kazi ya Serikali Kuu. Kwa hiyo, tunachotegemea ni kwamba halmashauri sasa zitakuwa thabiti na zitaongozwa vizuri ili ziweze kuisaidia Serikali Kuu katika kutekeleza mambo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubali kwamba Serikali imepeleka fedha nyingi kipindi hiki katika halmashauri; lakini fedha hizo zinapotoka halmashauri wao wanasema bomba limetema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nani anayekwenda kusimamia fedha hizo? Kitu cha kwanza, je, tunao watendaji wazuri ndani ya halmashauri? Halmashauri sasa zimegeuka zimekuwa vilinge vya siasa. Sina maana ya ku-*criticize* mamlaka ya uteuzi, lakini kuna haya ya kufikiria sasa taratibu za kuteua wakurugenzi ambao watakuwa na uwezo wa kusimamia halmashauri hizi ili kuhakikisha sasa Serikali Kuu ambayo sasa inatoka fedha, ambayo inatoa sera ili wananchi waweze kupata huduma zinazostahili na hasa kuweka halmashauri na kuonesha uhalali wake wa kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao wakurugenzi ambao ni wazuri ndani ya halmashauri, siyo kwamba katika halmashauri zote 184 wote ni wabovu, lakini kuna wengine wamekaa kihasara hasara. Tuchukulie halmashauri, kama walivyosema Kamati ya *PIC,* kwamba wakurugenzi wapewe mikataba, wakurugenzi wateuliwe. Ni sawa kwa sababu Katiba yetu inasema hivi, lakini msiteue watu kwa sababu walikuwa wanagombea Ubunge; wawe ni wale ambao wana uwezo wa kuwa na akili ya kusimamia na kuhakikisha halmashauri hizi zinatimiza haja yake ya kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu niende kwenye mapato. Halmashauri hazina mikakati thabiti ya kukusanya mapato, lakini halmashauri hizi kisheria zimepewa nafasi ya kukusanya na kutumia. Kwa hiyo, zinakusanya hazifanyi *retention,* zinakusanya na kutumia. Kwa hiyo, tunategemea watahakikisha kwamba hizo fedha za wananchi zinatumika ipasavyo katika kuhakikisha

wanatimiza malengo yao ya kuangalia ustawi wa wananchi katika halmashauri yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yamesemwa mengi, utaweza kuona ni namna gani halmashauri zimeshindwa kukusanya mapato ambayo yameoneshwa katika taarifa yetu. Kwa mfano, halmashauri zinashindwa kukusanya ushuru wa huduma kwa sababu hawana taarifa ya mauzo ghafi ya wale wanaotoa huduma. Sana sana wanategemea *TRA*, lakini *TR*A yenyewe wakati mwingine haitoi taarifa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Halmashauri, ukienda Kibaha na Chalinze wale wana viwanda, lakini ushuru wa huduma unalipwa katika Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam na kwa hiyo kwa sasa Kibaha na Chalinze hawawezi kukusanya ushuru huo. Kwa hiyo, tunataka Serikali ilitazame jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kukaimu kwingi sana katika halmashauri, Idara nyingi nyeti zinakaimiwa na ni kwa nini? Ni kwa sababu vigezo vilivyowekwa kwa ajili ya kupandisha watu madaraja ili waweze kufikia kuwa wakuu wa idara vinawaumiza. Ni pamoja na kwamba ili mtu awe Mkuu wa Idara awe na *degree* ya *masters.* Kwani *masters* ndiyo inayosimamia mambo? Kinachosimamia ni ule uwezo wa mtu. Wawapime watu kwa kuwawekea *key performance indicators* ili mtu asipotimiza asimamiwe, atimize na aweze kuleta matokeo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri pale kuna Mkurugenzi anapaswa kusimamia watu wake wa chini, kuna *RAS* anapaswa kusimamia halmashauri, kuna Mkuu wa Mkoa na pia kuna TAMISEMI. Nina uhakika kwamba TAMISEMI wanafanya kazi, lakini kazi hii inawaelemea kwa sababu hii Wizara ni *giant*. Ina watu wapo pale wanakodoa macho wanasubiri mpeleke fedha, wanasubiri wakusanye halafu wanafanya mambo wanayoyataka wao. Kwa kweli tunawashukuru Mawaziri, wale wa TAMISEMI wanafanya kazi, wanasimamia lakini wanazidiwa. Kwa hiyo, ni vyema wahakikishe kwamba wanapata wasaidizi ambao wana uwezo wa kuziendesha halmashauri hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutokupeleka fedha za maendeleo; halmashauri inakusanya fedha na sisi hii sera au tuseme maelekezo ambayo tulitoa, kwamba halmashauri zichukue sehemu ya asilimia ya mapato ili waweze kuwaonesha walipakodi katika nchi; kwamba tunalipa kodi katika halmashauri lakini tunapata huduma fulani au mradi fulani. Kwa hiyo, sasa hiyo asilimia ambayo tunawapa ambayo tunawaambia walipe hawapeleki na nyingine wanakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbuka halmashauri zinapewa fedha za *OC* kutoka *Central Government,* wanawachangia fedha nyingi. Kwa mfano, nilikuwa naangalia, hebu twende Halmashauri ya Iringa, wamepewa *OC* bilioni 1.17, yaani wanakusanya fedha, wanachukua ile 60% yao, bado Serikali ina wa-*supplement* fedha, halafu wanalamba zote. Yaani ile *supplement* ya Serikali *(60%)* na za maendeleo nazo wanazitumia. Kwa hiyo, kule ndani ya halmashauri hawategemei kupata mabadiliko makubwa ambayo yanatokana na usimamizi wa halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi kutokamilika; ipo miradi mingi ambayo haikukamilika, ya mabilioni ya fedha, zaidi ya milioni 206, lakini jambo hili linatokana na nini? Ni kwa sababu Serikali ilitoa sera ya wananchi kuanza kuibua miradi na miradi haikamiliki. Kwa hiyo, kunakuwa na magofu mengi sana ya shule na ya zahanati ambayo hayakamiliki. Tunaomba Serikali iweke sera, kwamba kama wananchi wanaibua mradi halmashauri iingilie kati ili waweze kuwaelekeza cha kufanya wakati halmashauri inapopata fedha. Kwa hiyo, yapo mapagale na maboma mengi sana, ambayo mpaka sasa hivi Serikali haikamilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri Serikali sasa; kuwepo na udhibiti wa matumizi ya fedha. Kama Serikali haiwezi kudhibiti matumizi ya fedha, msitegemee kwamba nchi hii, tutapiga kelele, lakini hakutakuwa na mabadiliko makubwa na wananchi wataendelea kulia. Kama sisi hatuwezi kuweka udhibiti wa fedha hatutegemei hata siku moja kulipa watu wetu mishahara mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kujenga barabara, tumalize; tujenge mashule, tumalize; tujenge hospitali, tumalize halafu tupate pesa za kuweza kusaidia watu wetu kupata mishahara mizuri halafu na wenyewe waboreshe maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya mapato. Halmashauri zinashindwa kuandaa vyanzo vya mapato, yaani unaweza kushangaa nchi hii bado tunategemea vyoo kukusanya ushuru. Nashangaa unawezaje kwenda na *POS* kumlipisha mtu ambaye anaenda chooni halafu unakuta halmashauri inakuja kabisa, Mkurugenzi anakuja na *book* anatuambia sisi sasa tuna miradi, miradi yetu tumejenga vyoo tunakwenda kukusanya, hii ni nchi gani ambayo miaka 60 ya uhuru bado tunakusanya ushuru wa vyoo? *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ipo miradi mingi. Kuna viwanda vidogo vidogo…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ya pili hiyo.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, wajiandae Mheshimiwa Nicholaus Ngassa na Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Awali ya yote niwapongeze Wenyeviti wetu wote watatu kwa hotuba zao nzuri. Vilevile nimpongeze CAG kwa namna ambayo anatusaidia Bunge hili kuangalia kama waswahili wanavyosema; "wacha mvua inyeshe tuone panapovuja."

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza na suala la madeni makubwa kwa taasisi mbalimbali za Serikali. Mimi nianze kushauri kwa sababu mlipaji mkubwa ni Serikali ambayo ndio Hazina. Utakuta Wizara inadaiwa bili ya maji au taasisi inadaiwa

bili ya umeme. Kwa nini basi fedha hizi badala ya kupelekwa kwenye Wizara kama (*OC)*, kwa nini mlipaji huyu asilipe moja kwa moja *TANESCO?*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa maana kwamba, Serikali, *TANESCO* wapeleke bili Wizarani, Katibu Mkuu asaini kukubali kwamba hiyo ni bili halali iende Hazina ikalipwe. Kwa sababu unapopeleka *OC* kwenye taasisi yoyote ile unakuta mwezi ule kwenye taasisi ile wana vipaumbele vyao wakaona kwamba kulipa bili ya maji au kulipa bili ya umeme sio kipaumbele kwa mwezi huo. Kwa hiyo ndiyo kisa cha haya madeni kuendelea kurundikana.  Kwa hiyo, nashauri taasisi kwa taasisi hizi fedha zote kwa sababu Mlipaji Mkuu ni mmoja analipa Hazina, basi hizi fedha badala ya kupeleka kwenye Wizara au kwenye taasisi husika ziende moja kwa moja kwenye taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linakuja kwenye mashirika yale ambayo tulitegemea yatengeneze faida, lakini *CAG* anaonesha hapa kwamba mashirika haya yanashindwa kutengeza faida. Hapa naomba niseme kwamba, ipo kasoro ambayo nimeiona kwenye haya mashirika; kwanza kwenye sheria zetu za manunuzi ya umma. Hapa napo nipendekeze kwamba, Sheria yetu ya Manunuzi ya Umma ifanyiwe maboresho kwa sababu haiwezekani Sheria hii moja ya Manunuzi ya Umma ikaenda kwenye taasisi zote zikiwa zina ibara zinazofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitoe mfano wa Taasisi kama *TTCL*. Tunategemea *TTCL* waje kushindana na *Vodacom* ama na *Tigo*. Wanasaini mikataba labda *TTCL* wana minara 10 na *Vodacom* wana minara 10; lakini *TTCL* kwa Sheria yetu ya Manunuzi ya Umma itawachukuwa miezi sita kuja kumpata mkandarasi na kutekeleza huo mradi na wakati wenzao hao *Vodacom* au *Tigo* wanasaini leo Jumatatu wanaanza kazi kwa sababu sheria zao hazipo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi nao vilevile kwenye Sheria yetu ya Manunuzi lazima tuchambue kwamba; kwenye Sheria hii ya Manunuzi hayo mashirika yanayokwenda kutengeneza faida yafuate mlengo gani na hayo mashirika

ambayo hayatengenezi faida yaende na mlengo gani. Vilevile, hoja nyingine za *CAG* zinaweza zikafutwa au zinaweza zikapungua iwapo tutakwenda kufanya marekebisho baadhi ya sheria zetu, kwa sababu, hoja zingine zinaibuliwa tu kwa sababu kutokuwa na sheria isiyokuwa rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ipo hoja iliyoibuliwa na matumizi mabaya ya fedha za Mfuko wa Jimbo. Sisi kwenye Kamati ya TAMISEMI tuliwaita, tukawaambia TAMISEMI watuletee halmashauri zote zinazodaiwa kutumia fedha hizi vibaya. 80% ya hoja zile zilikuja zile halmashauri ambako zimenunua kompyuta za shule, zimenunua *photocopy machine* za shule na pengine wamenunua viti. Hizo zote zinaonekana ni matumizi mabaya ya hizi fedha kwa sababu tu, fedha hizi kwenye sheria inasema inakwenda kutekeleza miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo itakuja tafsiri ya neno miradi ya maendeleo. Hivi mimi Mbunge nimekwenda kwenye mahafali ya shule fulani wakaniambia changamoto waliyonayo ni *photocopy machine,* nikachukua fedha za Mfuko wa Jimbo shilingi milioni tatu au milioni nne nikanunua *photocopy machine;* eti naambiwa ni matumizi mabaya kwa sababu sio mradi wa maendeleo. Kwa hiyo utaona kabisa kwamba hapa hoja zimeibuliwa kwa sababu tu ya tafsiri ya neno miradi ya maendeleo. Kwa hiyo wazo langu hapa ni kwamba ipo haja sisi kuja na marekebisho ya baadhi ya sheria ili kupunguza haya malalamiko au hizi hoja mbalimbali zinazoletwa na *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine, tunayo Sheria ya Manunuzi ya Umma lakini kadri tunavyokwenda; mwaka jana tumepitisha hapa Sheria ya *NeST*. Hivi, tumewianishaje Sheria hii ya *NeST* na Sheria ya Manunuzi ya Umma? Kwa hiyo na hapa hapa utaona kwamba ipo haja kubwa sana ya kuleta hizi sheria, baadhi ya taasisi ziletwe hizi sheria zake tuzifumue ili ziendane na wakati na ziendane ziweze kujibu hizi hoja za Mkaguzi Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusu utendaji wa baadhi ya taasisi za umma. Ninaamini ufanisi wowote wa taasisi yoyote ukiondoa muundo wa taasisi hiyo au sheria ya taasisi hiyo

unategemea sana weledi na uwezo wa Mkuu wa Taasisi husika. Hivyo basi, ukiona taasisi haifanyi vizuri, basi uwezekano mkubwa Mkuu wa Taasisi hiyo kukosa weledi au kukosa ujuzi husika wa taasisi anayoiongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa niende moja kwa moja kwenye halmashauri zetu. Serikali Kuu imepeleka fedha nyingi sana kwenye halmashauri zetu, ni ukweli usiopingika. Je, hawa tuliowapelekea fedha kwenda kuzisimamia, uwezo wao ukoje? Wamepatikanaje? *Vetting* yao ikoje? Kwa sababu Serikali hivi imeshafanya tathmini kuona taasisi inayoongozwa na mtu ambaye ana-*know how* ya taasisi hiyo, *performance* yake ikoje na taasisi ambayo inaongozwa na kiongozi ambaye hana *know how* ya taasisi hiyo *performance* yake ikoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu naamini ukimpeleka Mkurugenzi kwenye Halmashauri X hana taaluma ya utawala, hana taaluma ya uchumi, mnakwenda kumtumbukiza samaki kwenye bwawa la mamba, kwa sababu pale atakutana na wachumi, atakutana na watu wenye masomo ya biashara, wenye taasisi waliobobea kwenye taasisi zao. Uwezekano wa Mkurugenzi huyu kudanganywa ni mkubwa. Ushauri wangu; tuhakikishe kwamba wale tunaowakabidhi taasisi za kuiongoza basi wawe na uwezo na weledi wa taasisi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko hoja nyingine za Serikali kudaiwa na wazabuni (madeni ya wazabuni). Kama nilivyoshauri kwenye taasisi za Serikali kwa Serikali kudaiana na hata haya madai ya wazabuni. Ifike mahali mzabuni apeleke madai yake kwa Katibu Mkuu wa Taasisi husika au Afisa Masuuli wa taasisi husika, isainiwe apeleke moja kwa moja Hazina wamlipe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hizi fedha sio kwamba hazipo, tumeshazipitisha hapa kwenye bajeti kwamba taasisi fulani italipa bili ya umeme kiasi fulani, italipa maji kiasi fulani na matumizi mengine mengine; kwa hiyo hizi fedha wanazo. Kinachotofautiana hapa ni vipaumbele vya taasisi au Wizara husika. Kwa hiyo hayo ni machache nilikuwa niyashauri kwenye hotuba hizi zote tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, wajiandae Mheshimiwa Abubakari Asenga na Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia taarifa zilizo mbele. Kabla ya yote niseme naziunga mkono taarifa zote tatu zilizowasilishwa na Wenyeviti. Pia, naunga mkono taarifa yetu ya *PIC* iliyowasilishwa na Mwenyekiti wetu mahiri Mheshimiwa Vuma Augustine Holle, Mbunge wa Kasulu Vijijini. Pia nawashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kuhakikisha tunakamilisha hii taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo mawili ambayo sana sana itakuwa ni kuhusu suala la tija na ufanisi *(effectiveness* na *efficiency)* katika mashirika yetu ya umma na katika maeneo ambayo Serikali yetu imewekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ambalo ningependa kuchangia mchana huu ni eneo la uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka 2022/2023, kama taarifa yetu ambavyo inasema. Serikali yetu katika sekta ya mashirika ya umma ambapo takribani mashirika 250 ilikuwa imewekeza takribani shilingi trilioni 72 za Kitanzania. Kwa mantiki hiyo kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa *commitment* kubwa ambayo ameiweka katika mashirika yetu na kuhakikisha wanapata ukwasi wa kutosha katika kuendesha shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia uwekezaji wa shilingi trilioni 72, lakini mapato yasiyo ya kikodi na gawio ambayo ni *return* yake ni asilimia moja kwa maana ya shilingi trillioni moja na matarajio ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha tunakwenda mpaka 30%. Sasa kama Mbunge na kama kijana ambaye natamani kuona Taifa langu linakwenda mbali; nini nishauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza; lazima tuwe na mfumo madhubuti utakaohakikisha matarajio ya Mheshimiwa Rais na kiongozi wetu Mkuu wa Nchi anafanikiwa. Unapoongea suala la mfumo huwa ni mambo mawili tu. Jambo la kwanza, ni suala la taasisi kwa maana ya *institutionalization* na jambo la pili kwa maana ya sheria. Kama nchi, kama tumeamua kusonga mbele lazima tuwe na sheria itakayohakikisha kama Taifa tunapata na kukusanya vya kutosha kutoa kwenye mashirika yetu ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nadharia na dhana kwamba uweledi; mimi ni mataalam wa masuala ya utawala sikubaliani nayo sana. Kwa sababu gani? Serikali inapoajiri Wakuu wa Taasisi za Umma jambo la kwanza wanasema wanaweka pale sifa za waombaji au sifa za waajiriwaji. Utakuta mashirika ya umma kwa kiwango kikubwa mashirika yetu ya umma wenye elimu ya chini wanaoongoza nchini hapa wana *masters*, wengine wana *PhD* na wengine ni *Professors*. Utasemaje hawana weledi hawa watu? Weledi upo, tunahitaji sheria kali itakayowadhibiti hawa watu ndiyo tutaamua kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunatoa mifano, unasema zamani Singapore ilikuwa kama Tanzania, Malaysia ilikuwa kama Tanzania wenzetu wamefikaje huko? Ndiyo maana tunasoma zile *literature*, lazima tuamue tusonge mbele Waheshimiwa wenzangu. Tukiendelea kusema weledi hawa watu wana weledi. Ameenda amesoma na hata zile bodi utakuta labda mtu alikuwa kiongozi Serikalini, amestaafu bado ana nguvu amepewa Bodi, bado ana weledi na ana uzoefu juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hapa ni mfumo wetu. Lazima tubadilishe sheria, lazima tubadilishe hizi taasisi na ndiyo maana tunashauri sheria ya uwekezaji nchini iletwe Bungeni tuipitishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia katika suala la mashirika ya umma. Kama ambavyo matarajio ya Mheshimiwa Rais yamesema; tunataka angalau tukusanye 80% kutoka haya mashirika ya simu. Lazima kuwe na uwajibikaji *(accountability)*. Hamuwezi kwenda

bila *accountability* kwenye taasisi ambazo mtumishi wa umma anaingia kazini saa 2.00 au saa 3.00, anakwenda kunywa supu, anakaa mpaka saa 5.00 anapiga *story*, anarudi saa 7.00 anaenda *lunch*, anarudi ofisini saa 9.00 na saa 9.30 anaenda nyumbani. Hatuwezi kupata ufanisi katika nchi hii ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuweke sheria za kubana mifumo yetu. Mheshimiwa Rais amekuwa anasema mifumo haisomani. Hii maana yake nini? Mifumo haisomani haimaanishi kwamba macho haionani, mifumo haisomani maana yake ni urasimu tulionao nchini. Unakuta mtu amepitishiwa taarifa yake *BRELA* halafu *TIC* faili hilo hilo linaenda linasubiri wiki mbili tenakwa ajili ya maamuzi mengine wakati *BRELA* na *TIC* wanaamua kitu kimoja ambacho kinaenda kuamua kuhusu uwekezaji wa nchi. Ndugu zangu hatuwezi kwenda katika mazingira ya urasimu wa aina hiyo, lazima tubadilike Watanzania kama tunataka kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimekuwa nikisema kwenye Mpango wa Maendeleo Taifa wa sasa tunaoamua kupitisha 2025 - 2050 lazima tuachane na urasimu kama tunaamua kwenda mbele. Kama tunaamua kubaki tunapiga danadana, tutaendelea na utaratibu wa *business as usual,* watakuwa wananabadilishwa wakuu wa mashirika ya umma, wanabadilishwa Wenyeviti wa Bodi, lakini biashara itakuwa *business as usual*. Nashukuru kwa jambo la kwanza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ninapenda kulichangia ni kwenye suala la ufanisi na tija ni Umeme vijijini *(REA)*. Kwanza nianze kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Sita. Tulikwenda pale kuangalia Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Ndugu zangu kwa ambao hamjafika, pale ni uwekezaji mkubwa sana umefanyika kwa nchi yetu; tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii miradi tumezoea kuoina Brazil, Ethiopia na Misri kule. Ukienda pale ni uwekezaji mkubwa lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko; hongera sana kwake.

Alipoingia ule mradi ameukwamua kwa kiwango kikubwa, ni uwekezaji mkubwa. Tulifika pale sisi Wajumbe wa Kamati, kwa mtu ambaye huwezi kujua uwekezaji uliofanyika pale unashangaa. Tulitembea na gari pembeni ya mradi barabara ya lami kwa saa moja na bado tunaendelea kuzunguka tunaangalia mradi. Serikali yetu imefanya jambo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tushauri kitu kimoja kwa ajili ya ufanisi na tija. Pamoja na kuwekeza shilingi trilioni 6.5, tumeweza kusambaza umeme vijijini. Kwa sasa nchini karibu vijiji vyote vimefikiwa na *line* za umeme lakini bado kuna changamoto kubwa ya wananchi kupatiwa umeme. Nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, waumize vichwa na wataalam wao tuhakikishe nyumba za wananchi zinapata umeme. Wao watabanana nao kwenye ankara kule kwenye *tariffs;* wapate umeme kwa sababu hakutakuwa na tija, umeme umetembea kutoka mjini, umekwenda kilometa 20 au 30, halafu unakuta kwenye hicho kijiji mwananchi mmoja tu ndiyo anaunganishiwa umeme. Pale tutakuwa tumewekeza kwa hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba watafute *model* nzuri wahakikishe wananchi wanaunganishiwa umeme hata kama ni bure. Akiwekewa umeme inakuja kwenye suala wao wawabananishe kwenye viwango vile vya *tariffs* zile za malipo. Ni bora mtu akose hela ya kuweka LUKU ila awe na umeme ndani, siku akipata hela ataweka na umeme atawasha; umeme ni maendeleo. Hilo jambo la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, ni mashirika ya umma na mitaji. Ningependa kunukuu taarifa ya Kamati yetu hapa; "Baadhi ya taasisi na mashirika ya umma kuwa na mitaji mikubwa isiyozalisha *(nonproductive asset)*."

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi umebaini kwamba kuna baadhi ya mashirika yana mitaji mikubwa ambayo haizalishi *(nonproductive)*. Mitaji hiyo ni kama vile majengo, ardhi, mitambo iliyopitwa na wakati ambayo haina ufanisi ikilinganishwa na teknolojia iliyopo kwa sasa. Hili nalo ni jambo lingine katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusikubali kuendelea kubaki na mambo kama haya. Shirika lina uwezo, lina *asset* halafu halizalishi haya mamo tusikubaliane nayo. Waziri wa Uwekezaji na Waziri wa Viwanda ni wajibu wao kuhakikisha tunasonga mbele kama nchi. Tukiendelea kukumbatia mambo kama haya, ndiyo yale yale unakuta mtu ana uwezo anatoka kwenye shirika binafsi anakwenda kwenye shirika la umma anashindwa kufanya kazi. Tuachane na hayo mambo. Kama Taifa lazima tusonge mbele. Tubadilishe sheria ili tuweze kuleta tija katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii ya kuongea mchana huu na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Abubakari Asenga, wajiandae Mheshimiwa Mohamed Kassinge na Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia taarifa za Kamati zetu tatu. Kama walivyotangulia kusema Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa na yamesemwa mengi na ni tajamala na sudi na ni shukrani kwa Mwenyezi Mungu kupata nafasi ya kusimama hapa katika Bunge lako, kuweza kuwasilisha mawazo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuendelea kuunga mkono uwazi katika Serikali yake na ndiyo maana taarifa kama hizi za Kamati ya *CAG* zinasomwa wazi na kila Mtanzania anaweza kujua namna Serikali yake inavyoenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wetu walivyowasilisha mara kadhaa hapa, taarifa ina mazuri na ina changamoto zake na changamoto katika maendeleo yetu ni kawaida, zitakuwepo lakini kubwa ambalo Watanzania wanataka kuliona ni kwamba, wanaposema kuna changamoto au ubadhirifu wa fedha au kama kuna kasoro, basi zichukuliwe hatua kwa haraka na tuna imani na Mawaziri wetu, watazifanyia kazi changamoto hizo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nikushukuru wewe wakati naelekea kwenye kuchangia kwa sababu ulitembelea jimboni kwangu takriban wiki moja ama mbili zilizopita. Ukaonana na wananchi wa Kilombelo, ukapata nafasi ya kuwasikiliza katika changamoto zao za miwa, wengine wakakwambia mambo ya barabara za mitaa zimeathirika sana na wengine wakakwambia mambo ya tuta na mafuriko na wewe ukatuahidi kwamba, kwa sababu meza yako ni kubwa basi utaendelea ku-*push* kwa kadri utakavyoweza na sisi tuna imani na Mawaziri wetu ambao wamekuja mara kadhaa Kilombero na kwa kweli wametusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia hasa katika Kamati mbili za *PAC* na *LAAC* na nilikuwa Mjumbe wa *LAAC* kabla ya kuwa Mjumbe wa Miundombinu. Nimepitia kwa haraka haraka tu na mambo ni mengi, lakini nimechagua machache ambayo nafikiri naweza nikatoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, katika *PAC* nimesoma, jambo kubwa la *TRA (Tanzania Revenue Authority)* na mapato. Kwa nini nimesoma jambo hili? Kwa sababu sisi kama Waheshimiwa Wabunge mara zote tukisimama hapa tunataja vitu ambavyo tunataka pesa. Sasa kwa namna yoyote ile lazima tuwe makini sana na Serikali yetu inapataje pesa na mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unashangaa sana unapoona Taarifa ya Kamati na katika nchi yetu *Tanzania Revenue Authority* mpaka leo inaandikiwa na *CAG* hapa kwamba haitambui wateja wake wote katika nchi yetu, haitambui walipakodi wote katika nchi yetu. Bado *TRA* inaomba kuwezeshwa kwa kiasi kikubwa katika kuwa na mfumo utakaotambua walipakodi wote wa nchi hii ili tuweze kukusanya na kufanya maendeleo ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuwa, *TRA* inaomba iwezeshwe katika mfumo wa *data cleaning up exercise* ili uweze kufuta *data* zisizo rasmi za walipakodi na kuondoa malalamiko yale ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akisema mara nyingi sana, wafanyabiashara wanalalamika kusingiziwa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa *TRA* chini ya Mkurugenzi Mkuu wa *TRA* wa sasa hivi kwa kweli tuna imani kubwa anaendeleza ile sera ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kwamba *TRA* siyo kituo cha polisi. Ili *TRA* iweze kupata zaidi ikae na wafanyabiashara, izungumze nao changamoto zao na nimeona Mkurugenzi Mwenda anafanya kazi hiyo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara husika ihakikishe inaisaidia *TRA* kuondokana na hizo hoja za *CAG*, ikamilishe mifumo hii. Pamoja na kwamba inafanya busara kukaa na wafanyabiashara kuzungumza nao na kuondoa yale mambo ya upolisi kamata kamata, basi tupate mapato ya kutosha na nimeona mwaka huu katika taarifa zao ni kwamba wameanza kukusanya mpaka kuzidi katika kiwango cha asilimia ambacho walipaswa kutozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, katika *PAC* nimeona taarifa ya kuhusu Bodi ya Mikopo, wenzangu wamesema hapa, nami nataka kusema. Taarifa ya *CAG* inasema, mara zote ambazo wanaihoji Bodi ya Mikopo, Bodi ya Mikopo imeonesha kuwa na upungufu wa bilioni 199 na kuna taarifa baadhi ya waombaji wa Bodi ya Mikopo wanapewa pesa nyingi kuliko waliyoomba na kuna wengine walioomba wanapewa pesa kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili wamesema kwamba vijana hawa kuna wengine wanakosa kupewa mikopo kwa sababu ya Vitambulisho vya Taifa kwa maana ya *NIDA*. Wamependekeza kwamba, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iwe sasa ni mfuko rasmi ili ipate vyanzo mbalimbali vya mapato na vingine kutoka katika uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hili ni suala la msingi sana, kwamba, lazima sheria ije hapa tufanye mabadiliko ya bodi ya mikopo iende katika mfuko rasmi ili iweze kupata vyanzo kutokana na uwekezaji, kwa sababu kama *CAG* anaenda anawahoji Bodi ya Mikopo, kila mwaka inakuwa *story* za upungufu wa bilioni 199. Pamoja na Mheshimiwa Rais kuwekeza

nguvu kubwa na kuongeza posho kwa wanafunzi lakini hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaumia sana wewe kama mwakilishi wa wananchi ama kama Mbunge ukikutana na kijana ambaye ameshindwa kwenda chuo kwa sababu ya kukosa pesa. Sasa sisi ndiyo tunachangia kama Waheshimiwa Wabunge na ndiyo nimesema lile la *TRA*, wakusanye vizuri ili Mheshimiwa Rais apate nguvu ya kukidhi hii bilioni 199 ili hawa vijana wote wanaoingia chuo kikuu waweze kupata pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupa mfano, nilikuwa jimboni, nimenunua maji katika duka fulani, kuna binti alikuwa pale akaniona, akanikumbuka akasema, Mheshimiwa Mbunge nina shida. Akaja pembeni akawa ananielezea, mwaka jana nilipata nafasi ya kusoma *University of* Dar es Salaam; nilishindwa kwa sababu niliomba mkopo nikakosa. Angalia kwenye simu yangu Mheshimiwa Mbunge na safari hii wameniita lakini nimeshindwa kwenda kwa sababu ya mkopo. Kweli nimechukua zile *details* nimempa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, nimewapa watu wa Bodi ya Mikopo wamsaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kweli ni jambo la kuliangalia kwa umakini sana, ushauri huu ulileta na Kamati na Taarifa aliyoitoa CAG kwamba Mfuko huu ubadilishwe ili uweze kupata vyanzo mbalimbali, lifanyiwe kazi haraka sana ili tusaidie vijana wetu kwa sababu bilioni 199 kwa kweli siyo fedha ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka, nigusie Kamati ya *LAAC* ambayo nilikuwa mjumbe hapo nyuma na jana namshukuru sana Makamu Mwenyekiti na ni Mwenyekiti wa *LAAC* nimeona amewasilisha hapo, jioni nimemuona Makamu Mwenyekiti wa *LAAC* akifafanua mambo katika Televisheni moja ya Azam huko na kwa kweli katika lugha ambayo Makamu Mwenyekiti ameongea kuhusu *LAAC*, kama kweli Kamati yetu imeongea namna ile, basi sisi Waheshimiwa Wabunge na lile jambo limesemwa hadharani, ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Waziri Mchengerwa amebebeshwa zigo la TAMISEMI na yale madude yote, basi huu mzigo ni wa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini jambo hili, Mheshimiwa Waziri Mchengerwa atatusaidia kupunguza na yeye ni jembe, tunajua yeye ana kifua kikubwa, Mheshimiwa Rais alishamtaja, apunguze hizi hoja za *CAG*. Mfano, ukurasa wa 19, Taarifa ya *LAAC* inasema, bilioni 6.17 za *POS* za mashine ile ya kukusanya mapato hazijapelekwa benki. Sasa kama kweli *CAG* amelisema hilo jambo na vielelezo vipo vikathibitisha, kupitia Mheshimiwa Waziri Mchengerwa sisi tuna imani atachukua hatua tu. Yaani tungekuja hapa mwishoni kwenye majumuisho, atuambie wale ambao wana pesa *cash* hawajazikusanya benki, hatua gani zimechukulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nikiwa ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* hili jambo linasemwa, pamoja na mambo haya katika halmashauri zetu, sisi Ifakara *Alhamdulillah* tunaenda vizuri, lakini tulishasema kwamba halmashauri hizi ziwezeshwe katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kiwe jicho la mkurugenzi pale kabla taarifa za *CAG* hazijaja. Kile kitengo kiwezeshwe vya kutosha ili kiweze kusaidia halmashauri kuweza kutimiza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 22, kuhusu matumizi ya fedha taslimu, mpaka leo tunazungumza hapa. Mwaka jana taarifa hiyo 2023/2024, unaona kabisa Mheshimiwa Waziri Mchengerwa anabebeshwa zigo hilo la kwamba watu wametumia fedha taslimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa unaofuata wa 27, kuhusu madeni ya wazabuni, kwa kweli hata kwenye halmashauri yangu kuna malalamiko, lakini mkurugenzi hana majibu kwamba kuna baadhi ya fedha zimerudi katika mfumo, hajazipata akirejeshewa ataweza kuzilipa. Kwa hiyo, nami nasema, tunajua kweli siyo kwamba kila anachokisema *CAG* basi kinakuwa ni kosa. Mfano, halmashauri ikinunua *cement* kwa shilingi 15,000 na ile *cement* ikaenda ikajengea darasa au jengo bila kuweka vielelezo ya kutosha kwa *CAG* huo ni wizi; lakini halmashauri hiyohiyo ikinunua *cement* kwa 20,000 ikaambatanisha risiti na vielelezo kwa *CAG* hiyo inakuwa ni uhalali, hakuna wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hapa inakuja hoja ile ya *CAG*, kuwepo kwa mfumo mzuri ambao utatupa malighafi, utatupa *raw material* kwa bei ya soko kiasi kwamba tunaweza kununua vitu kwa bei rahisi na kulipa kwa wakati na kupunguza hizi hoja zote ambazo *CAG* amezionesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ally Kassinge, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula na Mheshimiwa Manyinyi, mjiandae.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia hoja za Kamati zetu tatu. Kamati ya *PIC*, *PAC* pamoja na ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* na kwa muktadha wa mchango wangu mchana huu nitajikita zaidi kwenye Kamati inayosimamia Hesabu za Serikali za Mitaa ya *LAAC* inayoongozwa na mama yangu Halima Mdee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri zipo kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ndiyo ibara ambazo zinazipa uhalali wa halmashauri kuwepo kwake na utekelezaji wa majukumu yake. Pamoja na hayo, zimetungiwa Sheria Sura 287, 288 na Sura 290 ambayo ndiyo inahusika zaidi katika kuzipa uwezo halmashauri zetu wa kukusanya mapato yake na kwa maana hiyo kwa kiasi fulani kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote haya, bado kumekuwa na changamoto ya ukusanyaji wa mapato katika halmashauri zetu. Zipo halmashauri ambazo zinazidi malengo waliyojiwekea na nitumie fursa hii kuzipongeza halmashauri hizi. Kwa maana hiyo, imepunguza kwa kiwango kikubwa utegemezi kutoka Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kipindi cha hivi karibuni imepunguza kwa kiwango

kikubwa sana hoja ya Serikali Kuu kutokupeleka fedha aidha za matumizi ya kawaida au ruzuku ya maendeleo kwenye halmashauri zetu. Katika eneo hili tunaishukuru na kuipongeza sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la ukusanyaji wa mapato katika mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, imekuwa changamoto kwa halmashauri ambazo zimeshindwa kufikia malengo. Hapa utaniruhusu nizitaje kwa uchache wake katika ukurasa wa 12 kama ambavyo Taarifa ya Kamati ya *LAAC* inazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Halmashauri ya Biharamulo, Tandahimba *DC*, Mtwara Mikindani, Nanyamba, Handeni, Newala, Kigoma Ujiji, Lushoto, Longido pamoja na Kilolo, hizi zimeshindwa kabisa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato. Ninatoa ushauri kwa Wizara inayosimamia Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. Hivi je, wanapata nafasi ya kukaa na wakurugenzi katika halmashauri hizi kufanya tathmini kwa nini wameshindwa kutimiza malengo haya? Wamepata kukaa na wakurugenzi kuweza kuainisha vyanzo vipya vya mapato? Wamepata kukaa na wakurugenzi kuweza kubaini ni kwa nini wanashindwa kufikia malengo? Inawezekana pengine ni kwa ajili ya uchache wa vyanzo vya mapato katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa ushauri kwa Serikali yangu hususan Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuweza kufanya tathmini hii ili halmashauri zetu ziweze kufikia malengo ya ukusanyaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninaweza kuchangia ni mawakala wetu katika mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kutowasilisha mapato. Katika Taarifa ya *CAG*, imebaini kwamba, katika halmashauri zipatazo 12 kiasi cha shilingi bilioni 5.65 zimeshindwa kuwasilishwa kwenye halmashauri zetu na mawakala wa ukusanyaji wa mapato. Kitu cha kushangaza mpaka taarifa hii inawasilishwa hapa Bungeni, hatujaelezwa ni hatua zipi za kisheria zimechukuliwa na Serikali kwa mawakala ambao bilioni 5.65 zipo mikononi mwao. Hizi ni fedha za

wananchi, zingeweza kwenda kujenga zahanati, madarasa, barabara na miradi mingine ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninaweza kuchangia ni madeni ya watumishi; katika halmashauri 55 ambazo zimeweza kuhojiwa na Kamati, kiasi cha shilingi bilioni 38.8 ni fedha ambazo zinadaiwa na watumishi kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa na madeni haya kwa bahati mbaya sana yanatakiwa yalipwe na Serikali Kuu kupitia Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kupitia Bunge lako, Serikali ilipe madeni ya watumishi hawa ili kuongeza tija ya utendaji kazi. Wakati mwingine utendaji kazi na morali ya utendaji kazi inapungua kwa sababu watumishi wa kawaida tu wanadai fedha za likizo, fedha za matibabu na fedha za kukaimu madaraka. Ili kuongeza tija kwa watumishi wetu kwenye mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, tunatoa rai kwamba Serikali Kuu ilipe madeni haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ninapenda kuchangia ni madeni ya wazabuni au wakandarasi. Hili pia limezungumzwa na mtani wangu, jirani yangu Mheshimiwa Kuchauka. Katika mamlaka zetu za Serikali za Mitaa 55 zilizohojiwa na Kamati yetu ya *LAAC,* tunaelezwa kwamba kiasi cha shilingi bilioni 14.2 zinadaiwa na wakandarasi na hizi pia zinatoka Serikali Kuu. Serikali Kuu ichukue hatua ya kupeleka fedha kwenye halmashauri hizi ili wakandarasi wetu hawa, tena bahati nzuri wengi wao ni wakandarasi wazalendo wa ndani, waweze kulipwa madeni haya na waweze kupata moyo wa kuendelea kufanya kazi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ambalo ninapenda kuchangia ni kutopelekwa kwa fedha za miradi ya maendeleo ile 40% na 60% inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri zetu. Kwa bahati mbaya sana, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam peke yake Ilala inadaiwa shilingi bilioni 21 ambazo hazijapelekwa kutekeleza miradi ya ndani, miradi ya maendeleo ambazo ni fedha za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni halmashauri yako na tunaomba kupitia Bunge hili fedha hizi za miradi ya maendeleo zinazotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam zipelekwe ili zikajenge barabara, zikaimarishe vituo vya afya na zahanati, zikaimarishe madarasa na vyoo katika shule zetu za msingi na sekondari na maeneo mengine ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba niunge mkono Hoja za Kamati zote tatu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge kwa taarifa yako, hatua zimechukuliwa kwa wazembe wote na wameshaondolewa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, ajiandae Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii nami nichangie. Kwanza naanza kwa kuunga mkono hoja za Kamati zote tatu zilizowasilishwa na kuwapongeza sana viongozi wa Kamati hizo; kazi waliyofanya ni nzuri na imetusaidia. Pia, nampongeza CAG kwa kazi kubwa na nzuri aliyowekwa kama jicho la Serikali, kwa kweli ametupa mwanga na kuweza kuona mianya iko wapi na nini kifanyike kwa maana ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze tu kwa swali la kwamba, pengine kuna utaratibu gani ambao Serikali inapaswa kuchukua hasa pale ambapo halmashauri zinakuwa zinakiuka taratibu ambazo zimewekwa makusudi katika suala zima la matumizi ya pesa? Kwa sababu haya malengo yapo na kanuni zipo, lakini tumepata taarifa halmashauri nyingi zimekiuka taratibu za fedha na hasa katika pesa wanazopelekewa za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta wamepokea pesa za maendeleo, lakini zimetumika maeneo mengine tofauti na maendeleo; wakati huo huo pesa za maendeleo wanazopaswa

kutenga hawatengi kulingana na makubaliano yalivyo. Sasa labda tujue pengine Serikali inachukua maamuzi gani katika hayo kwa sababu utekelezaji unakuwa siyo sawa kama ambavyo unatarajiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni maagizo ambayo yanatolewa na Kamati mbalimbali na hasa zinapokuwa katika ziara. Tukizungumzia hizi Kamati tatu, kuna maagizo ambayo zinatoa katika maeneo zinakokwenda, lakini utekelezaji wake hatuuoni katika taarifa ili kuweza kujua wametekelezaje. Je, ni nini kinafuatia hapo? Maana yake inakuwa kama ni ziara za kawaida wanatoa maagizo, wakurugenzi hawatekelezi na hakuna pengine *follow up* inayofanyika katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pengine tujielekeze pia katika kuona kazi kubwa inayofanywa na Kamati zetu na maelekezo, Serikali inasimamiaje katika utekelezaji kwenye hizo halmashauri husika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie kile kitendo cha Mkimbiza Mwenge Kitaifa alipozungumza waliotembelea miradi, naye amekuwa ni jicho la kumsaidia CAG katika kazi aliyofanya. Katika pesa nyingi wanazokusanya za makusanyo ya ndani, hakuna miradi ya vielelezo wanavyoweza kusema kwamba mradi huu umetokana na pesa za ndani, mara zote wanategemea pesa zinazotoka Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine ingekuwa ni hali halisi na muda muafaka sasa wa kuwataka pia katika fedha za ndani tuweze kuwa na miradi ya vielelezo. Kwa sababu kuna halmashauri zinakusanya pesa nyingi sana, lakini pesa zile zinaishia katika matumizi ya kawaida wakisubiri Mfuko Mkuu wa Serikali kuwapelekea pesa hizo. Pengine sasa wakati umefika wa kuzielekeza halmashauri kutumia pesa katika miradi ya maendeleo. Tuweze kuona hali halisi ya mchango wao kwa miradi ya kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine yamezungumzwa, lakini nataka nizungumzie tu suala la ukaimu katika halmashauri zetu. Tumeangalia katika suala zima la ukaimu kwenye halmashauri,

nilikuwa nauliza kujua ni idara ngapi na vitengo vingapi viko katika halmashauri? Unakuta kuna idara tisa na vitengo tisa lakini halmashauri inakuwa na makaimu saba, ina makaimu sita kati ya tisa, hivi tunazitakia mema kweli halmashauri hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine utendaji unazorota kwa sababu tu wale wanaokaimu si kwamba hawana uwezo, lakini kulingana na kuitwa kaimu hata yale maamuzi yao wanatoa katika hali ya kutokujiamini sana. Pengine tungeweza kuona hali halisi kama Mheshimiwa Mbunge mmoja alivyosema, kwamba, tunaangalia tu *qualifications* tungeweza pia kuwapima kwa utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wanaokaimu, wanafanya kazi kwa muda mrefu lakini mwisho wa siku wanaondoka na anayekuja bado pia atataka kujifunza kutoka kwa aliyekuwa pale. Kwa hiyo, lazima pia tuangalie halmashauri hizi ambazo zina upungufu mkubwa wa Wakuu wa Idara nini Serikali inatakiwa kufanya? Serikali iziangalie kwa jicho la huruma, tunazirudisha nyuma kwa sababu ya kukosa watendaji wenye kujiamini katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kutokuwasilishwa kwa mapato yanayotokana na mawakala shilingi bilioni 5.65 ambalo limezungumzwa kwenye ukurasa wa 17. Suala hili nadhani si la kufumbia macho kwa sababu kama wameingia mikataba wamekubaliana, inakuwaje pesa nyingi kama hizo zinakuwa haziwasilishwi? Halafu hatua gani inachukuliwa? Unaweza ukakuta mwaka unapita wakala yuleyule tena ameingia mkataba na halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tuangalie pia upande wa pili ambapo wapo mawakala wengine ambao wanakusanya zaidi na fedha zinazowasilishwa kule haziendi zote kama zinavyotakikana, kwa hiyo pia kuna suala la *collusion* katika maeneo hayo. Tuna uthibitisho mdogo tu kutoka kwa hawa mawakala wengine wanaokusanya pesa, kuna wakala mmoja aliwahi kulalamika kwamba yeye kwa mwezi kakusanya zaidi ya shilingi milioni 20, kuna wale wanaorejeshewa fedha zao asilimia

tano; akarejeshewa asilimia tano za milioni tatu akaanza kuhoji wakamfumba fumba pale, lakini tulielekeza lifanyiwe uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna pande mbili hapa ambazo tunatakiwa kuangalia namna ambavyo mikataba wanaingia na namna ambavyo usimamizi unakuwa. Kwa hiyo kuna mianya mingi fedha zinapotea huko ni vyema Serikali ikatupia jicho ili kuondokana na wala rushwa hawa au kupoteza fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 30 wamezungumzia masuala ya miradi ya kupanga, kupima na kumilikisha. Halmashauri nyingi zinadaiwa na ninaomba ni-*declare interest* tu kwa sababu wengi pia wamechukua kipindi kile cha nyuma ambapo kuna niliowakuta wakati nikiwa Mheshimiwa Waziri wengine wamechukua wakati wangu na wengine wamechukua wakati mwingine, lakini hata wale tuliowakuta mpaka leo hawajarejesha, ni nini kinafanyika pale? Matumizi mengine yanapelekwa na wanauza viwanja halafu wakati mwingine wanauza 100% ya viwanja, lakini pia hawawezi hata kulipa fidia kwa watu wanaodai. Hili nalo lazima tuliangalie miradi hii kama ikiweza kufanya vizuri suala tunalolalamikia la kupanga, kupima na kumilikisha lingekuwa limekwisha.

Mheshimiwa Spika, ninao mfano hai kabisa wilaya yangu, jimbo langu tumebakiza 12% ya kupima ardhi yote ya wilaya kwa sababu tu ya kutumia fedha hizo vizuri na kuzielekeza palepale kwenye ku-*reinvest* kwenye ardhi, lakini tukichukua fedha zinakwenda kuwa *re-invested* kwenye maeneo ambayo siyo ya ardhi tunaua sekta hii migogoro haiwezi kuisha kwa sababu ardhi haijapangwa, haijapimwa, na haijaweza kupangiwa matumizi mazuri. Kwa hiyo, kwa fedha hizi ambazo Wizara inatoa ningeomba sana usimamizi, Kamati iwe kali kabisa katika zile halmashauri ambazo hazijarejesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa ni nyingi sana bilioni 42 wamerudisha bilioni 20.42, bilioni 21 bado hazijarudi, lakini bado wanaendelea kupata pesa zingine. Wakati huohuo kuna pesa ambazo zimekwenda kinyume na matumizi milioni 327 zimekwenda nje ya utaratibu na wakati huo huo wanapoandika

miradi yao wanakuwa wameainisha watatumiaje na kama kuna madeni wanaenda kulipaje hasa yale ya utwaaji wa ardhi napo bado wanadaiwa. Unawezaje kudaiwa hadi kwenye fidia wakati andiko lako ulisema utalipa kwanza kabla. Wakipewa fedha haiendi moja kwa moja kunapohusika. Ningeomba Kamati iendelee kusimamia na Serikali pia ione hili ni jambo la msingi ambalo linakwenda kuondoa migogoro mingi. Kuna halmashauri ambazo zimekuwa sugu katika urejeshaji ni vizuri pia zikaangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la *PIC* wamezungumzia suala la mashirika pengine kutokuwa na mitaji ya kuweza kujiendesha lakini tuangalie malengo yao. Kwa mfano ya *TIB* wakati inaanzishwa ni wazi shirika hili lilianzishwa kutoka *TIB-corporate* na lilirithi madeni. Sasa kama limerithi madeni linajikuta pia halifanyi kazi nzuri, lakini Serikali kwa maana *BOT* pia nayo wana malengo ya mitaji kwamba ni bilioni 200 ndiyo shirika linaweza likajiendesha, lakini mpaka leo wana bilioni 88 na *point*. Tunatarajia nini pale? Mwisho wa siku tutakuta limewekwa chini ya uangalizi wa *BOT* lakini kuanzishwa kwa *TIB* kulikuwa na malengo makubwa ya kuweza kuongeza mitaji katika taasisi zingine za kimaendeleo. Sasa kama lengo halifikiwi halafu shirika lenyewe pia mtaji unakuwa pungufu Serikali itupie jicho katika maeneo hayo kwa sababu malengo yake ni makubwa katika kuweza kuwekeza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme, wamezungumza wenzangu, kadiri unavyoongeza uwigo wa kuunganisha umeme ndivyo jinsi unakuwa na uhakika wa fedha kwa Serikali kwa maana kupitia zile *tariffs* zao katika kulipa umeme kama alivyozungumza Mheshimiwa Ngassa. Tuone tu namna ya kuweka *flat rate* katika kuunganisha, tusiangalie zaidi kupata faida katika kuunganisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haina maana umeme unapita mtu na hajafikiwa, tuweke *rate* ya kufanana, watu wengi wahudumiwe na fedha nyingi Serikali itakusanya kutokana na matumizi ya umeme. Tuchukulie umeme kama kitu ambacho ni *necessary* ni muhimu na siyo *luxury* kwa maana ya anasa hapana. Tulikichukulia kama ni muhimu tukagawa umeme kwa wote wakalipia *flat rate* bado tutakusanya fedha kwa namna ya

matumizi yanavyotumia kwa hili nalo ni jambo la msingi ambalo tunatakiwa kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze sana *CAG* kwa maana ya hali halisi ya mashirika yalipofikia. Kati ya halmashauri 184, halmashauri 181 zinaonekana zimefanya vizuri ni tatu ambazo hazipo vizuri na ukiangalia hapa zimeongezeka zinazofanya vizuri kutoka 170 mpaka 181. Maana yake ni kwamba sasa kuna hali halisi inayokwenda vizuri katika suala la usimamizi kinachotakiwa pale ni kuongeza nguvu na kasi ya usimamizi hasa katika zile hoja zinazojirudia rudia kwa sababu unakuta halmashauri moja ina hoja ya kujirudia, kila mwaka ile hoja haifutiki, sasa kwa nini hoja isifutike kama kuna umakini katika kusimamia? Kwa hiyo, ningeomba hili nalo liendelee kusimamiwa kwa sababu ni jambo ambalo linakwenda kinyume na taratibu za matumizi ya fedha, lakini kinyume na maelekezo ya taarifa zinazotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la utekelezaji wa makusanyo kwenye hizihizi halmashauri, halmashauri ilijiwekea malengo ya kukusanya bilioni 911, imekusanya bilioni 912 maana yake wamekwenda zaidi kwenye 28%, lakini malengo haya yamefikiwa na kuvukwa, lakini kwenye matumizi kunakwenda ndivyo sivyo. Kwa hiyo kuna namna ambavyo pia tunahitaji kusimamia na namna ya kufuatilia kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala zima la gharama za mitaji hasa kwenye masuala ya mashirika kama *TTCL, MSD* pamoja na *NARCO* ambayo yapo na yanaweza kuzalisha lakini hayazalishi kulingana na utaratibu ulivyo haya yanatakiwa kutupiwa jicho. Tuangalie malengo ya kuanzishwa kwa mashirika haya na kama yanatakiwa kujisimamia na kujiendesha inakuwaje hayajiendeshi lazima pale kutakuwa na changamoto *either* usimamizi wa *management* au bodi zenyewe si kali katika kusimamia na kuweza kuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuangalie wapi wanakwama kama rasilimali ilipo. Unakuta maeneo mengi *NARCO* wanakodisha hawawezi pia hata kuwa na *ranch* za mifano mikubwa ambazo zinaweza kuwa mahali pa kujifunza.

Kwa hiyo nadhani hilo nalo ni jambo la msingi ambalo tunatakiwa kuliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la *NHIF* hasa kwa upande wa Benjamin Mkapa, ninaomba tuone namna bora ya kuweza kuwasaidia kwa sababu walitoa huduma. Kwenye upungufu wa elimu ninadhani wanatakiwa kuelimishwa ili waweze kuona jinsi gani wanaweza waka-*recoup* hela yao kwa sababu wameshatumia rasilimali zao, dawa wameshatoa halafu usipowarejeshea kabisa napo pia kunakuwa na tatizo. Kwa hiyo kuna haja ya kuona namna bora ya kuelimisha kwenye upande wa *NHIF* katika maeneo yote ili wanapojaza zile fomu na namna ya matumizi, basi walau kwenye mwongozo uweze kwenda sawa na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema hawa hawalipwi kwa sababu tu walikosea, mwisho wa siku tutajikuta pia hiyo *NHIF* inakuwa haina maana kwa sababu kama mtu anakwenda pale ataambiwa atoe *cash* kwa sababu akienda na kadi yake hawarejeshewi pesa yao maana yake nao watashindwa kuitumia. Niombe sana hiyo nayo iangaliwe kwa sababu inaweza ikaleta changamoto kwa sisi watumiaji na watu wengine wanaotumia ambayo ikaonekana kwamba wameshindwa kulipwa gharama zao.

Mheshimiwa Baibu Spika, nimalizie kwa suala moja ambalo nataka kuliongelea kama muda unaruhusu kwenye suala zima la madeni ya Serikali ambayo yapo. Ukiangalia Madeni ya Serikali, Serikali ikipiga kelele kidogo katika kubana zile taasisi malipo yanalipwa, lakini kwa nini ule ukali wanaouonesha kwa watu binafsi wasioneshe kwenye mashirika? Mtu binafsi ukichelewa kulipa kesho unakatiwa maji, lakini taasisi za Serikali unakuta Magereza wanadaiwa, Polisi wanadaiwa, lakini ukija kwenye *DUWASA* inadai zaidi huku, *TANESCO* na *TPDC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mambo hayaendi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, hayupo. Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii ya Taarifa tatu ambayo ni Taarifa ya *CAG* ambayo ina *component* ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, lakini kuna Taarifa ya hesabu yaliyokaguliwa ya Serikali za Mitaa na vilevile Taarifa ya hesabu yaliyokaguliwa ya Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa letu la Tanzania. Sisi sote ni mashahidi na kule kwenye Manyoni Mashariki kuna kazi nyingi sana ambazo zimefanyika ndani ya hii miaka minne, kwa hiyo sisi tunamuahidi kumlipa mwakani

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na maeneo manne ya kuchangia leo; eneo la kwanza nitachangia kwenye hoja ya benki yetu ya uwekezaji yaani *Tanzania Investment Bank (TIB,)* lakini vilevile nitachangia kwenye hoja ya Bodi ya Mikopo Tanzania hususan ile ya elimu ya juu na muda ukiniruhusu nitachangia kuhusu ile miradi miwili ambayo ipo chini ya Wizara ya Fedha na *TANROADS* ya ukaguzi wa pamoja wa magari ule Mradi wa Nyakanazi – Bukoba, lakini tuna mradi kama huo huo ambao upo pale Manyoni kwenye Kata ya Muhalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme katika hoja ya Benki ya *TIB* ametangulia kusema Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula hapa, nadhani nia ya Serikali ya kuanzisha Benki ya *TIB* ilikuwa ni nia njema tukizingatia kwamba Mheshimiwa Rais sasa hivi ameweka nguvu kubwa na *focus* kubwa kwenye uwekezaji kwa hiyo tulitegemea sasa hata Serikali iweke nguvu kubwa katika kuiwezesha Benki ya *TIB*, lakini taarifa zilizoletwa kwenye Kamati zetu hususan kwenye Kamati yangu ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kifupi niseme Benki ya *TIB* inapumulia mashine. Inapumulia mashine kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sasa hivi ipo chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania *BOT*. *BOT* huwa inatoa miongozo ili hizi benki za kibiashara *(commercial banks)* ziweze ku-*operate* lazima *bank* iwe ina *minimum capital* ya bilioni 200, lakini *TIB* sasa imekuwa kwa muda mrefu ina-*operate in less than 200 billion* kwa mwaka ambayo ni *risk* kubwa lakini imekuwa *mistrusted* na wateja lakini vilevile hata ile azma ya Serikali ya kwamba tuwasaidie wawekezaji wa ndani nadhani inaenda kufeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni muda muafaka sasa jicho la Serikali likaangalie jinsi gani tutaisaidia benki yetu ya uwekezaji. Sote ni mashahidi, tuna wafanyabiashara wengi, wakandarasi wengi...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya kuna Taarifa

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpa Taarifa mchangiaji *Doctor* kwa mchango wake mzuri kwamba Serikali kwa miaka mingi mfululizo ilishaji-*commit* kila mwaka kuipatia hii benki shilingi bilioni 100. Kwa hiyo wao ndiyo wameitelekeza lakini na *Hansards* zipo, ilisha-*commit* kila mwaka kuipatia hii Benki shilingi bilioni 100 ili iweze kufanya kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa hiyo Taarifa. Kama nilivyotangulia kusema kwamba hii ni benki muhimu ukizingatia kwamba sasa hivi nguvu kubwa ya Serikali na Mheshimiwa Rais ni kuvutia wawekezaji. Katika azma ya kuvutia wawekezaji tunahitaji kuhakikisha kwamba benki yetu tunailea, lakini katika kuilea tunahitaji kuangalia kwamba sasa inapewa mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamechangia hapa kwamba ile *commitment* ambayo Serikali iliitoa kuhakikisha kwamba benki yetu inaenda kusimama ili wakandarasi

mbalimbali ambao wanaenda kukopa kwenye hizi *commercial banks* waweze kukopa kwenye benki yetu. Vilevile kuwa na benki za Serikali ambazo ikitokea *any financial risk* au *shock* zinaweza zikasaidia Serikali inahitaji kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ushauri wangu ni kwamba kama ambayo Serikali imetoa *commitment* hii, sasa tuiombe Serikali naWizara ya Fedha tuiangalie hii benki ili tuweze kuhakikisha kwamba sasa inaenda kusimama ili iweze kusaidia wawekezaji wetu mbalimbali wa ndani na wa nje, lakini hususan wakandarasi ambao wamekuwa waki-*struggle* kupata mikopo kwa ajili ya kuendeleza hizi shughuli za miradi hususan miradi ya *TANESCO*, miradi ya maji hata miradi ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunatambua kwamba *BOT* inailea hii benki na nadhani ni azma ya Serikali sasa kuhakikisha kwamba Benki yetu ya *TIB* inakwenda kufanya kazi vizuri. Kwa hiyo, nia yetu ni kuhakikisha kwamba sasa inaenda kuisaidia hii Benki yetu ya *TIB* ili wale wawekezaji wa Tanzania waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Sisi sote ni mashahidi kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais ndani ya hii miaka miwili idadi kubwa sana ya watoto wanaotoka katika familia maskini wameweza kupata mikopo. Wote ni mashahidi Mheshimiwa Rais ameweza ku-*pump* hela nyingi zikaingia bodi ya mikopo kiasi kwamba tumeweza kupunguza sana *pressure* ya watoto ambao walikuwa wanakosa hela ya kusoma katika elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi mwaka jana na mwaka huu Mheshimiwa Rais aliruhusu fedha ya mkopo iende katika hata katika vyuo vya kati kwa watoto wale ambao wanaenda kusoma masuala ya ufundi. Haya ni mabadiliko makubwa na lazima tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakini mimi nina hoja hapa kuhusu Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia nchi za mwenzetu wameshahama kutoka kwenye Bodi kuja kwenye Mfuko wa Ufadhili wa Elimu ya Juu. Hoja yangu ni nini hapa? Kwa mfano

mwaka huu hata mwaka jana tumeweza kutoa mikopo kwa 70% ya waombaji, 30% hawakuweza kupata mikopo, hii 30% ni vijana ambao wanatoka vijijini. Nia ya Serikali ni nzuri kuhakikisha kwamba watoto wote wanaweza kupata mikopo, lakini tunatambua kwamba Serikali ina *commitment* nyingi, lakini lingine ni kwamba kuwa ile Bodi inakuwa haina ile *autonomy* ya kuweza kuhakikisha kwamba inaweza ikasimama yenyewe na ikahakikisha inatafuta vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, tunategemea chanzo kimoja cha Serikali ruzuku kutoka Serikalini na zile fedha ambazo zinakusanywa ambazo kimsingi hazitoshelezi kufikia *demand* ya watoto hususan wale wanaotoka katika familia duni. Ushauri wangu ni nini hapa? Kama nchi nyingine ambazo zinafanya ningeshauri sasa tui-*transform* hii Bodi ya Mikopo kutoka Bodi tuunde Mfuko wa Ufadhili wa Wanafunzi wa Elimu ya Juu na faida zake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya kwanza ni kuwa na uhuru wa kuwekeza yenyewe ita-*generate profit, profit* ita-*revolve* itaenda kusaidia wale watoto wengine. Pili, itapunguza utegemezi kwenye Serikali kwamba 100% hela zote ambazo zinaenda kwa watoto wetu zinatoka kwenye bodi ya mikopo. Tatu kuna *options* nyingi za ku-*invest* wakishakuwa Mfuko wanaweza wakaamua ku-*invest* hata katika *treasury bonds,* wanaweza waka-*invest* kwenye *real estate* lakini vilevile wanaweza wakajenga hata zile *hostel* ambazo watoto ambao wanafadhiliwa na huu Mfuko maana yake wataenda kukaa kwenye zile *hostel.* Hili ni eneo ambalo kimsingi linahitaji mabadiliko ya kisheria na kwa hili niishauri sasa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ifanye mapitio ya sheria ya uundaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, lengo ni kuhakikisha kwamba sasa tuje na sheria ambayo itaenda kutengeneza huu Mfuko wa Ufadhili kwa ajili ya Elimu ya Juu. Nyingine ni kwamba itasaidia kuipa uwezo huu Mfuko kuweza kusimamia suala la uwekezaji, lakini watakuwa na *options* mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo niliomba nichangie leo ni kuhusu ule mradi wangu ambao upo Manyoni Mradi wa Ukaguzi wa Magari wa Pamoja, lakini huu mradi vilevile upo Nyakanazi Mkoani Kagera (Bukoba). Huu mradi ulisimama 2016/2017/2018 na kwa Manyoni ulishafikia 60%, lakini kwa Nyakanazi ulishafikia 50%. Huu mradi ulikuwa ulikuwa unafadhiliwa na Serikali ya *EU* ambayo ni *grant,* lakini taarifa iliyokuja kwenye Kamati ni kwamba kulikuwa kuna shida kidogo kwenye suala la mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niiombe Serikali huu mradi una tija mbili kubwa sana. Kwanza kuwepo na vile vituo vya ukaguzi wa magari vinaenda kusaidia kulinda barabara zetu. Ninyi nyote ni mashahidi kwamba magari haya yanapotoka Dar es Salaam kwenda kwa mfano nchi nyingine yanapita kwenye barabara yetu kuu panapokuwa hakuna vituo vya ukaguzi kimsingi inakuwa ni hatari sana kwa ajili ya barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi wakati *design* ya hii miradi inaanza lengo kubwa lilikuwa ni kuwa na *one stop centre* ambayo kutakuwa na huduma mbalimbali sehemu moja. Kwa mfano pale Muhalala Manyoni kile kituo kikijengwa pale kutakuwa na watu wa *TRA*, kutakuwa na Stesheni ya Polisi, watu wa Uhamiaji na wengine ili kuhakikisha kwamba sasa tunalinda hata ukusanyaji wa mapato kwa kupitia magari ambayo yanasafirisha mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niiombe na niishauri Serikali huu mradi ni wa muhimu sana kwa Taifa letu, lakini vilevile kama nilivyosema utakuza ukusanyaji wa mapato kwa *TRA,* lakini ni mradi umeshakaa muda mrefu. Kwa mfano pale Muhalala ukipita sasa hivi tayari mradi umeshaanza kubadilika hata sura. Niiombe Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi waangalie kwa jicho lingine huu mradi ambao kimsingi unaweza ukawa una tija kubwa sana na tayari umeshafika 60% kwa Manyoni, lakini vilevile kwa Nyakanazi ulishafika zaidi ya 50%. Niiombe Serikali iende ikahuishe ule mradi ili basi tuweze kuona tija ya ule mradi kwa maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la ukusanyaji wa mapato kwenye Serikali za Mitaa. Taarifa ya *LAAC* imesema hapa kwamba halmashauri nyingi mlifanya vizuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana, lakini niipongeze Kamati na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha jioni tutaanza na Mheshimiwa Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Askofu Gwajima, Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, Mheshimiwa Nancy Nyalusi, Mheshimiwa Priscus Tarimo na Mheshimiwa Anatropia Theonest.

Ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023;**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa Kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na 11 Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023; na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na michango kwenye taarifa zetu tatu za Kamati. Sasa nimwite Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay na Mheshimiwa Festo Sanga, ajiandae.

**MHE. SAMWELI S. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nipate kuchangia kwenye taarifa za Kamati zetu tatu, *PAC, PIC* na *LAAC*. Kwanza nianze kuzipongeza Kamati zetu kwa uchambuzi mzuri ambao wameufanya kwa niaba ya Bunge, kwa jinsi ambavyo wamewasilisha na kwa ufafanuzi ambao baadhi ya wajumbe wameufanya baada ya taarifa hizi kuwasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kwenye eneo la taasisi ambazo Serikali au tuseme makampuni na mashirika ambayo Serikali imewekeza na ina hisa huko na nianze na zile taasisi ambazo Serikali ina hisa chache. Kwenye eneo hili nipongeze kwa sababu, gawio limeendelea kuongezeka na Serikali imeendelea kupata fedha kutokana na uwekezaji ambao imeufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa Serikali kwenye haya mashirika au hizi taasisi ni takriban shilingi trilioni 2.56, lakini imekuwa ikipata gawio. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali imepata shilingi trilioni 231.1 hizi ni fedha nyingi na zinaenda kusaidia maendeleo yetu kwenye maeneo ya

madarasa, kwenye zahanati zetu, kwenye vituo vya afya na huduma zingine za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili nitoe angalizo kwa sababu, mashirika yanayotoa gawio kati ya 56 ni mashirika 15 tu, mashirika 41 hayatoi gawio. Eneo hili Serikali iliangalie na kufanya uchambuzi wa kina ni kwa nini mashirika hayo 41 hayatoi gawio kwa Serikali kwani Serikali imewekeza huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ni mashirika ambayo Serikali ina hisa nyingi. Kwenye eneo hili kuna changamoto kubwa kwani katika mashirika mengi Serikali imewekeza fedha nyingi zaidi ya shilingi trilioni 76, lakini gawio linalotolewa ni kwenye wastani wa shilingi bilioni 100. Hii ni fedha kidogo ukiangalia fedha iliyowekezwa na ukilinganisha na ile ya kwanza ambayo nimesema utagundua kwamba, Serikali imewekeza fedha nyingi, lakini kipato unachokipata kwenye mashirika haya ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika mengine ambayo yameainishwa hayafanyi vizuri sana, ambapo nikiangalia kwa jinsi ambavyo *nature* yake ilivyo. Nichukue mfano wa Shirika letu la Simu, *TTCL;* Kampuni za Simu kwa hapa kwetu Tanzania ukiangalia shughuli zinazofanyika unaona matangazo ya kampuni za simu ni mengi na biashara yoyote ili uweze kufanya, biashara ni matangazo. Bila matangazo hakuna chochote kinachoweza kufanyika na biashara yako watu hawawezi kuijua, lakini unavyoambiwa *TTCL* imepata hasara au inafanya vibaya kwa miaka mitatu mfululizo maana yake ni hatujatumia fursa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TTCL,* nimewahi kusema hapa, sasa tuangalie namna ya kuliboresha kama inawezekana. Kampuni nyingine zinazofanya kazi inayofanana zinafanya vizuri, ni lazima watu ambao wanatufanyia kazi *TTCL* wajitafakari kama wanafanya kazi iliyo sawasawa. Sisi Wabunge ni mashahidi, ukienda huko mtaani huoni tangazo lolote la *TTCL*, ukienda kwa wale vijana wanaotembea na *line* za simu, *line* ya *voda* unaipata papo kwa papo, *Airtel, Tigo*, lakini za *TTCL* kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana *line* ya *fiber,* ukiomba huduma ya kuunganishiwa *fiber* kuna urasimu mwingi. Ni fursa ambayo wao wanayo mashirika mengine hawana, *T-Pesa* huwezi kuiona popote. Kampuni nyingine zinafanya vizuri halafu unaambiwa hili shirika letu linafanya vibaya. Lazima tufanye uchambuzi wa kina tatizo liko sehemu gani na Serikali ikubali kuchambua kama kuna tatizo la msingi la kimuundo lirekebishwe, kama kuna jambo la kisheria nalo lirekebishwe, ili hatimaye Shirika kama *TTCL* liweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mashirika mengine kama *TTCL* ambayo yanafanya vibaya. Eneo moja ambalo naishauri Serikali ni kampuni, mashirika au taasisi zetu tunazotarajia zifanye biashara, Serikali ipunguze mkono, kwamba, tunatarajia tupate wafanyakazi ambao wapo *competent* na watu *competent* wanashindaniwa. Shirika la Serikali ambalo linafanya biashara lenyewe mpaka liombe kibali cha kuajiri Ofisi ya Rais, Utumishi, huyo mtumishi bado atakuwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri jana Mheshimiwa Kunambi alishauri, watumishi waliopo kwenye mashirika yetu haya yanayofanya biashara, watengenezewe utaratibu mahsusi wa kupimwa utendaji kazi wao. Sio kwamba, tu mtu umepata kazi ya Serikali, basi kustaafu kwako miaka 60, ukifanya hivyo ufanisi utakuwa ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi Mheshimiwa Ngasa amesema, ukiruhusu hilo ndiyo utakuwa na wafanyakazi wale wanaoingia asubuhi kazini, atazurura mpaka saa 9.00, anaenda nyumbani. Hakuna chochote alichosogeza wakati wewe unatarajia angalau tupate faida kwenye shirika ambalo analifanyia kazi au shirika analolisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa tuanze kuwapima na tutengeneze vigezo mahsusi kwa wafanyakazi wa mashirika au taasisi zetu zinazofanya biashara ili hatimaye tija iwepo. Ukiangalia mashirika ya umma, taasisi za umma, ndizo zina wafanyakazi wengi kuliko mashirika binafsi, lakini sekta binafsi kwa watu wachache inafanya vizuri sana kuliko sekta ya umma, hapo

lazima kuna tatizo. Lazima tuangalie kama tunataka tuendelee kuwekeza na kupata tija ambayo tunaitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kugusa eneo hilo, nami nichangie kidogo eneo la umeme, hasa kwenye vijiji miji. Sisi ni Wabunge, toka mimi nimekuwa Mbunge sijapata kuona vigezo vya eneo fulani kuitwa kijiji mji, lakini tunafahamu kwa mujibu wa sheria, vijiji vinajulikana, miji inajulikana, unavyosema sehemu fulani imekuwa sasa ni kijiji mji ni kigezo gani kinachotumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini tunawakwamisha wananchi kupata maendeleo kwa kuwacheleweshea umeme au kuwacheleweshea huduma ambayo ingewasaidia kufanya shughuli zao za maendeleo kwa sababu umeme unachangamsha shughuli za wananchi. Kama tunataka maendeleo, umeme ni chachu ya maendeleo, tupeleke umeme kwa masharti nafuu na hatimaye fedha hizo tuzikusanye kutokana na ankara ambazo wananchi wetu au wateja wanalipa. Fedha zitapatikana kwenye uwekezaji ukishapeleka umeme. Haiwezekani maeneo mengine tunapeleka umeme kwa shilingi 27,000, halafu maeneo mengine shilingi 320,000, Watanzania ni hawa hawa, uwezo haujatofautiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nigusie ni *Tanzania Investment Bank,* ni benki muhimu, kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania kiuchumi. Unasikia tu kwenye miradi mingi inayotekelezwa, wakandarasi wa Kitanzania utaambiwa wao hawana uwezo wa kufanya mradi fulani; tumesomesha, watu tunao, wana kampuni, lakini kwa sababu, mitaji ni kidogo unakuta kazi nyingine hawawezi kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiiwezesha *TIB* Watanzania wanaweza kupata mikopo ya gharama nafuu hatimaye wakafanya kazi kubwa za ujenzi kwenye nchi yetu, wakashiriki kwenye ujenzi wa nchi yao. Hatuna namna na hatuna uchaguzi, benki tumeianzisha, tulikuwa na malengo mazuri, lazima tuweke fedha, ili tuwasaidie Watanzania kupata mtaji katika kufanya shughuli ya kuchangamsha uchumi wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania itajengwa na Watanzania kwa kuwezeshwa na nchi yao, Tanzania haiwezi kujengwa na wageni. Lazima tuone namna ya kuwasaidia Watanzania kwenye eneo hili na namna ya kuwasaidia ni kuwapatia mitaji watu ambao tayari wameshaonesha jitihada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya mwisho ambayo nataka niongelee ni kwenye eneo la mikopo ya 4:4:2, kwa maana ya asilimia nne kwa akinamama, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa wenye ulemavu. Kamati imechambua vizuri, kuna baadhi ya halmashauri zinafanya vizuri, lakini nyingine zina changamoto. Niwapongeze Madiwani wenzangu wa Halmashauri ya Wilaya ya Hangang' kwani tumekuwa tukitenga fedha, kwa ajili ya akinamama, vijana na watu wenye ulemavu na nimpongeze mkurugenzi wetu kwani, hivi karibuni ametangaza shilingi bilioni moja, ili ikakopwe na akinamama, vijana na watu wenye ulemavu ili hatimaye wajiletee maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili tumekuwa na miradi ile ambayo tunaongea kwenye mfumo wetu wa *NeST*. Kama mfumo huu una changamoto zile fedha zikienda kwenye makundi yetu kuna shughuli nyingi za ujenzi na vijana wengi tumewasomesha kwenye masuala ya ujenzi, masuala ya umeme na vitu kama hivyo. Hizi fedha zikienda upande huo, watu hawa wakapewa miradi na wao wakapata fedha zao kwa haraka, tutazungusha fedha na mikopo italipwa na watu watabaki na fedha. Tutachangamsha uchumi wa vijana, tutachangamsha uchumi wa akinamama na walemavu nao watapata uchumi. Eneo hili ni muhimu. ninaomba tuangalie kwa kina, ili tuhakikishe kwamba, malengo yale ya kuwawezesha wananchi wetu yanafikiwa kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa nafasi. Ninaunga mkono hoja zetu zote tatu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng.* Hhayuma. Sasa nimwite Mheshimiwa Zacharia Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Askofu Gwajima, ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Kwanza niungane na wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu wa Rehema aliyetujalia wasaa huu, afya njema na baraka kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze Serikali kwa kazi kubwa inayoifanya, hasa katika Jimbo langu la Mbulu Mjini na maeneo mengine nchini. Kazi kubwa imefanyika na pia, nizipongeze Kamati zetu zote tatu kwa taarifa zao walizowasilisha hapa zikiwa zimeelezea kwa kina kwa kadri ambavyo taarifa ilivyo na uhalisia wake katika shughuli mbalimbali za mashirika hayo pamoja na halmashauri zetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimpongeze *CAG* kwa kazi kubwa. Amefanya kazi kubwa sana na mpaka anapotuletea taarifa hii *CAG* amepita maeneo mengi, ametoa taarifa nyingi amewadokeza wahusika ili waweze kuthibitisha mbele yake uhalisia wa hoja ambazo zimejitokeza kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, pia nizungumzie eneo lake, *CAG*, kwa kadri anavyofanya kazi. Tungeiomba sana Serikali iwe na muundo unaotoka Taifa, Mkoa na kwenye halmashauri zetu. Kwa nini nasema hivi? Ni jambo gumu sana wakaguzi wa ndani kufanya kazi ya ukaguzi kwa kutegemea menejimenti ya halmashauri akiwemo mkurugenzi na watendaji wengine kwa maana ya vitendea kazi, uwezo wa kifedha na pia, mazingira ya utendaji kazi. Kwa hiyo, nashauri kama inawezekana Serikali itoe kipaumbele, hasa kwa bajeti inayokuja, kuwajengea uwezo wale wakaguzi wa ndani wawe ni idara inayojitegemea ambayo iko nje ya halmashauri kuliko sasa ilivyo kwa sababu, hawawezi kuwa na kauli wala uwezo wa kutenda kazi na kufuata maadili ya kazi yao kwa sababu, uwezeshaji na mazingira ya kufanya kazi yana muambata na halmashauri zetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja kubwa sana ya Serikali kutazama jambo hili, ili kuona kwamba, walau wakaguzi wa ndani wanakuwa chini ya Mkaguzi Mkuu na muundo wao unajitegemea, ili kuweza kufanya kazi zenye tija. Hoja hizi tunaamini zitapungua sana kwa upande wa

halmashauri, nikizungumza kwa maana ya pale halmashauri utendaji kazi wao unamtegemea zaidi mkurugenzi, lakini inawezekana baadhi ya halmashauri na mapungufu yale yanamgusa moja kwa moja Mkurugenzi kama Mweka Hazina Mkuu. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali itazame eneo hili kwa namna inavyowezekana, ili walau kwa namna ya pekee hawa watumishi, wakaguzi wa ndani, wawe na ofisi yao nje ya halmashauri, wawe na magari kama vitendea kazi na watengewe fedha ili waweze kufanya kazi na kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa ya *LAAC* kuna taarifa ya makusanyo ya mwaka 2022/2023 kama ilivyokaguliwa. Kulikuwa na makusanyo ya malengo kwa maana ya bajeti iliyotarajiwa yenye shilingi bilioni 911, pia, kwenye makusanyo halisi kwa mwaka huo ikaonekana wamekusanya shilingi bilioni 912. Eneo hili nina ushauri fulani, kuna makisio madogo yanayowekwa kwenye halmashauri zetu nchini na sisi tunazibariki kwa maana ya, malengo wanaleta wao na mwisho wa siku yale malengo wanajikadiria, halafu katika ule ukasanyaji moja kwa moja unakuta tunasema wamefika asilimia mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Serikali itazame na tutazame upya kwenda nyuma zaidi kwa miaka mitatu halmashauri ipi ilikuwa imekusanya kiwango gani na imeongeza kwa kiasi gani ili kuleta mapato halisia na yenye kukusanyika, lakini yasiwe yanajirudia kwenye yale malengo ambayo mtu anajikadiria na mwisho wa siku yale malengo hayafikii kiwango fulani au hayaongezeki katika mwaka ule wa fedha. Hii itasaidia hii hali ya kusema tumekusanya zaidi ya asilimia mia moja, kumbe tunajikadiria, lakini makadirio hayana uhalisia. Kwa hiyo, tutazame upya badala ya baadaye katika miezi sita au mwaka mmoja wanaomba tena kutanua mafungu kwa sababu eti wanafika zaidi ya asilimia mia moja. Kwa hiyo, hapo kuna haja ya kutazama upya viwango vyetu vya makusanyo, ili walau tuweze kupata makusanyo halisi kwenye halmashauri zetu na mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwenye Taarifa ya *LAAC* ni kwamba, utaratibu wa semina kwa vikundi ni muhimu sana. Tunaipongeza Serikali imepunguza hoja nyingi za ukaguzi, lakini pia, mafanikio yamepatikana kwenye hali halisi ya hati safi

na hati inayoridhisha, hati chafu zimepungua sana, lakini ili kuleta tija, nadhani kuna haja ya semina kwa Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi za Mkaguzi wa Ndani hazipati majawabu na hazipati maamuzi ambayo yanaipa halmashauri tija na pengine wale ambao walikuwa wamesababisha zile hoja kutokuchukuliwa hatua ama kutobadilika haraka kwa sababu, zinaletewa zile taarifa. Mheshimiwa *RC* na timu yake wanakuja, lakini majawabu yanayotolewa ni kama vile hayakazii sana uzito wa kupunguza zile hoja na namna ambavyo zile hoja zinadhibitiwa katika halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hoja inakuja kukaguliwa katika ngazi ile ya hoja za mkaguzi, Baraza ambalo Mheshimiwa *RC* anakuwepo, mkaguzi wa ndani alishahangaika sana kuomba nyaraka, alishahangaika sana zifanyiwe kazi, lakini mwisho wa siku zimeshindikana. Ni kwamba, zile zinaweza kuwa na utata na matatizo ambayo pengine wazalishaji au waliosababisha zile hoja wameshindwa kuziondoa zile hoja kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye mashirika ya umma. Serikali inatoa ruzuku kila mwaka ikitegemea gawio na ufanisi zaidi kwenye haya mashirika. Ninadhani kuna haja ya kutazama vizuri sheria na kanuni zinazosimamia hayo mashirika ikiwemo taratibu za kusimamia watendaji ambao wanateuliwa na wale watumishi, lakini pia, ukiwemo mfumo mzima kwa kutazama na kuona kwamba, walau yale mashirika ya umma wanapopewa ruzuku na wao wanafanikiwa kufikia malengo, lakini pia, kuleta ruzuku Serikalini kwa maana ya gawio kwa sababu, bila gawio utendaji wa mashirika haya utategemea sana kila siku Serikali yetu ipeleke ruzuku ambayo ruzuku hiyo, kama kodi, ingeweza kuhudumia maeneo mengine, ili na wenyewe waweze kupata uwezo mkubwa wa kiuendeshaji na makusanyo katika mapato wanayopangiwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia sana wakati fulani watu wanaogopa, lakini badala ya mtu kuondolewa kwenye ile nafasi, anabaki kwenye ile hali ya kawaida na mshahara unabaki pale pale, tunampeleka tena mtu mwingine, kadri ya miaka

inavyokwenda na kila mwaka tunakuwa tunapeleka fedha za ruzuku lakini mafanikio ya mashirika hayo hayapandi na kuleta tija zaidi katika yale malengo mahsusi ya Serikali, hali hii inaisababisha Serikali ishindwe kufikia malengo yale iliyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali ijielekeze zaidi katika uwekezaji wa miundombinu na uwekezaji wa fursa za kujenga miundombinu, pia na uanzishaji wa miradi ambayo baadaye inatoa kwa sekta binafsi ili iwe mwendeshaji na Serikali ipate hisa (imiliki hisa) badala ya uendeshaji. Picha hii iko kwenye *TTCL*, minara tunayojengewa kwenye maeneo yetu katika sehemu mbalimbali, huwa inashindwa kuhimili ushindani wa minara mingine. Kadri ambavyo unaona wapigakura wako au wananchi wako walio wengi hawako kwenye mtandao ule wa *TTCL* wako kwenye mitandao mingine, lakini sisi tunajenga minara huku hatufanikiwi kupata wateja kwa maana ya uzalishaji uliotarajiwa hatufikiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari yake kubwa hii ni pale ambapo sasa tunawekeza nguvu kubwa, lakini kile tulichotarajia hatukifikii kukipata. Mifano hii ingefanyiwa tathmini na kufanyiwa mapitio ya hali hii ya minara ya *TTCL*, kwa vyovyote Serikali itakubali kutangaza na kuwapa wawekezaji ili waweze kuendesha minara hiyo ili tupate kufanikiwa na isibaki kama minara ambayo wananchi wengi huwa hawanufaiki nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni miradi tuliyoianzisha, kwa mfano miradi ya barabara. Kule kwetu kuna Barabara moja ya Garbabi – Mbulu kilometa 25.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia, muda wako umeisha malizia, *windup.*

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi mengine nitaandika kwa maandishi. Nashukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia. Sasa nimwite Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa nichukue nafasi ya kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote tatu ambazo zimewasilisha hoja zao hapa mezani, wamefanya kazi zao vizuri sana na tuwapongeze wamelitendea haki Bunge na wametusaidia Wabunge kujua mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sana kwenye mashirika ya umma kwa maana ya mashirika yaliyoko ndani ya nchi yetu. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Rais, amekuwa mstari wa mbele sana kwenye kusaidia kusimama haya mashirika ya umma kwa kutoa maelekezo mbalimbali. Pili, nimpongeze Msajili wa Hazina wa sasa ndugu yetu Nehemiah Kyando Mchechu, amefanya kazi kubwa sana na kazi ambayo kwa kweli hadi sasa kwa sisi ambao tunafuatilia utendaji wa mashirika ya umma kwenye Taifa letu, tunaona kabisa akiwa ametutendea haki Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kurejea maneno ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa anazungumza na mashirika ya umma na watendaji wake. Alisema hivi; "Kwenye mageuzi haya, Mchechu na Waziri wa Fedha huwezi ukiona wakisifiwa hata siku moja, siku zote Waziri wa Fedha analaaniwa, kwa hiyo na wewe Mchechu utalaaniwa tu hapa. Nyingine zitakuja *personal* na nyingine zitakuja kikazi, lakini hii ndiyo kazi niliyokupa. Simama na uifanye."

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ya Mheshimiwa Rais ni maneno ya kiujasiri kwamba, unapokwenda kufanya *revolution*, mapinduzi ama *reform,* siyo jambo rahisi ambalo kila mtu anaweza akapendezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye ripoti za Serikali za utendaji wa mashirika ya umma, kuna mambo mengi yameongelewa humu ndani. Hata hivyo, moja ya vitu ambavyo vinasikitisha ni changamoto ambazo zinasababisha utendaji wa mashirika ya umma kuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto ambazo wamezizungumza wanasema ni *nonproductive assets* kwamba

kunakuwepo na kiwango kikubwa cha mitaji ambayo haiwezi kuwa na uzalishaji. Pili, wanazungumza kwamba, mashirika kushindwa kutumia fursa. Pia, wanazungumzia ukosefu wa mitaji na wanaongelea kuhusu suala la hasara, zaidi ya miaka mitatu unakuta shirika linapata hasara. Hizi ni changamoto ambazo mashirika ya umma kwenye Taifa letu yanazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kama Mbunge nina kazi ya kushauri na kwa niaba ya wananchi wa Makete ninaomba nishauri. Kwanza, ili tuwe na mashirika ya umma ambayo yanafanya kazi na yanafanya uzalishaji tunaona faida na yanatoa gawio kwa Serikali, licha ya kwamba siyo mashirika yote ambayo ni *business oriented,* mengine ni mashirika yanayotoa huduma, lakini kwenye suala la ufanisi kwenye Taifa letu, kuna mambo kadhaa lazima tuyaangalie na ninaungana na Kamati kwa yale waliyoyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nashauri ni upatikanaji wa watendaji wa mashirika ya umma kwenye Taifa letu. Mfumo wa upatikanaji wa watendaji, mtendaji ndiyo *engine* ya taasisi (shirika la umma). Kwa sababu gani? Vikao vya Bodi vinaweza vikakaa mara mbili kwa mwaka, lakini karibu mwaka mzima anayeshughulika na shirika ni mtendaji wa shirika husika na watumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naishauri Serikali kwa nia njema tu, tukiangalia jinsi ambavyo ufanisi kwenye mashirika mengine umekuwa ukifanyika. Mathalani, kwenye mataifa mengine yaliyopo karibu kama Rwanda jinsi ambavyo yanapata watendaji kwenye mashirika yao ya umma. Pili, kwa dunia ya sasa jinsi ambavyo watendaji wanapatikana kwenye mashirika ya umma ni lazima kuwe na ushindani *(competitive merit recruitment),* lazima iwepo kwenye mashirika yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano ulio hai, sisi kama Wabunge tumeona *WHO* - Shirika la Afya duniani, ili kupata Mtendaji wa Shirika la Afya Barani Afrika *(Zonal Africa)* waliweka ushindani na ndugu yetu Dkt. Faustine Ndugulile alishinda. Sasa hii maana yake ni nini? Hii inampa mzigo Dkt. Faustine kuhakikisha kwamba anakwenda kuweka kile kitu ambacho alikuwa na

maono yake kwenye kichwa, lakini unapokuwa na watendaji ambao upatikanaji wao muda mwingine wameteuliwa na sikatai sana kwenye uteuzi, lakini ni lazima twende kwa mbadala mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshateua sana hawa watendaji, tumeona *performance* ya mashirika yetu imekuwa katika namna gani, sasa, twende kwenye mlango mwingine kwa makusudi ili tuone ufanisi wao inakuwaje. Kwa kuweka ushindani, tunampata Mkurugenzi wa shirika fulani kwa ku-*compete*, kwa kuangalia *CV*. Tunao Watanzania wengi wana uwezo na uelewa ambao wanaweza kuwa ni msaada mkubwa kwenye Taifa letu na kuhakikisha haya mashirika yanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana kama Taifa, tukiendelea kulifumbia macho tutabaki kwenye sababu. Inawezekanaje kwenye *TTCL* wanasema shirika linasuasua ni kwa sababu limeshindwa kutumia fursa, shirika linashindwa kutumia fursa, una mtendaji ambaye unamtegemea aka-*utilize* fursa zilizopo, lakini sisi tunapewa sababu ndani ya Bunge kwamba wameshindwa kutumia fursa. Hili jambo ni kwamba, kuna umuhimu wa kupata watu ambao ni *expert* wa haya mambo hususan kwenye mashirika ya umma ili mashirika yetu ya umma yawe ni yenye tija na Watanzania ambao ni washindani na wana uwezo wa kusimamia mambo haya, wakaweza kupata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye wenyeviti wa bodi. Nashukuru yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengine wamechangia ni muhimu sana kuangalia wenyeviti wa bodi zetu, *qualification* isiwe kwamba amestaafu akapate sehemu ya kupumzikia, hili haliwezi kuwa ni kitu cha tija sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Bodi ni moja kati ya watu muhimu sana kwenye uendeshaji wa shirika la umma, kwa hiyo ni muhimu sana Wenyeviti wa Bodi muda mwingine wawe ni watu ambao ni *ma-expert* pia kwenye hicho kitu ambacho anaenda kukisimamia. Vilevile, *plus* wajumbe wake wanapatikana katika mazingira yapi? Tuwe na wajumbe ambao wana msaada kwenye shirika.  Siyo sehemu ya kwenda kupata

fursa ya kufanya kazi, lakini pia kwa ajili ya maslahi yao binafsi. Kwa hiyo, ni muhimu sana Wenyeviti wa Bodi wawe ni wenyeviti ambao wana faida kwa Taifa na wana mawazo mbadala kwa ajili ya kuhakikisha kwamba shirika linaendelea na linasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili la Wenyeviti wa Bodi ni muhimu sana pia Msajili wa Hazina ambaye ana dhamana ya kusimamia mashirika ya umma, kujua bodi ipi inakaribia *ku-expire* ili waanze kutafuta wajumbe wengine. Haiwezekani shirika la umma likakaa miaka mitano, kumi halina bodi na ukategemea hilo shirika la umma lilete matunda na tija! Kwa hiyo, ni muhimu sana na mimi kama Mbunge ninalishauri hilo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni lazima kuwepo na *performance contract* kwenye utendaji wa kazi. Mtu ameteuliwa hajapewa *KPI* (zile *indicators* za utendaji kazi), yeye anajifanyia tu kazi anavyojisikia. Ni muhimu sana kukawa na *performance contract,* bwana ukifanya moja, mbili, tatu kwenye shirika hili tunategemea tutaendelea kuwa na wewe, usipofanya tunakuondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani shirika limeleta hasara kwa miaka mitatu na unakuta kwamba bado mtu anaendelea kuwa ni yule yule kwamba ni Mkurugenzi, watumishi wanaendelea kuwa wale wale. Sisi tunaona ni sawa na Taifa linaona ni sawa, kwamba huyu mtu analeta ripoti ya *ku-fail* kwa miaka mitatu na bado anaendelea kusimamia shirika la umma. Kwa hiyo, mimi kama Mbunge ninashauri ni vema sana kuwa na watu ambao wanapewa *performance contract* ya utendaji *(key performance indicators),* ili waweze kutuletea majibu ya kile ambacho tunaona ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani shirika linaambiwa kwamba lina changamoto ya mtaji wakati kuna fursa ya kwenda kukopa. Haiwezekani shirika linapewa ruzuku na Serikali mwaka huu, mwakani na ni shirika la biashara! Linapewa ruzuku kila mwaka na halizalishi faida na sisi tukaona kwamba, ni sawa hawa watu wanaweza kuendelea, hiki siyo kichaka cha kwenda kutengeneza fedha na hiki siyo kichaka cha kwenda kuzamisha

Taifa letu. Tunategemea mashirika ya umma yawe na msaada kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, ninaomba kuwe na *performance contract* kwa watendaji wa mashirika kwenye Taifa letu. Mtu akishindwa awekwe *bench*. Taifa lina watu zaidi ya milioni 62, Taifa lina watu ambao wasomi ni wengi na wanaweza kwenda kufanya kazi na wakalisaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo ninalishauri kwenye mashirika ya umma; haya mashirika ni *independent entity* kwenye Serikali. Pia, hili ningetamani sana niishauri Serikali; Shirika la umma siyo Idara ya Wizara, shirika la umma siyo idara ya taasisi fulani, shirika la umma lazima lenyewe kwanza lisimame *in a full autonomy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazungumza haya? wakurugenzi wa haya mashirika huko, *most of cases* simu za kupewa maelekezo ni nyingi sana. Shirika la umma ni lazima lipate nafasi ya kufanya kazi lenyewe kuliko kupokea maelekezo mengi. Matamko yakiwa mengi kwenye shirika la umma, haliwezi kufanya kazi. Mkurugenzi wa hiyo taasisi lazima atakuwa mwoga tu kwa vyovyote vile. Ninaishauri Serikali kwamba ni muhimu kuwapa nafasi Wakurugenzi wa mashirika ya umma wafanye kazi *in a full autonomy,* pasiwepo na hii *interaction* ya kuingia unafanya hivi. Serikali *iki-deal* na bodi inaweza ikafanikiwa. Kwa maana ya kila siku Mkurugenzi anaacha *ku-deal* na zile *goals* ambazo amejiwekea kwa mwaka, muda wote anapokea maelekezo kutoka kwa huyu, kutoka kwa huyu, hilo shirika haliwezi kukua. Siku zote watu watakuwa wanafanya kazi kwa uwoga kwamba, "nikifanya hivi labda Mheshimiwa Waziri au Serikali itachukua hivi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema taasisi za Serikali zikaangalia jinsi ya *ku-deal* na mashirika ya umma, tuwaache wafanye kazi ili waweze kuwa na fursa ya kujitegemea, lakini pili tuwadai matokeo, siyo kila siku unawaingilia, itakuwa siyo kitu kizuri sana kwa ajili ya utendaji kazi wa haya mashirika ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yalikuwa ya kwangu na ni muhimu sana kwenye mashirika ya umma. Mwisho, nilikuwa na ushauri kwenye mambo machache sana kuhusu suala ambalo amelizungumza *CAG*. *CAG* amezungumza kwenye suala la kodi

zilizoshikiliwa zenye thamani ya zaidi ya trilioni 10 kwenye Mahakama za Rufani. Trilioni 10 ni fedha nyingi sana. Unazungumza trilioni 10 ziko kwenye Mahakama za Rufani ambazo zinafanya hizi kesi zinashindwa kuhukumiwa kwa sababu ya kutofanya uteuzi wa Wajumbe wa bodi na uhaba wa bajeti. Hiyo haiwezi kuwa hoja ukasimama hapa ndani ukaijenga kwamba, kuna trilioni 10 ziko maeneo, lakini tunashindwa kuzichukua kwa sababu kuna changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *in a records* na hizi ni Mahakama za Rufani, ujue kabisa kwamba siyo taswira nzuri kwenye nchi kuona zinazidi kuongezeka kila mwaka. Yaani tumetoka kwenye trilioni tano kwa miaka mitatu, minne iliyopita, leo tunazungumzia trilioni 10 na tunakimbizana na hizi kodi nyingine zilizoko huku wakati tuna uwezo kwenye hizi trilioni 10. *In fact,* inawezekana trilioni 10 zote kwenye Mahakama za Rufani siyo zetu, inawezekana nyingine tukashindwa kesi na wakawa wameshinda wafanyabiashara, lakini inawezekana sisi tukapata hata trilioni tatu, trilioni tano, trilioni sita na zikaweza kulisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali hili jambo ni lazima tulichukulie katika *u-serious* wa hali ya juu sana. Hii sababu ya kukosa kuteua wajumbe, uhaba wa bajeti ya Mahakama ya Rufani, haiwezi kuwa sababu ya msingi ya sisi kushindwa kupambania hizi trilioni 10 zikaenda kusaidia Taifa letu, kwenda kujenga vituo vya afya kule Makete, kwenda kusambaza umeme na kusaidia taasisi nyingine za Serikali. Kwa hiyo, niiombe Serikali ni muhimu sana tuachane na hii biashara, tufanye uteuzi wa wajumbe, lakini pia tutoe fedha kwenye Mahakama ya Rufani haya majalada yaishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini umewahi kuona biashara ina *bureaucracy?* Biashara ikiwa na *bureaucracy* unatengeneza *loophole* ya rushwa. Kwa sababu inawezekana hawa watu unataka uniambie hizi trilioni 10 hapa zimekaa, maana yake tunataka tujenge msingi wa hoja kwamba, kuna watu hawataki kuzifanya hivi kwa sababu wametengeneza huu ni mtego wa kupata fedha mfukoni mwao; "Bwana lete hiki kidogo, fanya hivi." Niwaombe hili dirisha la rushwa lifungwe, Serikali ipate fedha, wafanyabiashara waweze kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea pia kukusanya hizi trilioni 10 zinatuletea *benchmark* mbaya na taswira mbaya kama nchi. Ni muhimu sana Serikali kama mnatusikiliza, hizi sababu ambazo zimeletwa hapa ziweze kufanyiwa kazi na ziweze kutusaidia kwenye Taifa letu tuweze kupata hizi fedha za trilioni 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni ya kwangu na ya mwisho kabisa. Imenisikitisha kwamba, Serikali imekuwa ikisisitiza na Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza kuona mifumo inasomana. Huu mfumo wa *TANCIS* na hivyo ving'amuzi ambavyo wanavifunga kwenye malori, kama ripoti ya CAG inasema zaidi ya lita 1,001,500 za mafuta ambayo yalikuwa yanasafiri kwenda nje ya nchi, haya mafuta yametoka bandarini yakiwa yanaonekana yanasomeka nchi nyingine, halafu kumbe yameishia ndani ya nchi na kuipotezea Serikali kodi ya milioni 929 sawa na bajeti ya Wizara ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is shame* katika utendaji. Ni muhimu sana mifumo ikasomana….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga, malizia.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana mifumo ikasomana. Hii mifumo ikisomana tuachane na hiya mambo. Hii tu ni ile ambayo ameiona *CAG* ambavyo haijaonekana, je, makontena mangapi yanasomeka yanakwenda Zambia, Malawi na yanaishia hapa hapa Tanzania na kodi inakwepwa? Ni lazima tuwe wazalendo kwenye Taifa letu. Hatuna nchi nyingine zaidi ya Tanzania, ni lazima tuipende na watendaji walijue hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga. Sasa Nimwite Mheshimiwa Benaya Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Tarimo na Mheshimiwa Anatropia Theonest, ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa ushauri wangu. Kwanza kabisa nizipongeze hizi Kamati tatu kwa kazi nzuri, najua kazi ilikuwa ngumu, lakini wametuletea taarifa ambayo kwa kweli ukiisoma unaielewa kwa urahisi sana. Kwa hiyo, nawapongeza sana Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya ziara yenye mafanikio makubwa Mkoa wa Ruvuma, alikuja Ruvuma hivi karibuni na miongoni mwa kazi alizozifanya alizindua jengo la Halmashauri yetu ya Mbinga Vijijini. Jengo hili najua ndilo linalotumika na Wakurugenzi na Watendaji kwa ajili ya kufanya kazi. Kwa maana hiyo, kwa sababu watendaji walikuwa wamekaa maeneo tofauti tofauti, pengine ilikuwa rahisi kutengeneza hoja. Sasa wanakaa sehemu moja wakiwa na usimamizi wa mkurugenzi mahali pamoja na najua sasa hoja zitakuwa zinapungua sana. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo matatu ama manne kwenye hii taarifa, hasa ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Katika taarifa hii ukiisoma kwa ujumla wake unaweza ukaipongeza Serikali kwa namna inavyoonekana kwamba, sasa zile hati chafu zimepungua. Unaweza kuona hati chafu zimebaki tatu toka zilivyokuwa kwa mwaka uliotangulia, hivyo kuna ongezeko la hati zinazoridhisha. Vivyo hivyo, unaweza kuona kwa eneo kubwa kwamba, Wakurugenzi wameweza kujibu baadhi ya hoja. Ukiingia ndani ukapitia vile vipengele, unaona hii sifa inayoonekana hapa juu inaanza kufutika, hata hivyo, kwa ujumla wake niipongeze Serikali, hoja nyingi na kwa maeneo mengi yamepungua pungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unaweza kuona kwenye upelekaji wa mapato yaliyokusanywa kwenye benki. Miaka mitatu iliyotangulia kulikuwa na fedha nyingi sana ambazo zilikuwa hazipelekwi, lakini sasa hivi ni shilingi bilioni 6.7 ambayo haikupelekwa. Sasa unaweza kuona haya kwa namna moja ni mafanikio; lakini swali la kujiulliza, ni kwa nini hizi bilioni 6.7 hazikupelekwa ilihali tayari zimekwishakusanywa? Kwa nini

Halmashauri ya Momba haikupeleka milioni 470? Kwa nini Halmashauri ya Kigoma Mji haikupeleka milioni 282? Ni kwa nini Halmashauri ya Msalala haikupeleka zaidi ya milioni 113? Fedha hizi zimekwishakusanywa, zipo, lakini bado watendaji wetu tuliowaamini wafanye hizi kazi hawapeleki hizi fedha

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha ni kwamba baadhi ya hizi hoja na ni nyingi, tayari Bunge lako hili lilipitisha maazimio; sasa kwa nini hatua zisichukuliwe? Kwa hiyo, niiombe sana Serikali kwa sababu hatuwezi kukaa hapa kila leo tunapitisha maazimio halafu utekelezaji wake hautekelezeki, haifurahishi wala haipendezi sana. Niombe waliopewa mamlaka haya wachukue hatua. Kwa sababu mtu alikusanya fedha, kwa nini asipeleke benki? Niombe sana wachukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, kuna fedha zaidi ya bilioni 61 zilitengwa kwenye vitabu vya Wakurugenzi kwa maana ya Halmashauri na watu wamezipangia matumizi, lakini fedha hizi hazikukusanywa; na unaweza ukaona sababu zenyewe wala si za msingi, sababu zingine kwa baadhi ya Halmashauri ni kuridhika tu, kwamba sasa wana chanzo kipya kizuri kinawaletea fedha hizi zingine wanaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maafisa biashara; kwa mfano chanzo cha leseni za vileo, kila leo *grocery* zinafunguliwa, sasa kwa nini zisifunguliwe wasikusanye? Vilevile kuna maduka na vibanda ambavyo halmashauri wamepangisha, watu wamo na wanafanya biashara; na maeneo mengi ya namna hiyo. Kwa nini fedha zisichukuliwe humo? Hoja hii haijaja leo, ilikuwepo mwaka jana, ilikuwepo mwaka juzi na mwaka huu tena ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe sana Serikali tuchukue hatua, chukueni hatua kwa wahusika hawa. Kule kuna watumishi wengi tu ambao wamepewa mamlaka ya kufanya kazi hizi lakini hawafanyi; na ukipata Mkurugenzi legelege ndiyo hawafanyi kabisa. Kwa hiyo, niombe pamoja na Wakurugenzi wawasimamie watendaji wenzao ili wafanye hizi kazi, wakusanye hizi fedha tupunguze mzigo mkubwa kwa Serikali Kuu, tuzikusanye hizi fedha pale kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tumeambiwa tunadaiwa madeni makubwa makubwa, kuna madeni hapa ya bilioni 87 ambayo hayajalipwa. Kama fedha hizi bilioni 61 zingekusanywa na halmashauri tungepunguza madeni, kwa sababu kwenye fedha hizi ziko kweli fedha za Serikali Kuu, lakini vilevile ziko fedha za halmashauri, ziko fedha zaidi ya bilioni 17; kwa sababu nimezitenganisha hapa, nimezitenganisha kwa mtindo kwamba zile za watumishi ziko zinazodaiwa na Serikali Kuu, lakini zipo zile wanazodaiwa halmashauri. Kwenye watumishi halmashauri wanadaiwa shilingi bilioni 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama halmashauri inadaiwa bilioni 17, huko nje kuna bilioni 61 hawajakusanya, wakikusanya hizo bilioni 61 si watalipa haya madeni ya watumishi wao ambao wanawadai, tukiacha yale ya Serikali Kuu? Vivyo hivyo kwa wazabuni, tena hawa kwa kweli wanatia huruma sana. Hasa hawa wazabuni wa pale wanaohudumia chakula na *stationery*, vipato vyao ni vidogovidogo sana. Sasa mtu amekuletea leo chakula, kesho una kikao kingine anakuletea, keshokutwa una kikao kingine anakuletea; halafu mtu huyu anakopa kwenye benki huko, wakati huo huo anatakiwa alipe na riba. Leo hii halmashauri zetu wanadaiwa zaidi ya bilioni 29; halafu kesho wanakwenda kuwaambia tupe chakula tule. Kwa kweli haipendezi niombe sana ndugu zangu waliopewa kazi hizi wawasimamie hawa watu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo lingine ambalo linasikitisha kidogo, ni suala hili la wakuu wa idara kukaimu, tena kwa muda mrefu. Hivi sababu ni nini? Kwa nini wakaimu muda mrefu? Yaani kwa nini tusichukue hatua papo kwa papo? Kwa nini labda mkuu wa idara anakaimu miaka mitano hadi miaka sita? Kama hana sifa si aondolewe ili aletwe mwenye sifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Malaika, ni sisi sisi Watanzania ndio tutakaokalia hivyo viti, kwa hiyo kama yuko Mtanzania pale anafanya kazi kwa miaka miwili, mitatu, minne hadi mitano kwa nini asithibitishwe kuwa mkuu wa idara? Kwa hiyo niombe sana na hili tayari tulikwishaliwekea azimio humu; sasa sijui tufanye nini ilihali sheria iko wazi? Kwa kweli inatia hasira sana, yaani hata kumthibitisha mtu kwamba afanye ile kazi

anayoifanya kila siku kwa miaka mitatu, minne, mitano tunakuwa na kigugumizi. Kama hatoshi aondoke aje mwingine athibitishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nina hasira naomba niishie hapo na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Kapinga. Nimwite Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa ili niweze kuchangia kwenye taarifa hizi za Kamati zetu tatu. Kwa kuanza, niseme ninaunga mkono mawazo yote na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa sababu nimeona wamefanya kazi kubwa kwa niaba yetu. Kwa hiyo mapendekezo ya Kamati zote kwa ujumla, *PIC, LAAC* pamoja na *PAC,* ninayaunga mkono asilimia mia moja na niwapongeze sana Wenyeviti wa Kamati, Makamu Wenyeviti, Makatibu pamoja na Wajumbe wa Kamati zote; wamefanya kazi kubwa kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwa ujumla wake utakwenda kwenye ushauri, yaani naongezea kwenye yale mapendekezo ambayo Kamati zimetoa; na nitatumia mifano ambayo mingi wenzangu wamekwishaigusia na mingine mingi nitaileta mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ripoti ile ya *PIC* nianze kwenye lile eneo la kampuni, mashirika na taasisi ambazo hazifanyi vizuri. Nilikwishawahi tena kuchangia kwa mwelekeo huu ambao ninauleta leo, kwamba cha kwanza tuhakikishe kuwa watu wanaokwenda kusimamia katika mashirika haya na katika *organizations* hizi kuwa ni wabobevu kwenye taaluma inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano Kiwanda cha Ngozi pale Moshi, Karanga *International Leather Industries Limited.* Inatakiwa anayekwenda kuwa mkurugenzi mkuu pale awe mbobevu kabisa wa masuala ya Ngozi, masuala ya *production*

na masuala ya *marketing* awe anafahamu. Huwezi hata siku moja ukamchukua mtu ambaye hakuwahi kuuza hata mafuta ya taa, hakuwahi kuuza hata kwa kubadilishana hata kitu chake binafsi kilichochakaa unampa kiwanda kikubwa kiingie kwenye soko kishindane na kilete faida. Haiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, angalia wenzetu sekta binafsi wanavyotafuta ma-*CEO* wao. Mtu anayekuja kuwa *top* pale *Vodacom* ni mbobevu; kama siyo moja kwa moja kwenye *telecoms* basi ni mbobevu kwenye biashara. Iweje sisi tuchukue mtu labda na A zake za chochote twende tumwambie asimamie pale Kiwanda cha Ngozi. Kile kiwanda tumewekeza zaidi ya bilioni 150, tena za kutoka huko *NSSF* kwa kushirikiana na magereza; kinatakiwa kiajiri watu 10,000, lakini na kwamba mpaka leo kimeajiri watu 250 wanaleta *pair* mbili, *pair* tatu. Kila mara ninasema kwenye makongamano kuwa siyo kabisa nia ya kuanzisha ile; siyo kusudio kabisa; na kwa njia hiyo hatutakaa tufikie *full capacity. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama basi tumeamua hatuajiri hivyo basi tuuze *share* kama tulivyouza *TPC* Kiwanda cha Sukari, tulivyouza *TBL*, tulivyouza *share* Benki ya *NBC* na maeneo mengine ambayo yanafanya vizuri; lakini vinginevyo tutabaki hapa miaka 10 inapita. Haiwezekani umempa mtu kiwanda kinatakiwa kitengeneze vitu kiuze halafu unalipa mshahara kwa ruzuku, yeye ni nini kitamfanya ahakikishe kinafanya kazi? Ni nini kitamsukuma? kwa sababu mwisho wa mwezi mshahara utakuja, wake na wafanyakazi wengine, auze asiuze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nimesimama hapa sekta ya ngozi iko katika hali mbaya. Ngozi inayopatikana Tanzania leo kwa zaidi ya 95% inauzwa *West Africa* kama chakula, yaani tumefikia hapo, kwamba ngozi inayotoka Tanzania 95% inauzwa *West Africa* kama chakula. Vile viwanda vichache vinavyo-*operate* kama hii *Mo ternaries* hawapati tena ngozi, kwa sababu kama inauzwa kama chakula uchunaji wake nao hauna umakini tena, wanaacha nyama kidogo na nini, hali ambayo haifai tena kwa utengenezaji wa *leather product*. Sasa *industry* nzima inakufa kwa sababu hata viwanda tulivyonavyo haviangalii kule ambako tunaweza kupata *raw materials.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana haya mashirika; kwa mfano twende kwenye shirika lingine; tunaongelea leo *Tanzania Postal Corporation*. Leo watu wana-*struggle* kutuma vifurushi mikoani kwa kupitia mabasi; na una vifurushi vitatu vinne unataka kutuma mikoa tofauti; kwa mfano uko pale Moshi; cha kutuma Dodoma unakwenda Shabiby, cha kutuma Mwanza sijui unakwenda kwenye basi lingine. Kwa nini *Tanzania Postal Corporation (TPC)* isilete mtu wa kibiashara, hata kama tutamchukua kule *DHL* au sehemu nyingine, aje mbobevu wa kutuma vifurushi, achore namna tutakavyokuwa tunatuma vifurushi nchi nzima ukiwa kwenye mkoa wowote siyo vifurushi mpaka mizigo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DHL* leo wana ndege na wana meli kwa sababu ya vifurushi tu. Tunaanza na vifurushi vidogovidogo kama bahasha, tunatoka kwenye bahasha tunakwenda mpaka kwenye kontena za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *TRL* wameanza hizi treni; tuhakikishe kwamba *TPC* wanaweza kuwa na behewa moja kwa sababu tumekwisharuhusu. Kwanza yenyewe ni ya Serikali, lakini tumekwishabadilisha sheria tukasema sekta binafsi iwezekeze kwenye reli; waweke behewa la mizigo pale, linavutwa, tunahakikisha kwamba kuna *network* ya mizigo. Kwa kufanya hivyo shirika hili litatengeneza faida, litatengeneza ajira na litaleta fedha Serikalini. Leo tumekaa, lina ofisi nchi nzima zingepigwa vumbi watu wanaenda pale hata kuzi-*repair* haiwezekani hiyo *network* kuitumia. Tena tunaweza kuanza kwa kutumia *network* ya sekta binafsi ya usafiri kwanza kabla ya kununua usafiri wetu. Tusafirishe magazeti, tuseme Posta itafanya na magazeti yafike *on time*. Wewe ukisha-*produce* kitu chako kiko Moshi kiko sehemu gani kitafika sehemu yoyote. Leo tumeweka watu wanalipwa kwa ruzuku tunasema shirika linaleta hasara ilihali *market* iko *fluctuated.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwa mfano Kiwanda cha Sukari Mkulazi; nilishawahi kusema, kimeanza juzi, ni cha Serikali. Ninataka niwaambie, si kwamba ninakiombea mabaya, lakini kwenye ushindani kwenye soko tutarudi kulekule tulikokuwa *TPC* mpaka tutafute tena wabia tuwape. Sasa kabla ya kusubiri huko

ni kwa nini sasa tusianzishe mchakato wa kuhakikisha kwamba tunapata *competitor* mwingine ananunua *share* zetu pale anasimamia vizuri tunapata gawio ajira zinakuwa vizuri; tutasubiri mpaka hatua ambayo imeleta hasara mwaka wa kwanza, mwaka wa pili na mwaka mwaka wa tatu ndipo turudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TTCL* ilimzaa leo *Airtel*, imetoka *TTCL;* lakini wakati *TTCL* ina hiyo miundombinu yote kipindi hicho chote zimeshakuja kampuni ngapi, zimeanza zimefanikiwa na zinafanya kazi sisi *TTCL* hasara tu, hasara tu; sasa hivi na mkongo wa Taifa hasara tu, hasara mpaka lini? Kwa nini tusitafute namna ya kuuza *share* au ya kutafuta watu *competent* wafanye kazi, wawekewe malengo ya muda ili waweze kuleta faida? Kwa hiyo kuna maeneo mawili hapa, moja njia mbili za kufanya aidha tutafute watu ambao ni *competent* wapewe uhuru wanaotakiwa na siyo wapewe hela. Yale mashirika yana *resources,* yana *assets* yanaweza kwenda benki yakakopesheka, yakafanya kazi, yakajilipa mshahara, yakaajiri watu na yakaleta faida Serikalini. Hilo linawezekana, wala hatuhitaji kuwe na watu ambao wataleta labda teknolojia ya ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie, mashirika yote tuliyobinafsisha wanaokuja kufanya kazi pale *top* ni wachache sana, wengine wanaajiri haobhao watu wetu ndiyo wanafanya kazi huku chini na matokeo ni mazuri. Pale *top* tu kwenye *brain* wanakuja *brains* wachache hapo juu lakini huku chini ni watu wetu wanafanya kazi, wanasimamiwa vizuri na *productivity* inaongezeka, faida inaongezeka na kwa kweli tutaona tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shida ya ajira Serikali haiwezi kuajiri watu wote Tanzania, haya mashirika yanaweza kuajiri na yakaisaidia sana Serikali. Hilo ni eneo moja ambalo nimesema niliongelee kwa undani

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ripoti hiyo hiyo ya *PIC* ukiangalia mahesabu na mwenendo wa Benki ya Maendeleo ya *TIB* yanatia hasira. Hela iliyowekwa namna ilivyokopeshwa, hasara ilizopata, wakati huo huo ukiangalia upande wa pili *balance sheet* ya *CRDB* faida za kutosha tena *commercial,* ukiangalia *NMB* kuna faida, hadi benki ndogondogo zinatengeneza faida.

Ukijiuliza ni nini? Maana yake ni yaleyale, *competence* ya watu tunaoweka. Kingine ambacho wameweka ambacho amekiongelea ndugu yangu Richard Sanga ni kuingiliwa kwenye maamuzi na Serikali. Kwenye mikopo kampuni haijakidhi vigezo, simu inatoka Serikalini, huyo apewe huo mkopo haraka ni mdau. Hatuwezi kutoboa hata tufanyeje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIB* ilitakiwa iwe mkombozi leo wa sekta binafsi kwa kuwasaidia hasa wazawa, lakini *TIB* imekuwa uchochoro; hela zinaingia pale zinatoka watu wanakopeshwa. Ninakumbuka *industry* ya maua pale Arusha tukahakikisha na pale Namanga i-*operate* masaa 24, maua yataenda nje kwa ajili ya *horticulture industry*. Tumechukua hela tumezitupa pale tumefunga kila kitu, mashamba yako pale hayana kazi; lakini ni kwa sababu ya kuingiliwa katika maamuzi. Tungeweka *CEO* kwa *qualifications* anazotakiwa kuwa nazo tukampa na malengo leo *TIB* ingekuwa ina mtaji mkubwa na ingekuwa imewasaidia Watanzania wengi sana na ingeendelea kusaidia watu wengine na sekta binafsi ingeendelea kukua kupitia kwa Benki ya *TIB*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata kama tunafikiria kuwekeza hela pale tui-*operate based on merit* na siyo vinginevyo na Serikali ikae pembeni kabisa wala isiingilie kwenye maamuzi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kusema tu, yaani tukishafanya hivyo; ikiwa bodi inakaa mwezi wa kwanza, wa pili wa tatu hakuna matokeo, vunja; wako Watanzania wengi wenye akili wamesoma na wenye uwezo. *CEO* amekaa pale umempa malengo miezi mitatu, minne, mitano mwaka haja-*deliver* aondoke. Tuwe na *contracts based,* tutaweka watu *competent* na tutapata matokeo mazuri sana kwenye maeneo haya; vilevile tutamsaidia sana Rais katika kupunguza tatizo la ajira na tutapata hela nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke kwenye *PIC* niende *LAAC,* hapa napo kuna shughuli nzito sana, lakini hii ripoti yote inatakiwa kila kipengele tukifanyie siku yake ndipo tutaitendea haki; lakini hatuna hiyo *luxury* ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kipengele namba 2:3:3 ambapo tunaongelea manunuzi, sura ile ya 410, pamoja na usimamizi wa mikataba. Hapa ndipo kwenye shimo la kuchomea fedha za Serikali. Kitengo cha Manunuzi kwenye *Local Government* na usimamizi wa mikataba kwenye *Local Government* ambapo tunapeleka zaidi ya 70% ya fedha yetu ya maendeleo ya bajeti kuu. Hapa ndiyo mahali ambapo fedha zinapotelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tumeshindwa kabisa kutengeneza mfumo ambao unajua kwamba bati la *ALAF gauge* hizi bei hii kwenye mkoa huu, kwenye wilaya hii na hii? Simenti bei hii na hii na vitu vingine, tukawa tuna *fixed price,* angalau kwenye haya *materials* yanayotumika sana badala ya kuacha watu wana-*tender* tu? Tunasema tu anaye-*tender* wa chini na wa juu sijui ndiyo apewe. Tumeshindwa kweli kujua bati la *ALAF,* bati la nje, bati la hivi na *gauge* hizi, tuka-*map* nchi nzima tukajua bei zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vitu *basic* tukajua kabisa bei zake tukahakikisha tuna-*control* hata kwenye ujenzi tu. Kama nchi tunashindwa hiyo? Tena tukaweka *emphasis* kwenye *local products,* kwamba bati la *ALAF* hapa, bati linalotengenezwa Tanzania na bati linalotoka hapa bei yake kutoka hapa Dar es Salaam mpaka Kigoma. Kutoka kule Mbeya mpaka Arusha tujue bei. Tunapopeleka mradi tayari tuna *estimate* sisi wenyewe mkononi; hilo linashindikana, mpaka tunaacha Sera ya Manunuzi inatuumiza na kesho inatuumiza wakati sisi wenyewe tupo kila siku? Ninafikiri hatuitendei haki hii nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus, malizia.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nilikuwa nina mambo mengi sana hapa kwenye suala la manunuzi, lakini niishie hapo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia basi hata angalau wakurugenzi kwenye miradi tuwe na kipimo cha kuwapima. Tusisubiri tu mradi umeshashindikana tunaenda tunatoa taarifa. Kuwe kuna vipimo kwamba mradi huu umalizike kwa muda, *value*

*for money,* lakini kila kitu kiende kwa wakati, tunashindwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo tunaweza tukiamua wenyewe na sisi ndiyo tutakaotunga sheria siyo wengine. Hatuwezi kumlalamikia mtu yeyote hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. Sasa namwita Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Pia, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati kwa kuweza kuwasilisha hizi Taarifa kwa umahiri. Pia, nawapongeza Wajumbe wa Kamati ambao wametumia muda mwingi, akili, roho na utashi wao kushughulikia na kuchambua hizi Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kamati zinatutesa kwelikweli; hizi taarifa za Kamati zinakuwa ni nyingi, taasisi zinakuwa ni nyingi na hoja zinakuwa ni nyingi mpaka wakati mwingine unajiuliza twende na lipi tuache lipi. Kwa hiyo, walichokiweka hapa ni sehemu ya makubwa ambayo hizi Kamati zimejadili. Kujadili ni hatua moja lakini hatua ya pili inayosikitisha ni kuwa tunaleta taarifa hapa mara kwa mara, lakini utekelezaji wake hauonekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu hususan ya *PAC* tumekuwa tukileta masuala kadha wa kadha ambayo mwaka hadi mwaka yanajirudia. Nianze kwa kutoa wito. Moja kati ya kitu ambacho tunaweza tukafanya kama Bunge la sasa kabla halijahitimishwa, msingi ambao tunaweza kuujenga ni kusimama kwa pamoja tukaiazimia Serikali na kutaka ilete utekelezaji wa uteuzi wa Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi ya taasisi kwa maana ya Bodi za Rufaa za Kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani tangu asubuhi Wajumbe wamekuwa wakichangia. Kila aliyekuwa anachangia kibwagizo kimekuwa habari ya *TRAB* na *TRAT*. Mara nyingi tumekuwa tunakuja tukijadili habari ya mapato ya Serikali.

Tumekuwa tukijadili habari za ukusanyaji wa kodi na mambo kadha wa kadha, lakini hakuna wakati tumekuja kujadili hapa tukasema *estimate* za *TRA* wameweza kukusanya kwa 100%. Kila mwaka bajeti yake ni *deficit,* lakini bajeti ambayo imekuwa na nakisi imekuwa na maelezo ya kwa nini haya mambo au kwa nini bajeti haiwi 100% na hicho ndicho utakachoanza kusema. Miaka hadi miaka Bunge hili katika Kamati ya *PAC* limekuwa likieleza uundaji na ukamilishaji wa hizi Bodi za *TRAB* na *TRAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya *random sampling* nikatafuta Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya *PAC* iliyoleta kwenye hili Bunge tarehe 30 Juni, 2014, mpaka tarehe 30 Juni, 2025, ikatoa maelekezo mahususi ikisema; "Ili TRA iweze kufikia lengo la kukusanya mapato kwa 100% ni lazima rufaa za mashauri ya kodi zilizopo kwenye mabaraza kwa muda mrefu ziundwe Kamati ili ziweze kushughulikia hayo masuala ya rufaa ya kodi." Walienda mbali zaidi wakasema, "Haya mashauri ambayo yapo yana thamani ya zaidi ya shilingi trilioni sita" Huo ni mwaka 2014 na 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikajiuliza, changamoto imekuwa ni kushauri au changamoto imekuwa ni wanaoshauriwa? Nikaitafuta taarifa ya Kamati hiyo hiyo ambayo ilikuwa inaongelea mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021, iliongelea nini kuhusu masuala ya mashauri ya kikodi. Ilieleza hivi; "Kumekuwa na mashauri ya muda mrefu na nakisi ambayo imekuwa ikijitokeza *TRA* imechangiwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kutoshughulikia ipasavyo kwa madeni ya kodi pamoja na uwepo wa mashauri ya kodi ambayo hayajatolewa uamuzi katika vyombo vya sheria kama Mahakama, Bodi ya Rufaa za *TRAB* na Baraza la Rufaa ya Kodi – *TRAT.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hapa ni hesabu za Serikali za mwaka 2021 wakiongelea habari za kuundwa kwa hizi bodi. Pia nikatafuta taarifa nyingine ambayo Bunge lako au Kamati Tukufu ya Bunge hili iliwasilisha taarifa zake, ambapo ilikuwa ni Novemba 2023. Hii ni taarifa au ni hesabu za Serikali za Mdhibiti na Mkaguzi ya Juni 2022, akaeleza yaleyale akasema; nasoma ukurasa wa 12; "Kuchelewa kusajili mapingamizi ya kodi *(Tax objection)* yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 40 na katika mapitio ya *register*

za kodi katika mikoa mbalimbali...” alisema mikoa ya kikodi 137. Hiyo nimefanya *sampling* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ambayo tunaiongelea hapa, Kamati yetu imerudia maagizo yaleyale. Sasa nataka niulize swali, changamoto ni sisi tunaoshauri au changamoto ni wanaoshauriwa lakini nikaamua nijipe *homework*. Mbona mara nyingi tumekuwa tukiongelea kutotimia kwa wajumbe wa hizi bodi. Tatizo ni nini? Wanapaswa kupatikana Mbinguni au wanapaswa kuwa wa rangi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikabidi niifuate sheria sasa ambayo imetengeneza hizi bodi ambayo inaitwa *the tax revenue Appeals Act Cap. 408,* nimechukua *revised* ya 2019. Inaeleza kutakuwa na kuundwa kwa hizi bodi; akasema bodi ya kwanza itakuwa ni *TRAB;* katika Bodi ya *TRAB* akasema kutakuwa na *chairperson* na huyo *chairperson* atateuliwa na Waziri. Huyu Waziri tunashinda naye hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waziri anataka kutuambia hii nchi ya watu milioni 62 haikupata yeyote ambaye anaweza kuwa Mwenyekiti wa Bodi? Pia, sheria hiyo hiyo ikaeleza sifa za anayeweza kuwa Mwenyekiti wa Bodi. Tena sifa ni nyepesi tu, *an experienced lawyer* (mwanasheria mzoefu) lakini mtu ambaye ana uzoefu na sheria ya kodi anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika akaeleza makamu mwenyekiti atapatikanaje na halikadhalika wajumbe, lakini imekuwa muda mrefu hapa tunaongelea. *TRA* wanatuambia hizi bodi za rufaa hazina wajumbe. Hakuna Mwenyekiti lakini Waziri anashinda hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukatoka nikaenda kwenye *Tax Revenue Appeals Tribunal (TRAT)* anayepaswa kumteua mwenyekiti ni Mheshimiwa Rais. Hapa nirudi palepale. Tumekuwa tukiongelea pengine majukumu ni makubwa sana ambapo pengine Mheshimiwa Rais hakumbushwi vizuri, au pengine kuna watu wanapaswa kumkumbusha kuhakikisha anaweza kuteua hawa wajumbe kwa lengo lilelile la kuhakikisha thamani ya fedha,

lakini kiasi cha fedha tunachopaswa kukipata kinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu wameeleza ukiongelea shilingi trilioni 10 katika nchi ambayo *TRA* inakusanya shilingi trilioni 22 mpaka 23, lakini unaongelea shilingi trilioni 10 zimekuwa *withheld*, ni vitu ambavyo havieleweki. Sababu nyingine ameieleza Mbunge aliyemaliza hapa kwamba ni kukosa bajeti. Hivi unawezaje ukawa na mashauri ya shilingi trilioni 10 halafu unaongea kwamba hatuna bajeti ya kutengeneza au ya kuhudumia zile Mahakama za Rufaa za Kikod, yaani ni vitu ambavyo huwezi ukavifikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Bunge kama linataka ku-*set precedency* na kama linataka kutendea haki Watanzania, tuiagize Serikali na tuipe *time frame*. Kamati zote kwa maana hizi taasisi zote *TRAB* na *TRAT* ziwe na wenyeviti na ziwe na wajumbe na zianze kufanya kazi, yaani lazima zifanye *full functioning* ili tuweze kuondoa hii kero ambayo imekuwepo kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda ni mchache lakini natambua kwamba kama mkiamua kuokoa hizi fedha ambazo zimeshikiliwa, lakini mnachopaswa kujua hizi fedha pia ni za wafanyabiashara. Unavyochukua shilingi trilioni 10 uka-*withheld* yule mfanyabiashara hawezi kupata hizo fedha na wewe huwezi kupata hiyo fedha. Unamuathiri kiasi gani kwenye biashara yake? Hicho kitu pia tunapaswa tujiulize. Tunataka ku-*achieve* nini? Hayo ni masuala ambayo yanahusu usimamizi wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mfupi naomba nieleze kitu kingine ambacho kimekuwa kikijitokeza kwenye taarifa zetu ambacho katika taarifa ya sasa tumeongelea bidhaa zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi hususan kutofungwa ving'amuzi, *Electronic Seals (e-seals)*. Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali alifanya *sampling* tu, alikuta ni zaidi ya shehena 200 *plus* ambazo zilikuwa zina *seal* ambazo hazi-*detect*. Ni kwa kiwango gani tumepoteza fedha nyingi ambazo tulipaswa kuchukua ambazo zingeweza kuwasaidia wananchi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, mmoja wetu ameeleza hapa vizuri tu, kwamba kulikuwa na shehena ya mafuta na hiyo naweza kurejea kwenye taarifa mbalimbali miaka hadi miaka. Kamati zako Tukufu zimekuwa zikieleza juu ya kukosa ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazopita nchini, tume-*cite* zaidi ya lita milioni moja ambazo zilisafirishwa zikionekana kwamba ni shehena inayoenda nchi nyingine, lakini ni mafuta yaleyale yamepita na yakatumika hapa nchini. Hiyo ni hoja imejengwa na Kamati kwa zaidi ya miaka mitano mfululizo; naweza nikawasomea hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ni kwamba, wanaosimamia hizi mamlaka wanaelewa au hawaelewi? Kama wanaelewa tunaweza sote kuamini kwamba hawanufaiki na hiyo *loophole* ambayo wanaitengeneza? Hiyo inatutengenezea mazingira ya kuamini wakati tukipambana kukusanya fedha za vyoo kama alivyoeleza mama yetu, wakati tukikusanya fedha za *barrier* na wakati tukihangaika na fedha ndogo ndogo, fedha nyingi zinapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ila siyo kwa umuhimu, niongelee upotevu wa maji katika halmashauri, kwa maana ya Mamlaka ya Maji Tanga. Wamesema upotevu wa maji kwenye hiyo halmashauri au mamlaka ya maji ni zaidi ya 34%. Hiyo zaidi ya 34% ni kinyume cha matarajio ambapo inapaswa kuwa 20% tu ambayo imepangwa na *EWURA*. Ina maana maji mengi yanapotea ambapo maji wanaita *nonrevenue water* yanapotea na ni maji ambayo yangeweza kuwasaidia wananchi wetu wa Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa mara nyingi nikija hapa kuongelea na kulalamika juu ya upatikanaji wa maji, lakini kuna halmashauri na kuna mamlaka zinaweza kupoteza maji mengi kwa kiasi hicho, ambapo sasa hayo maji yalikuwa na thamani zaidi ya shilingi bilioni tano. Pia, kwenye halmashauri hiyo hiyo kuna taasisi mbalimbali za umma ambazo hazilipi ankara zao za maji licha ya kwamba tumewapitishia bajeti ya kulipa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni machache, lakini tuamue; kupanga ni kuchagua. Tunaweza kulia mwaka hadi mwaka lakini

tukiamua kufanya maamuazi kama hii habari ya *TRAB* na *TRAT* tunaweza kuleta mabadiliko na Bunge letu likakumbukwa kwamba tuliwahi kuweka msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia. Sasa namwita Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, baada ya hapo Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi niweze kuchangia katika hoja za hizi Kamati zetu tatu, *LAAC, PIC* na *PAC*. Naendelea kuipongeza Serikali yangu kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kuifanya hasa kazi ya uwekezaji. Tumeona kuna miradi mikubwa imeendelea kufanyika na hii yote ni kwa malengo na matumaini kwamba ni kwa ajili ya kusaidia Taifa na kusaidia wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani huwa nashindwa kufahamu kwamba Serikali inafanya juhudi za kuwekeza, lakini Serikali hiyo hiyo inafika mahali inaamua kuua kile ilichokiwekeza. Leo tunaangalia miradi mikubwa kama huu Mradi wa Reli wa *SGR*. Ni mradi mkubwa ambao tunatarajia kwamba utasaidia sana nchi yetu kwanza, katika kukuza uchumi; lakini bado tumeshindwa kufanya tathmini ya mradi wa reli ile iliyokuwepo ile ya mkoloni tuliyoikuta na tumeshindwa kufanya tathmini ya reli ya *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndiyo maana nasema Serikali inakuwa na nguvu za kuanzisha, lakini baada ya muda sijui inakata tamaa ile miradi inakufa. Leo tunafurahi sana kuwa na Bomba lile la Hoima (Uganda – Tanga), lakini tunalo Bomba la Mafuta la *TAZAMA* na tunayo Reli ya *TAZARA*. Sasa hiyo yote ni miradi ambayo ni ya Serikali ambayo ilipaswa kutupatia uchumi mzuri lakini tumeiua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza unasikia tuko hapa tunasema tunataka tupeleke reli mpaka Kalemie kwa ajili ya kwenda ku-*tap* mzigo wa *DRC,* lakini tumesahau kwamba reli kama hii ya *TAZARA* mpaka leo hivi tunavyozungumza ni reli

ambayo inaenda mpaka Zambia na mpaka *DRC* tena kule katikati. Ni kwa sababu gani imeshindwa kuwa na tija? Sababu ni ndogo tu kwamba, Serikali imeshindwa kuzipa *private companies* ili ziweze kuendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ule uendeshaji wa Serikali unasababisha ile reli yote pamoja na mabilioni yote ambayo sasa tunaendelea kulipa, ni reli ambayo inaonekana kama haina tija. Bahati nzuri wewe unatoka mikoa hiyo ya Njombe ambako ndiko *TAZARA* inapita, ni shehena ngapi za mizigo ambazo zinasafirishwa kwa njia za barabara wakati reli ipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo lipo bomba ambalo linaenda mpaka kule Zambia Kapiri Mposhi, lakini leo ni malori mangapi ambayo yanatembea kwenye barabara hiyo? Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba hata hii miradi ambayo tunazungumza kwamba tunaanzisha hizi reli nyingine na tunaanzisha mabomba mengine mwisho wa siku Serikali siku ikimaliza inafika mahali sijui tuseme inatafuta kuyaua au inafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko mjumbe amezungumza hapa Kiwanda hiki cha Sukari tulichonacho hapa cha Mkulazi. Ni kiwanda kimeanza lakini, leo ukienda ukiangalia tayari wameanza kushindwa kuuza sukari.  Mwisho, kitakuwa kama Kiwanda cha *TPC* ambacho kilikuwa ni kiwanda chetu tukafika mahali tukaona tumeshindwa kukiendesha tukawapa *private company* kimeweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama tunataka kwenda yapo mambo ambayo lazima sasa tukubaliane kwamba tumejifunza na tulifanya makosa. Sasa tufike mahali tuseme sasa basi na tuone namna nzuri ya kwenda. Namna pekee ya kuweza kwenda ni hata yale mashirika ambayo tumeyaanzisha ambayo leo yanatuliza humu ambayo tunaendelea kuyapa fedha. Shirika kama *TTCL* ambalo wakati tunaanzisha hata ule Mkongo wa Taifa tulisema sasa sisi tumeula, lakini bado ni shirika ambalo halifanyi vizuri. Halifanyi vizuri kwa sababu mbili tu; kwanza tunaendesha sisi wenyewe. Vilevile, hata wale watendaji tunawachagua kwa

kuangalia sisi wenyewe kwamba tumchague nani, lakini siyo nani anaweza nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati mwingine lazima tuchukue maamuzi magumu kama tunataka kwenda mbele, kwamba mashirika yote watendaji wote wa mashirika tufike mahali tuseme hivi; nani anataka kuendesha shirika hili? Waombe na washindanishwe. Wakiomba na wakishindanishwa maana yake tutawapa malengo. Mtendaji yule ameshindwa kufikia malengo aondoke na mtu mwingine aingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara wakati mwingine unaweza ukakuta mtu ni mwadilifu, lakini ni kwamba hana zile *technique* za biashara. Kwa hiyo, utakapomweka pale kwa sababu umedhani kwamba ulivyomwangalia ni mwaminifu au mwadilifu ukimweka kwenye biashara inamweka nje. Ndiyo maana bado tunaendelea kujiuliza kwamba tutakaa kila leo tunaendelea kuzungumza na tunafanya makosa na madeni yanaendelea kuongozeka. Tunafanya *investment,* lakini mwisho tunashindwa ku-*recoup* kile tulichokiweka. Kwa hiyo tuna kila aina ya sababu tufike mahali tuchukue maamuzi magumu na mojawapo ya maamuzi magumu ndiyo kama hayo. Kwanza kwa mashirika yetu yote, yale ambayo Serikali inaendesha tuyabinafsishe, wawekezaji wayaendeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba wakati mwingine Serikali yetu inaua yenyewe viwanda na mashirika. Nami nitatoa mifano, pale Musoma Mjini kulikuwa na kiwanda cha *MUTEX*, ni kiwanda ambacho Serikali yenyewe ilishindwa kukiendesha, baadaye ikampa mwekezaji. Mwekezaji amekiendesha kiwanda baada ya miaka michache na yeye akaanza kusuasua. Hivyo basi, Serikali ikaamua kumnyang'anya mwekezaji, hata kabla haijatafuta namna gani kiboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka siku Serikali imnyang'anye mwekezaji, wale watu hawajalipwa maslahi yao mpaka leo, kiwanda kimekufa mpaka kesho. Kwa hiyo, haya yote ni mambo ambayo Serikali inayafanya na wakati mwingine unasema labda inafanya aidha kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Siyo hivyo tu, leo hawa watu tumesikia kuna madai ya wakandarasi na

wazabuni. Hawa wakandarasi hawa sisi wenyewe ndiyo tunafika mahali tunalia tunasema jamani eeh! Hivi inakuwaje Watanzania tunashindwa kupata wakandarasi wazuri? Tunashindwa kupata wakandarasi wazuri kwa sababu tunawaua wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi amejitahidi, ametengeneza mtaji, amefika mahali anaanza kuwa kama wakandarasi wakubwa, huyo huyo akishapewa kazi akimaliza miaka minne, miaka mitano hajalipwa. Zile fedha kakopa benki, huyo mkandarasi atakua? Hawezi kukua, hata wazabuni halikadhalika. Unakuta hao wazabuni ndiyo wanaolisha shule zetu, akienda akishakuwa na deni kubwa hawezi kulisha anaachwa hapo anaendelea kudai miaka na miaka, tunatafuta mzabuni mwingine. Sasa, kutokana na hali hiyo ndiyo maana wakati mwingine tunasema labda hii Serikali yetu ina-*regulate* yenyewe, ikiona tunataka kukua inaamua kutufubaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunasema lazima tufike mahali tuchukue maamuzi magumu. Nami nilifika mahali nikajaribu kufanya utafiti kujua, hivi kwa nini mkandarasi wa nje yeye anapewa riba, lakini wa ndani hapewi riba? Kumbe sababu yenyewe ni rahisi tu. Mkandarasi wa ndani akienda kuomba riba kwa sababu amefanya huduma anaambiwa wewe tunaku-*blacklist*. Kwa hiyo, anafika mahali hawezi kuomba kwa sababu anaogopa atakosa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, labda tufike mahali tuweke sheria moja kwa moja ieleweke kwamba jamani eeh; mkandarasi yeyote anayefanya kazi akisha-*raise certificate* na hakuweza kulipwa, basi apewe riba kama ambavyo yule mkandarasi wa nje anavyopewa. Tofauti na hapo maana yake ni kwamba tutaendelea kujiua sisi wenyewe na hii nchi ni yetu wote na hao watu ni wa kwetu ambao tunatarajia wafike mahali wawe wakubwa na watakapokuwa wakubwa, basi waweze kutusaidia katika kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia tu kwamba, hata leo tukitaka, hii reli ya *TAZARA* ni kati ya reli ambayo inaweza ikatusaidia tukapeleka mzigo mkubwa sana Congo, *DRC* tena kwa gharama nafuu na ikaweza kujiendesha tukaweza kupata

Uchumi, lakini hilo litawezekana pale tu tutakapoibinafsisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hili bomba la mafuta lililopo bado linaweza kufanya kazi nzuri kwa sababu ukiangalia kimahesabu, badala ya kubeba mafuta lita 30,000 usafirishe mpaka *DRC,* ni suala tu la *pump,* ina-*pump* mafuta yanatoka hapa mpaka Zambia, lakini tumeshindwa kulitumia kwa sababu gani? Ni kwa nini tushindwe kufanya tathmini ya kuona kwamba hivi, haya mawazo ambayo tulikuwa nayo toka huko na tukaweka *investment* mbona sasa tumeshindwa kuyaendeleza? Bado tunakuwa na mawazo ya kuanzisha vitu vingine ambavyo ni vilevile na mwisho wa siku vitafika mahali na vyenyewe vitakufa na baadaye tutarudi kule kule *the business as usual*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru Mheshimiwa Mathayo. Sasa namwita Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa ambaye atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipa nafasi. Kipekee ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kuzipongeza Kamati hizi tatu zilizofanya kazi kwa niaba yetu, Kamati ya *LAAC*, *PAC* na *PIC*. Najua walikuwa na kazi nzito ya uchambuzi, kwa hiyo ni lazima tuwapongeze kwa sababu wamesoma ripoti zao kwa niaba yetu ambao tulikuwa kwenye Kamati nyingine. Kwa hiyo, hongera sana kwao kwa haya ambayo wameyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninachukua nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Mwaka jana nikichangia ripoti hii ya *CAG* kwenye Kamati hizi tatu niliongelea habari ya kuangalia jinsi ya kubadilisha *recruitment style* hasa kwa Wakurugenzi wa Mashirika yetu ya umma. Nikawa nimesema ni bora wangepewa miaka mitano wawe na mikataba ili iweze kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka *somewhere* mwaka huu Mheshimiwa Rais akiwa anaongea na Wakurugenzi wa Mashirika haya ya Umma na Wenyeviti wa Bodi, Ikulu, ni kama aligusia hilo jambo na akalitolea maelekezo kwamba sasa ifike hatua wakurugenzi wa mashirika haya ya umma waanze kupatikana kwa ushindani. Vilevile, akagusia kwamba kwa Wenyeviti wa Bodi tumwachie kwanza aendelee mwenyewe, nadhani maelekezo yalishatoka. Kwa hiyo, tunategemea Mchechu ambaye anasimamia huko angeanza kuliangalia hili; na Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji yuko hapo, ili tuweze kwenda kwenye hiki kitu ambacho Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamekiongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunaongea hivi? Tunaongea hivi kwa sababu ripoti hizi tunapozipata kila wakati yanarudiwa mambo yaleyale, yanachosha. Kama binadamu unajisikia vibaya unapokuwa unaongelea jambo lilelile huenda saa nyingine unawaza unadharaulika au ni nini? Wakati nachangia mwaka jana nilisema, kama Waheshimiwa Wabunge na hata Mheshimiwa Rais mwenyewe anarudishwa kikaangoni kila baada ya miaka mitano iko haja pia watumishi wa umma wasiwe na *comfort zone*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna rafiki yangu mmoja aliwahi kuniambia kwamba mbwa mwenye uhakika wa milo mitatu anapoteza uwezo wa kuwinda; hata panya akipita mbele yake kwa sababu ameshiba hawezi kumkimbiza. Kwa hiyo, hii ndiyo inayotokea, watumishi wa umma wame-*relax* mno, *permanent and pensionable* inawachanganya. Yaani mtu akishajua nimeingia huku ni mpaka miaka 60 *sometimes* wanapoteza *focus,* siyo kusema hawana uwezo. Wakati wanaajiriwa wanakuwa na uwezo mkubwa, ni wasomi, vyeti ni vizuri, lakini *as long as* kila anapoenda *comfort zone* inamzunguka, *there are times* haoni kitu cha kumsumbua maana anajua nikikosea hapa nitahamishiwa kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, jana ilisemwa habari ya Halmashauri ya Biharamulo hapa kwenye ripoti ya Kamati ya *LAAC*. Sasa ilivyosemwa Biharamulo tu nikashtuka, ya mwisho? Unajua kama Mheshimiwa Mbunge upo humu ndani Bungeni,

unasikia wilaya yako ndiyo ya mwisho kwenye kukusanya mapato, imefeli kukusanya, *of course* kwanza inauma na unahisi kuna kitu hakipo sawa na unachanganyikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamenipigia simu sana, wananiambia kama tunarudi huko tena tunaelekea wapi? Lakini nilipokuwa nasoma ripoti hii nikaona tulitakiwa tukusanye *3.5 billion shillings* ila sisi tumekusanya *2.26 billion shillings* ambayo ni sawa na 65%. Nikarudi nikasema nami ni Mbunge, halmashauri hii ni yangu, hatujawahi kuwa na bajeti ya *3.5 billion shillings* tangu nimeanza Ubunge. Bajeti yetu ya 2022/2023 ninayo hapa, ilikuwa ni *2.931 billion shillings* na kipindi hicho shule za *A-level* Biharamulo ninazo nyingi, tulikuwa tunakusanya ada ya watoto wa *form five* na *six* inaingia kama sehemu ya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa wamesamehe ada ilifanyika *restructuring*, hii barua ya Katibu Mkuu wa wakati huo, Profesa Shemdoe akimwandikia *RAS* wa Mkoa wa Kagera kwamba ada zimeondolewa kwenye mapato ya halmashauri. Kwa hiyo, halmashauri yetu imeshuka, tukatoka *2.9 billion shillings* tukaondoa shilingi milioni 291 ya ada ya sekondari tukaja *2.6 billion shillings* ambapo kwenye makusanyo yetu ya mwaka ule 2022/2023 tulikusanya *2.7 billion shillings* sawa na 103%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana makadirio yetu yalikuwa *3.0 billion shillings*, kwa mara ya kwanza tumefika bilioni 3.41 tukakusanya bilioni 3.19, maana yake tukaja 99.28% hatukufika 100. Mwaka huu ndiyo tuna bilioni 3.3, sasa tumeshakusanya shilingi milioni 928 tuna 27.37%. Sasa, nikawaza bilioni 3.5 mwaka 2022 ilitoka wapi? Ndiyo hapo ninaporudi kwenye suala la watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba hapa unisikilize kwa makini maana jana wakati ninauliza swali la nyongeza niliuliza habari ya watumishi. Nikasema Biharamulo kuna wimbi la watu kuondoka pale halmashauri, zinakuja barua zinatoka TAMISEMI moja kwa moja watu wanakuja pale wanasema nimehama, madaktari, walimu, watu wanaondoka pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kimoja tulijiuliza, *system* ya ajira pia lazima tuiangalie upya. Biharamulo haiwezi kuwa *stepping stone* ya watu kuja kujifunza kazi, baada ya miaka mitatu wakaondoka. Tunakuja tunakutana na watu wenye miaka 58, wakija kustaafu pale, yaani wanajifunza, wanapanda vyeo, wanaondoka wakifika miaka 58 tena wanarudishwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DT* wangu aliyeandaa ripoti hii aliyekuwepo hapa siku anafika tulimkataa, kaja pale kustaafu, yaani amekuja pale amebakisha miezi anastaafu. Matokeo yake hata ripoti aliyoiandaa unauliza hii *3.5 billion shillings* aliitoa wapi? Alimsainisha mkurugenzi na mwenyekiti, wamesaini lakini hatujawahi sisi kukusanya *3.5 billion shillings* wala hatukuwa nayo, hata mapato waliyosema tumekusanya ya *2.2 billion shillings* sisi tumezidi tuna *2.7 billion shillings*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, wanatuletea watu ambao wameshaingia kwenye usingizi tayari wafanye kazi na sisi tunaoenda kwa kasi, tunawezana wapi? Ndiyo maana nikasema, kwenye haya ambayo yanafanyika twende mbele turudi nyuma tutengeneze *system* ya kupata ajira ya miaka mitatu mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai, hata mashirika haya ya watu binafsi kuna mtu anafanya kazi kwa mkataba wa miaka mitatu mitatu mpaka anafikisha miaka 60, lakini anajua kabisa *after three years* nitakuwa *re-evaluated*, sijafanya kazi vizuri naondoka, kila mtu atakuwa na bidii. Ndiyo maana ndugu zangu sisi wote ni wanasiasa ni Waheshimiwa Wabunge hapa, yanayoendelea majimboni kwetu tuko hapa tunajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa Wenyeviti wa CCM, kwenye vijiji na vitongoji tumeona moto ulivyokuwa unawaka kule. Ile kazi ni kazi ya kuwatumikia wananchi, lakini tumeona ushindani ulivyokuwa mkubwa. Kwa nini ushindani mkubwa? Wamerudi kuomba idhini ya watu wanaowachagua wakitegemea wataongoza baada ya miaka mitano watarudi tena. Wote tuko humu, mwakani tutakuwa tunarudi kwa wananchi, umefanya vizuri watakuhukumu, umefanya vibaya watakuhukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema hata hawa watumishi, tuangalie *system*, tuko na *system* zetu za ajira lakini siyo Biblia wala Qurani, turudi nyuma turudi mbele lazima ifikie hatua tuone jinsi ya kwenda sawa. Mtu hawezi, atupishe katikati ya safari siyo hawezi, unamhamisha Biharamulo unampeleka Kyerwa; Hawezi, unamtoa Kyerwa unamrudisha Ngara; hawezi, baada ya miaka mitano unamrudisha Biharamulo tena, *what are we doing*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wamemaliza vyuo wako nje huko hawana kazi, leteni damu changa wapeni miaka mitatu mitatu, wameshindwa wanapisha, hivyo hivyo, hatuna hasara. Mawaziri kila siku Mheshimiwa Rais anabadilisha hapa lakini umeshasikia kazi inasimama? Umeshindwa hapa, umepigwa chini kaja mwingine, maisha yanaenda. Hatuhitaji *experience* hapo, uwezo wako wa kichwani wakishaku-*interview* utakutosha kukupa kazi kwa sababu hata haya mashirika wanapobadilisha wakurugenzi kila siku shirika halisimami. Mkurugenzi atahojiwa anakuwa na *job description* ile ajira itakuwa ya kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukinipa miaka mitatu hata TAMISEMI hawana haja ya kuhangaika kumhamisha kwamba amalize miaka mitatu yaani akifeli anaondoka mwenyewe. Siyo unamleta kwetu Biharamulo anakaa kwenye mafunzo miaka mitatu anaanza kuandika barua TAMISEMI anaomba ahame. Mnatuletea mwingine mafunzoni, akimaliza anaomba ahame. Yule aliyekuja mwenyewe kwa miaka mitatu anakuwa anajua kabisa kazi yangu ni hii huko ninapotaka kwenda kuna mwingine ana mkataba siwezi kwenda tena. *So, let's see this*, tufanye *re-structuring* tuweze kwenda sawa, hiyo ilikuwa ni moja kwa upande huu wa ajira za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia pia ripoti ya *PAC*, ninawapongeza sana kwa haya mambo ambayo wameyasema. Hata wakurugenzi hawa wa mashirika ya umma ambao tunasema Mheshimiwa Rais alisema waanze kupatikana kwa ushindani. Tuwape ushauri tu, kipindi wanaingia kwenye ushindani, kuna mashirika yetu ya umma hasa hivi viwanda wana mitambo ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mtu una mashine ya mwaka 1980 imeshakuwa *phased out*, mnakaa nayo mnaing'ang'ania. Inapoharibika *spare* moja tu unaweka *special order* kwenye kiwanda, kile kiwanda kitakuchaji *almost* nusu ya bei ya mashine mpya. Kwa nini haya madude mengine tusiyaondoe kwa sababu *efficiency* yake ni mbovu? Hayawezi kuzalisha, ondoa, uza chuma *scrapper,* hapo leta mashine mpya zinazoendana na *speed* ya sasa zifungwe ili ziweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tumezunguka, bahati nzuri wewe ni Mwenyekiti wangu wa Kamati, unaelewa huko tulipoenda. Kuna mashine nyingine ni kubwa kuliko nyumba, uwezo wa kuzalisha haina. Wakati sasa hivi zipo mashine ndogo tu ukibonyeza hapo unaondoka utakuta kila kitu imekufanyia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tuombe hata kipindi tunawaza hivi vyote, lazima tuendane na *system* mpya inavyoenda. Kwa mfano, Serikalini najua wanaendesha magari haya ya *Prado, Prado TXL* sasa hivi yamekuwa *phased out*. *TXL* na *VXL* zote zimekuwa *phased out* kwa sababu kuna hizi *Prado* mpya ambazo wameleta; *Adventure* na *All Rounder*. Sasa, ukija kuangalia vitu vinabadilika, lakini sisi kwenye mashirika tunaenda vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tu kwa kumalizia kwa sababu ni mchangiaji wa mwisho nadhani watanivumilia.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mwaka jana niliongea pia habari ya vile Vituo vya Forodha vya Pamoja vya Nyakanazi na Manyoni. Leo tumeona kwenye ripoti *60%* imelipwa, walishafanya kazi *60%* kwa Manyoni, *50%* kwa Biharamulo, lakini ukiuliza wale

watu zilikuwa ni fedha za *donors*. Wamefanya kazi nusu wameondoka, tunaambiwa wale watu wamefilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua habari ya *URSUS* si ndiyo hivyo? Tunarudi pale pale, kwamba *URSUS* walituletea vitu vya ajabu ajabu hapa kwa sababu ni mkopo baadaye tukaambiwa kampuni ile ilifilisika. Sasa, hatuwezi kuwa tunapopata pesa kama hizi za *donors* tunakuja katikati tunachezewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mtu anafilisikaje alishafanya kazi 50%? Hakulipwa pesa ya kuendelea? Yaani mkandarasi wa Tanzania anapewa 15% anafanya mradi anaumaliza, aliyefanya kazi 60% anafilisikaje? Naomba tuache kutaniana kwenye haya mambo, kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie hapa nisiseme sana, lakini wasidhani sisi tupo hapa kwa ajili ya kucheza. Hawa watu wanaocheza hii michezo lazima ifikie hatua wakome, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana *Engineer* John Ezra Chiwelesa. Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni ndani ya ukumbi wetu ambao napenda tuwatambue.

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, hawa ni watumishi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, Mkoa wa Lindi, hebu tuwaone. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Nadhani mwenzetu ametuonesha mfano, ameita watumishi wa halmashauri yake siku ambapo ripoti zetu zinajadiliwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tumefika mwisho wa wachangiaji tuliokuwa nao jioni ya leo na ninasitisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.35 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 31 Oktoba, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*